# Nipashe

Jumatano Novemba 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581124

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT TZS.1,048,875,802 KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#

## MAKALA MAALUM

**Serikali** yatoa ufafanuzi hali Bwawa la Mtera

UKURASA 4




UKURASA 13



Ndege ya Precision Air iliyopata ajali ikitolewa kwenye Ziwa Victoria katika eneo la Uwanja wa Ndege wa Bukoba, mkoani Kagera jana. **PICHA: ROSE JACOB**

# Manusura ajali ndege asimulia kilichotokea

• **Shujaa** Majaliwa aanza mafunzo, azidi kuoga manoti... *Endelea ukurasa 2 & 3*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### SHAHIDI AWATAJA MBOWE, MNYIKA KUWAVUA UANACHAMA



MBUNGE wa Viti Maalum, Cecilia Pareso, amedai kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia...

## Rais Samia akumbusha fedha za mabadiliko tabianchi

UKURASA 3



Baadhi ya wakazi wa vijiji vya Ng'wang'olo na Nyenze, Kata ya Mwadui Luhumbo, wilayani Kishapu, wakiangalia tope lililovamia makazi yao na kufunika mashamba, visima vya maji na wengine kulazimika kukimbia nyumba zao ili kuokoa maisha yao juzi, baada ya bwawa la Mgodi wa Almasi Mwadui kupasuka. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Tope bwawa mgodi wa almasi lavamia makazi, watu wahama

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA SC: TUTAWASHANGAZA UK.32 **KABWELA** UK.7



Ndugu, jamaa na marafiki wakiaga miili ya wafanyakazi wa MDH katika viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam jana, waliofariki katika ajali ya ndege ya Precision Air. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Manusura ajali ya ndege asimulia kilichotokea

**Na Romana Mallya**

MANUSURA wa ajali ya ndege, Nickson Kawiche, amesimulia jinsi rubani wa ndege ya Precision Air alivyohangaika angani hadi kutua kwenye maji na yeye alivyojiokoa baada ya maji kufika eneo la kiunoni.

Kawiche ambaye ni Meneja Mkaguzi kutoka Shirika la Usimamizi na Uboreshaji wa Huduma za Afya (MDH), katika safari hiyo alikuwa na wenzake saba kati yao watano walifariki dunia na kuagwa jana jijini Dar es Salaam katika shughuli iliyoongozwa na Mganga Mkuu wa Serikali.

Akizungumza baada ya kuaga miili ya wenzake ambao ni Dk. Boniphace Jullu, Dk. Alice Simwinga, Zacharia Mlacha, Neema Faraja na Sauli Epimark, Kawiche alisema haikuwa jambo rahisi kutoka salama.

Anasema kutoka salama ni kudra za Mungu, lakini pia maelekezo ya kutumia vifaa vya dharura waliyopewa awali kabla ya ndege kuondoka Dar es Salaam yalimsaidia.

Alisema kabla ya kuondoka, walitangaziwa na marubani kuwa wataruka kwa umbali gani na hali ya hewa ilivyo kwenye miji wanayokwenda na walielezwa sio nzuri.

Ndege waliyoipanda ilikuwa inatoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza kupitia Bukoba na walipofika Mkoa wa Kagera, walielezwa kwa mara nyingine kuwa hali ya hewa sio nzuri.

"Kwanza kabla hawajatueleza kuwa hali sio nzuri walitueleza matarajio yao ni kutua ndani ya dakika saba kisha watasubiri kwa dakika 20 ndipo wataelekea Mwanza na watatumia dakika 20."

Alisema rubani alipojaribu kutua ndani ya dakika saba za mwanzo alishindwa na kuwataarifu abiria sababu ya kushindwa ni hali ya hewa kuwa sio nzuri, mvua ilikuwa inanyesha na kwamba watajitahidi watue ndani ya dakika 10.

"Walitueleza ikiwa watashindwa watakwenda Mwanza, sikuona kama anakwenda kutua, alizidi kupanda juu zaidi angani na alikuwa akielekea uelekeo wa Misenyi ambako ni mpaka kati ya Tanzania na Uganda, baadaye Muleba wilaya inayopakana na Geita na kurudi mjini na kuzunguka ziwani, akajaribu kutua kwa kuishusha ndege, lakini baadaye alipaa tena.

Baada ya kurudi juu alikuwa anafanya kama alivyokuwa akifanya awali, lakini alikuwa haendi mbali, alizunguka kwenye mwambao wa ziwa, mjini.

"Ndipo akawa anashuka kwa mwendo wa kutua lakini cha kushangaza, sikusikia tairi zikiburuza, nilisikia mshindo mkubwa tu, kama sekunde 30 kwenye kiti nilichokuwa nimekaa maji yalikuwa yameshafika kiunoni.

"Nikafungua mkanda, nikasimama na wakati huo hakukuwa na ishara (sign), injini za ndege zilikuwa zimezima, hata ishara za kwenye mikanda zilizima, kulikuwa hakuna umeme kwenye ndege, ninahisi rubani alizima kabla hajafika chini."

### ALIVYOTOKA

Kawiche alisema alipochungulia nje na kuona uelekeo wa maji, ndipo aliposikia mhudumu akisema, 'nipeni boya bila boya siwezi kufungua mlango.'

"Yawezekana eneo alilokuwa amekaa mhudumu hakukuwa na boya au kutokana na ndege ilivyokuwa imekaa inawezekana liliondoka nafasi yake, hicho kilinikumbusha kuchukua boya langu, nikalichukua nikajifunga.

"Eneo nililokuwa maji yalinifikia kwa haraka na wakati ninawaza nisogee mbele nafsi ikakataa, nikaona bora nisubiri mlango ufunguliwe, kwenye hili niseme, nina mshukuru Mungu sana kwa kunipa utulivu, nilichokuwa nikisikia ndani yangu ndicho nilichokuwa nikikifanya.

"Nilimsikia mtu akifanya maombi kwa ujasiri sana na kutia watu moyo, lakini nilisikia tu kama maneno mawili ya kutambua huyu mtu anaomba kwa ujasiri, yalinifanya niseme ndani yangu kuwa, nimeshaomba na ujasiri niliokuwa nao ni kwamba Mungu amejibu, hali ya utulivu niliyokuwa nayo iliniwezesha nifikirie nini nifanye na nini nisifanye.

Hata nilipokuwa nikitaka nichukue simu, moyo ulikataa, Mungu alikuwa akiniongoza nielekee uelekeo upi, ujasiri ulizidi zaidi baada ya kuangalia dirishani na kuona nchi kavu haipo mbali na namna wale wavuvi wadogo wakiwa na vyombo vyao wakija kwa kasi upande wetu.

Baada ya mhudumu kufanikiwa kufungua mlango wa ndege wakatoka na kuning'inia kwenye ngazi za mlango.

Ni ule mlango wa nyuma ambao abiria huutumia kuingia, pale (mlangoni) tulining'inia kama wale wachezaji wa sarakasi, tulining'inia kama watu 10 au 15, tulikanyagana kwenye mabega na wengine kushika mkono wa mwingine, aliyepata fursa ya kushika chuma ya ngazi akawa anasaidia wengine.

Mmoja alikosa nguvu akaachia, niliamua kuvua boya nililokuwa nimevaa nikamtupia akawa anaelea. Mitumbwi minne midogo ikafika inayoendeshwa kwa makasia, waliokuwa juu yangu wawili tukawapa fursa ya kupanda kwa sababu ningeachia walikuwa hawana maboya wangezama, nilichukuliwa na mtumbwi mdogo kuliko yote, alikuwamo mama na mtoto wake.

Matukio yote hayo mpaka ndege ilipotua vilitokea ndani ya dakika 10 hadi 15.

### MARUBANI/WAHUDUMU

Alisema marubani walifanya kazi kubwa na kama wangewatangazia abiria wavae maboya kabla ya kutua wasingeweza kutoka ndani ya ndege.

"Tusingetoka ndani ya ndege tungekuwa tunabanana mule ndani, kilichosaidia kutoka namna ndege ilivyokaa na ilikuwapo nafasi.

### RUBANI AMPELEKA MHUDUMU NYUMA

Alisema wakati rubani akihangaika namna ya kutua, alimtoa mhudumu mmoja mbele na kumpeleka nyuma akimpa maelekezo.

"Kule nyuma wakawa wawili ninadhani alimpa maelekezo nini anatakiwa kufanya baada ya kutua."

Alisema wengi waliofanikiwa kutoka ni abiria waliokaa siti kuanzia namba nane kurudi nyuma na wale waliokaa namba saba kushuka chini ambako maji yalijaa aliyefanikiwa kutoka ni namba nne pekee.

"Tulichokikosa ni boti na wazamiaji wenye mitungi ya gesi wangeweza kusaidia watu ndani ya ndege na kuwaongezea hewa, hivi vingekuwapo kungekuwa na matokeo makubwa," alisema.

# Tope bwawa mgodi wa almasi lavamia makazi, watu wahama

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WANANCHI wa vijiji vya G'wang'olo na Nyenze, Kishapu mkoani Shinyanga ambao wameyakimbia makazi yao baada ya nyumba, mashamba na visima vya maji kufunikwa na tope baada ya bwawa la mgodi wa almasi Mwadui kupasuka na kusambaza tope katika maeneo yao.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 4:00 asubuhi na kusababisha madhara hayo katika vijiji hivyo ambavyo viko jirani na bwawa hilo.

Pia imeelezwa kuwa kati ya nyumba zilizozingirwa na tope hilo, 13 wananchi wamezingira na hawajatoka, hivyo mipango inafanywa ili kuwaokoa.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wananchi hao walisema walishangaa kuona tope zito linatiririka na kuvamia makazi yao, likitoka kwenye bwawa la mgodi wa almasi wa Mwadui ndipo wakaanza kikimbia kuokoa maisha yao.

Mmoja wa wananchi hao, Tabu Kikuya, mkazi wa kitongoji cha Manai kijiji cha Ng'wang'olo, alisema tope hilo zito lilitapakaa na kuvamia makazi yao, huku mashamba na visima vya maji vikifunikwa.

Naye Tungu Kwinyalija mkazi wa Kijiji cha Nyeze, Kata ya Mwadui Luhumbo, alisema tope hilo limefunika mashamba yake ekari nane na mpaka sasa hajui hatima ya maisha yake pamoja na wananchi wenzake kwa sababu hawana tena mashamba ya kulima mazao.

Kutokana na tope hilo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Manai, Ester Seni, aliiomba serikali kufanya tathmini ya athari zilizotokana na tatizo hilo na kuona namna ya kuwasaidia.

Pia aliomba serikali kutuma timu ya wataalamu kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini tope hilo kama linaweza kuleta madhara kwa wananchi kwa kuwa limetoka ndani ya mgodi, hivyo kuenda kukawa na sumu.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema katika tukio hilo hakuna madhara yoyote ya binadamu kupoteza maisha, zaidi ya mashamba na visima vya maji kufunikwa na tope.

Alisema mpaka sasa nyumba ambazo zimezingirwa na tope ni nyumba ambazo wananchi wameshindwa kutoka na serikali inafanya utaratibu wa kuwatoa pamoja na kuwapatia msaada wa chakula na maji waathirika wote wa tukio hilo.

Pia alisema tayari serikali imeshaunda tume kwa ajili ya kufanya tathmini ya athari ambazo wamezipata wananchi, pamoja na kuja na majibu ya kuona namna ya kuepuka majanga hayo kutokea tena.

Mjema pia alisema alisema tayari wamewasiliana na wataalamu pamoja na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa ajili ya kuchunguza udongo huo kama una athari kwa binadamu.

Alisema mpaka sasa shughuli za uzalishaji wa madini kwenye mgodi huo zimesimama hadi pale serikali itakapojiridhisha kuwapo na usalama.

Naye Meneja Uhusiano Mgodi, Bernard Mihayo, alisema kwa sasa hawawezi kuzungumzia suala hilo kwa kuwa wamekubaliana msemaji wa suala hilo atakuwa mkuu wa mkoa.




Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza katika moja ya mikutano iliyoandaliwa na Benki ya Dunia, kuhusu miradi mbalimbali ya mazingira inayosaidia kupunguza hewa ukaa kwenye mwendelezo wa COP 27, nchini Misri jana. Mkutano huo uliongozwa na Rais wa Benki ya Dunia, David Malpass (kulia). **PICHA: IKULU**

# Shujaa uokoaji apokewa Jeshi la Zimamoto, Uokoaji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SHUJAA Majaliwa Jackson, aliyeibuka kinara wa uokoaji katika ajali ya ndege iliyotokea Jumapili iliyopita mkoani Kagera, amepokewa rasmi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na ameripoti katika Chuo cha Mafunzo Handeni mkoani Tanga.

Kupokewa kwa kijana huyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumpatia ajira ndani ya jeshi hilo.

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa jeshi hilo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACF) Puyo Nzalayaimisi, ilisema Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna Jenerali John Masunga, anaujulisha umma kuwa kijana huyo ameshapokewa.

"Kamishna Jenerali John Masunga anaujulisha umma kuwa kijana Majaliwa Jackson Samweli tayari amepokewa katika jeshi hilo na anatarajiwa kuanza mafunzo muda si mrefu," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema Majaliwa anatarajia kuanza mafunzo ya Zimamoto na Uokoaji pamoja na uaskari katika chuo cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kilichoko Chogo wilayani Handeni, Tanga.

Katika taarifa hiyo pia, Kamishna Jenerali Masunga alitoa shukrani kwa wananchi na wavuvi wote wa mkoa wa Kagera walioshiriki kikamilifu kwenye uokoaji katika ajali hiyo na kusaidia kuokoa baadhi ya abiria.

Majaliwa alionekana shujaa baada ya kuokoa abiria 24 kati ya 43 waliokuwamo kwenye ndege iliyopata ajali kwa kutumbukia katika Ziwa Victoria, hivyo kusababisha vifo vya abiria 19.

Kutokana na kufanya hivyo, serikali juzi wakati wa kuaga miili ya abiria na wahudumu wa ndege waliofariki katika ajali hiyo, ilimtangaza shujaa na kumpatia zawadi ya Sh. milioni moja na baadaye Rais kupiga simu kwamba atampatia zawadi ya Sh. Milioni tatu.

Akizungumza katika Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, baada ya kutangazwa shujaa, Jackson alisema alitamani kuwaokoa watu wengi zaidi katika ajali hiyo lakini alipoteza fahamu wakati akiendelea na uokoaji.

Akisimulia ajali hiyo, Jackson alisema wakati akiendelea na shughuli zake za kuanika dagaa katika mwalo wa kisiwa cha Msila, aliona ndege ikitokea upande ambao haujazoeleka kwa ndege kwenda kutua ndipo akaanza kufuatilia kwa karibu kujua hali hiyo.

"Nilivyoona hivyo, nikajua si kawaida. Baada ya muda mfupi, nikaona ndege imeanguka ziwani, ndipo nikawaambia wenzangu ajali ile pale, tukachukua mtumbwi tukiwa wanne ili tukawaokoe waliomo ndani.

Hata hivyo, alisema walipokuwa wanakaribia eneo la tukio, wenzake walishindwa kuendelea kuogelea lakini aliendelea hadi alipoifikia ndege na kwenda moja kwa moja mbele ya ndege na rubani alimwonyesha ishara kuwa avunje kioo cha mbele kwa kuwa maji yalikuwa yakiingia kidogo kidogo.

Baada ya maelezo hayo, alisema alikwenda juu ya maji kutafuta kitu cha kuvunjia kioo lakini aliporejea alikuta maelekezo ya serikali kwamba asivunje kioo hicho. Baada ya hapo alisema alimwendea rubani na kumweleza maelekezo ya serikali kisha rubani akamwelekeza mlango wa dharura na kuufungua ndipo alipoanza kuwatoa watu waliokuwamo na kuwapeleka ufukweni.

### AOGA MANOTI

Kijana Jackson pamoja na kuzawadiwa fedha na serikali pamoja na Rais Samia, taarifa zaidi zilibainisha kuwa taasisi ya GSM Foundation imetangaza kumzawadia Sh. milioni tano kutokana na kazi aliyoifanya.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Gharib Said Mohammed, licha ya kutoa fedha hizo, alikaririwa na kituo kimoja cha habari kuwa yeye binafsi pia atamzawadia Sh. Milioni moja kutokana na ushajaa aliouonyesha.

# Samia akumbusha fedha mabadiliko tabianchi

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amezitaka nchi zilizoendelea kutimiza ahadi ya kutoa fedha kwa nchi maskini kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema fedha hizo zitawasaidia kupata teknolojia za kisasa na kutekeleza miradi ya kukabili mabadiliko ya tabianchi na changamoto zake.

Rais Samia amezitaka nchi hizo kuongeza juhudi za kutimiza malengo waliyoahidi ya kuzuia uzalishwaji wa hewa ya ukaa, ili isiendelee kuleta madhara yatakayoshindwa kuzuilika na yanayoathiri nchi zinazoendelea kwa kiasi kikubwa.

Alisema hayo jana wakati akihutubia Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP27), jijini Sharmel El Sheikh, nchini Misri ikiwa ni mara ya pili tangu achaguliwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwaka jana Rais Samia alihutubia mkutano kama huo wa wakuu wa nchi zaidi ya 120 uliofanyika nchini Scotland.

Alisema Tanzania kupitia Makubaliano ya Paris imeweka mikakati ya kitaifa ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kufikia mwaka 2030 na utekelezaji wake unahitaji Dola za Kimarekani bilioni 19.2 (Sh. trilioni 14.3) pamoja na uwezo wa teknolojia.

Aliitaja baadhi ya mikakati kuwa ni kuzuia uzalishwaji wa hewa chafu kupitia uchumi kati ya asilimia 30 hadi 35 ifikapo mwaka 2030, pamoja na kujenga na kupanua mtandao wa usafiri wa haraka unaotarajia kupunguza zaidi ya tani milioni 900 za kaboni inayozalishwa kila mwaka.

Vilevile, alisema nchi hiyo imedhamiria kuongeza matumizi ya vyanzo vya nishati mbadala kutoka asilimia 60 mwaka 2015, hadi 80 mwaka 2025 na kuhifadhi ekari milioni 48 za misitu ambayo ni asilimia 55 ya ardhi yote ya nchi.

Kwa mujibu wa Rais Samia, Tanzania imejipanga kupanda miti milioni 200 kila baada ya miaka mitatu huku akiomba uwapo uwiano wa bei za kaboni duniani, ili kuzalisha rasilimali kutoka kwa njia hiyo.

Alisema sayansi imeonesha uhusiano wa moja kwa moja kati ya ustawi wa binadamu na mazingira na uchumi unaotegemea asili unaweza kuwa na manufaa, ikiwa kutakuwa na maono ya pamoja na fursa zitakazoleta mabadiliko ya kimuundo.

Alisema ucheleweshaji wa hatua madhubuti za kushughulikia upotevu na uharibifu wa mali unalazimisha nchi zinazoendelea kutumia vyanzo vyao vya mapato kujenga uchumi unaostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha idadi kubwa ya watu ya wanaotegemea kilimo kiuchumi inaendelea kuwapo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
07/11/2022

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 09/11/2022 kampuni ya **LIUHE INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Gari zenye vipimo vikubwa kutoka Dar es Salaam kuelekeaa Rusumo Gari hizo zenye namba za usajili: **T330DLF/T932DMY, T942DMY/T905DMP na T665DLY/T904DMP**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   I. **T330DLF/T932DMY** **Urefu-18m Upana -4m, Kimo-5**
   II. **T942DMY/T905DMP** **Urefu-18m Upana -4.65m, Kimo-5**
   III. **T665DLY/T904DMP** **Urefu-18m Upana -4.4m ,Kimo-5**

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaam hadi Rusumo Kupitia Dodoma** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

117137702

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Serikali yatoa ufafanuzi hali ya Bwawa la Mtera

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

***KWA siku mbili mfululizo, Oktoba 29 na 30 mwaka huu, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu hali ngumu ya kimaisha inayowakabili wakazi wa Mtera mkoani Dodoma kutokana na uhaba wa samaki kwenye Bwawa la Mtera linalotegemewa kiuchumi na wakazi wengi wa eneo hilo.***

Nipashe iliyokuwa imepiga kambi kwa siku kadhaa kwenye kambi za wavuvi zilizoko Mtera, ilishuhudia baadhi ya wavuvi wametelekeza familia zao na kutimkia mikoa ya Singida na Tabora kunakopatikana samaki.

Mkurugenzi wa Uvuvi, Emmanuel Bulayi, katika ufafanuzi mahsusi kwa Nipashe kuhusu suala hilo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, alisema jana kuwa uharibifu wa mazingira, matumizi yasiyofuata utaratibu pamoja na mabadiliko ya tabianchi unaathiri uzalishaji wa samaki kwenye Bwawa la Mtera.

### MABADILIKO TABIANCHI

Bulayi alisema kupungua kwa maji kunakotokana na upungufu wa kiasi cha maji yanayoingia kwenye bwawa hilo kutoka kwenye mito ya Great Ruaha, Little Ruaha na Kisigo.

Alisema upungufu wa maji kwenye mito hiyo umesababishwa na uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vyanzo hivyo na mabadiliko ya tabianchi.

Alibainisha kuwa bwawa hilo lina ukubwa wa kilomita za mraba 660 na wastani wa kina cha maji cha mita 6.2.

"Kiwango cha maji hutofautiana kwa mwaka kulingana na kiasi cha mvua katika msimu. Bwawa hili lipo katika mikoa ya Dodoma na Iringa. Katika Mkoa wa Dodoma bwawa linazungukwa na wilaya za Chamwino na Mpwawa. Kwa Mkoa wa Iringa bwawa linapakana na Wilaya ya Iringa Vijijini.

"Bwawa la Mtera linazungukwa na kata saba zenye vijiji 17 vya Halmashauri za Iringa (9), Mpwapwa (3) na Chamwino (5). Bwawa lina jumla ya mialo 26 ambayo hutumika katika shughuli mbalimbali za uvuvi ambapo mialo 12 ipo Iringa Vijijini, mialo sita ipo Mpwapwa na mialo minane ipo Chamwino," alifafanua.

Mkurugenzi huyo alisema bwawa lina kambi za wavuvi 30 ambazo ziko maeneo ya Mandela, Kambona, Kichangani na forodha ya boti (Kijiji cha Mapera Mengi).

### HALI YA UVUVI

Mkurugenzi huyo alisema zana mbalimbali za uvuvi hutumika katika Bwawa la Mtera zikiwamo nyavu za makila, kokoro, kimia, mishipi na ndoano (migonzo).

"Zana ambazo hutumika kwa asilimia kubwa ni nyavu za makila. Hata hivyo, umiliki wa vyombo katika bwawa hilo ni wa mtu mmoja mmoja.


"Bwawa lina vyombo vya uvuvi 998, ikiwa vyombo 461 vilivyoko Iringa Vijijini, 153 Mpwapwa na 384 Chamwino. Samaki wanaopatikana katika bwawa hilo ni perege, mchena na kambare. Wengine ni ngarara, ngogo, sulusulu, mkunga, ngobero, mbapala, ndua (ningu), vitoga na kimbumbu," alibainisha.

Hata hivyo, Mkurugenzi huyo alisema samaki wanaopatikana kwa wingi ni aina ya perege ambao hupatikana kwa asilimia 96 kulinganishwa na samaki wengine ambao hupatikana kwa kiwango kidogo.

Bulayi alisema uzalishaji wa samaki katika bwawa hilo unatoa ajira zaidi ya asilimia 70 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi katika vijiji vinavyolizunguka.

Mwenendo wa uzalishaji wa samaki katika Bwawa la Mtera kwa kipindi cha miaka miwili kwa mujibu wa sensa ya uvuvi iliyofanyika katika bwawa mwaka 2021 ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:

**Mwenendo wa Uzalishaji wa Samaki Bwawa la Mtera**




Mkurugenzi huyo alisema wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa hutoa leseni za uvuvi, ushuru wa biashara ya samaki na faini kama vyanzo vya mapato ya serikali.

"Takwimu zinabainisha kwa mwaka 2021, jumla ya tani 4,123.23 zenye thamani ya Sh. bilioni 23.21 zilivunwa katika Bwawa la Mtera ikiwa ni sawa na asilimia 1.2 ya mavuno ya uvuvi katika maziwa, bahari, mito na mabwawa yote yenye shughuli za uvuvi.

"Jumla ya vyombo vya uvuvi 998 vilirekodiwa wakati wa sensa ya uvuvi iliyofanyika mwaka 2021 katika Bwawa la Mtera. Matokeo ya sensa yalionesha kuwa asilimia 90 ya vyombo vilikuwa aina ya mitumbwi ya mbao na asilimia 10 ni mitumbwi ya injini za kupachika," alisema.

Alisisitiza takwimu hizo zinathibitisha kuwa bwawa hilo linaendelea na shughuli za uvuvi.

### MIUNDOMBINU YA MASOKO

Bulayi alisema katika bwawa hilo, soko la samaki liko katika Kijiji cha Migori, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ambalo kwa sasa wavuvi wanalitumia kuuza samaki.

"Hata hivyo, miundombinu ya kuhifadhi samaki kama vyumba vinaendelea kuboreshwa. Shughuli nyingine zinazohusiana na masuala ya uvuvi katika Bwawa la Mtera ni pamoja na uandaaji, uchakataji, uhifadhi na uuzaji wa mazao ya uvuvi, kazi ambazo hufanywa na wanawake kwa asilimia 85," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema uchakataji hufanyika kwa njia mbalimbali zikiwamo ukaushaji wa samaki kwa moshi kwa kutumia matanuru ya asili, ukaushaji wa samaki kwa jua kwa kutumia vichanja pamoja na kukaanga samaki kwa mafuta na kusambaza sehemu mbalimbali kwa ajili ya kujipatia kipato na kuendesha maisha yao ya kila siku.

Sambamba na shughuli za uvuvi, Bulayi alisema wananchi wanaoishi kando mwa bwawa hilo wamekuwa wakifanya shughuli mbalimbali zikiwamo za kilimo cha mazao, ufugaji, biashara ya samaki, utengenezaji wa boti za uvuvi na shughuli za bodaboda kwa ajili ya kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao ya kila siku, kitu ambacho kimepunguza nguvu ya uvuvi katika bwawa.

### SHIDA ZILIZOKO

Mkurugenzi huyo alisema matokeo ya sensa ya uvuvi iliyofanyika mwaka 2021, yalibainika masuala mbalimbali ikiwamo kupungua kwa idadi ya wavuvi kutoka 2,369 mwaka 2014 hadi kufikia 1,738 mwaka 2021, sawa na kupungua kwa asilimia 27.

"Wilaya ya Chamwino ilikuwa na idadi kubwa ya wavuvi 769 sawa na asilimia 44, ikifuatwa na Iringa Vijijini 652 sawa na asilimia 37.4 na Mpwapwa 319 asilimia 18.3.

"Wakati wa sensa, wavuvi walieleza kuwa wamehama kutoka Mpwapwa na Iringa Vijijini kwenda Chamwino kufuatia hali nzuri ya uvuvi katika Wilaya ya Chamwino.

"Hata hivyo, tathmini ilionyesha wavuvi wa Bwawa la Mtera wana tabia ya kuhamahama kufuata samaki wanakopatikana. Kupungua kwa idadi ya wavuvi kulichangiwa na wavuvi kuhama kwenda vyanzo vingine vya maji kama vile Chimedeli na Hombolo vilivyo karibu na bwawa hili," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuongezeka kwa idadi ya wavuvi wanaotumia boti za injini za kupachika ni ishara ya kuimarika kwa teknolojia ya uvuvi kutoka kutumia mitumbwi ya asili inayotumia kasia.

"Aina za zana za uvuvi ambazo hupendelewa zaidi na wavuvi hazijabadilika sana. Kwa mfano, mwaka 2014 kulikuwa na Ringnets 438, lakini kwa sasa idadi imepungua hadi kufikia sifuri.

"Idadi ya zana haramu kama vile kokoro imepungua kwa asilimia 70 kutoka 493 zilizoonekana kipindi cha nyuma hadi kufikia 150 kwa sasa. Kupungua kwa zana haramu kulichangiwa zaidi na juhudi za serikali za kuondoa zana haramu katika bwawa hilo ambazo ziliratibiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi mwaka 2019-2021.

"Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 imeweka mazingira ya kutowabana wavuvi kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine iwapo wanafuata taratibu zilizoko katika eneo la sehemu husika. Hivyo, kuhama kwa wavuvi kutoka Mtera kwenda eneo lingine ni suala la kawaida," alisema.

### UCHAFUZI WA MAJI

Mkurugenzi huyo alisema uchafuzi wa maji unasababishwa na shughuli za kibinadamu kama ukosefu wa vyoo kwenye mialo, mabirika ya kunyweshea mifugo, shughuli za kilimo (viuatilifu) ndani ya eneo la bwawa maji yanapopungua, pembezoni mwa mito inayojaza Bwawa la Great Ruaha, Little Ruaha na Kisigo na maeneo ya hifadhi ya bwawa.

Pia alisema upo uchafuzi wa mazingira unaotokana na utupwaji ovyo wa mifuko ya plastiki huku baadhi ya wananchi wakitegemea shughuli zinazoharibu mazingira katika kujipatia chakula na kipato kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya familia.

Alitaja shughuli hizo ni uchomaji wa mkaa, ukataji wa miti kwa ajili ya mbao na kilimo na ufugaji ndani ya bwawa na kando ya mito inayoingiza maji kwenye bwawa na kuanzishwa kwa vijiji ndani ya maeneo ya hifadhi.

### MIKAKATI YA WIZARA

Mkurugenzi alitaja jitihada hizo ni kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi kwa utoaji elimu kwa wavuvi kuhusu matumizi ya nyavu halali na kudhibiti uuzaji na matumizi ya zana haramu.

"Kutoa elimu kwa wafugaji na wakulima juu ya kuzingatia kanuni bora ya kilimo na ufugaji na kuimarisha uwezo wa kufanya utafiti wa uvuvi kulingana na mahitaji halisi kwa kupitia taasisi za utafiti.

"Wizara pia inahamasisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kwa kuhamasisha jamii ya wavuvi katika kuanzisha na kuimarisha vikundi vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

"Wizara inaimarisha ushirikishwaji wa wadau wote katika kulinda, kuendeleza na kuvuna kwa njia endelevu rasilimali za uvuvi, kuweka miundombinu inayotakiwa kwenye mialo ikiwamo vyoo, soko, mizani na meza, eneo la kupimia samaki na vifaa vya kusafirishia samaki na kuanzisha viwanda vidogo vya kuchakata samaki," alisema.

Mkurugenzi huyo pia alisema wizara itaendelea kulinda, kusimamia na kutunza rasilimali za uvuvi kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyoko.

## HABARI KITAIFA

### Wafukua kaburi, wanyofoa viungo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATU wasiojulikana wamefukua kaburi la Neema Mlomba (26) wa Kijiji cha Luteba, Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe ambaye alifariki dunia kwa matatizo ya uzazi na kisha kunyofoa baadhi ya viungo vya mwili wake na kuondoka navyo.

Baadhi ya viungo vilivyonyofolewa kwenye mwili wa mwanamke huyo ni ulimi, moyo, kiganja cha mkono wa kulia, titi la kulia, mdomo na jicho la kulia.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kabla ya kufikwa na umauti, mwanamke huyo alifika katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya kitengo cha Wazazi Meta, kwa ajili ya kujifungua.

Homera alisema kwa bahati mbaya mwanamke huyo alifariki dunia Novemba 5, mwaka huu, wakati akijifungua ingawa mtoto aliyezaliwa alipona na yuko katika hospitali hiyo chini ya uangalizi wa madaktari.

Alisema mwili wa mwanamke huyo ulichukuliwa na ndugu zake na kwenda kuzikwa kijijini kwao Luteba Novemba 6, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Homera, asubuhi ya Novemba 7, mwaka huu, kaburi lililozikwa mwili wa marehemu lilikutwa limefukuliwa na mwili ukiwa nje ya kaburi umenyofolewa baadhi ya viungo.

"Tukio hili la kufukuliwa kwa mwili wa marehemu na watu wasiojulikana linaonekana lilifanyika usiku wa manane wa kuamkia Novemba 7, mwaka huu. Asubuhi wananchi walikuta kaburi hilo likiwa limefukuliwa na baadhi ya viungo kunyofolewa," alisema Homera.

Alisema tukio hilo linahusishwa na imani za kishirikina, ingawa mpaka sasa watu waliohusika na ukatili huo bado hawajafahamika.

Mkuu huyo wa mkoa aliliagiza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa haraka ili kuwabaini watu walifanya tukio hilo ili wachukuliwe hatua za kisheria.

# Ajali barabarani ilivyopoteza maisha ya watumishi sita Halmashauri Kiteto

**Na Jaliwason Jasson,** KITETO

WATUMISHI sita wa idara ya afya na mmoja idara ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, wamepoteza maisha katika ajali baada ya magari mawili kugongana uso kwa uso.

Ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 11:46 jioni katika Kitongoji cha Napiligunya, Kijiji cha Kimana, Kata ya Partimbo kwenye barabara ya Kiteto - Handeni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, alisema jana kuwa gari lenye namba za usajili T.323 DWP aina ya Landcruiser Prado TX, ambalo mmiliki wake bado hajajulikana, lilikuwa linatoka Handeni mkoani mkoani Tanga kwenda Dodoma likiendeshwa na Method Mariki (55), liligongana uso kwa uso na gari la kubeba wagonjwa (Ambulance), yenye namba za usajili SM 5117 aina ya Landcruiser.

Alisema gari hilo la wagonjwa ni mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto katika Kituo cha Afya cha Sunya, lilikuwa linaendeshwa na dereva Juma Mbaruku (45).

Kamanda Katabazi alisema gari hilo lilikuwa linatoka Kibaya, makao makuu ya wilaya ya Kiteto kwenda Sunya na kusababisha vifo vya watu sita waliokuwa katika ambulance hiyo.

Katabazi aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Muuguzi wa Kituo cha Afya Sunya, Joseph Bizuku (36), Daktari wa kituo hicho cha afya, Edward Makundi (47), Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Asamatwa Sunya, Kidd Said (36), muuguzi wa kituo hicho, Selina Nyimbo (31) na mfanyakazi wa maabara wa kituo hicho, Catherine Thadei (31).

Kwa mujibu wa Katabazi, kati ya vifo hivyo, kimoja kimetokea katika Hospitali ya Benjamini Mkapa na vingine vilitokea papo hapo.

Alisema majeruhi katika ajali hiyo ni watano ambao ni Ibrahim Selemani (71) mkazi wa Makuyuni Korogwe, ambaye aliumia kifua na amelazwa Hospitali ya Wilaya ya Kiteto, Method Mariki(55) dereva na mkazi wa Sinza, Dar es Salaam, aliyevunjika mguu wa kulia na amepelekwa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma.

Wengine ni Mbaraka Shaban(44) mfanyabiashara na mkazi wa Kimara, Dar es Salaam aliyeumia kichwa na amelazwa Hospitali ya Kiteto, Juma Mbaruku(45) dereva mkazi wa Sunya amevunjika miguu yote na amepelekwa Benjamini Mkapa, Nickson Muhongwa (36), daktari mkazi wa Sunya aliyeumia kifua, kichwa na mbavu amepelekwa Hospitali ya Benjamini Mkapa.

Kamanda alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa Toyota Landcruiser Prado TX, kutaka kulipita basi lililokuwa mbele yake bila kuchukua tahadhari, hali ambayo ilisababisha kugongana uso kwa uso.

Pia alisema katika ajali hiyo, alikuwapo mtoto wa miezi tisa ambaye ametoka mzima.



Mwenyekiti wa Kamati ya Amani na Jumuiya ya Maridhiano ya Viongozi wa Dini na Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, akizungumza na waandishi wa habari jijini humo jana, wakati akitoa pole kwa niaba ya viongozi wenzake kutokana na ajali ya ndege ya Shirika la Precision Air iliyotokea mkoani Kagera. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Shahidi awataja Mbowe, Mnyika kuwavua uanachama

**Na Grace Gurisha**

MBUNGE wa Viti Maalum, Cecilia Pareso, amedai kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na Katibu Mkuu, John Mnyika, wanashiriki katika vikao vya Baraza Kuu na Kamati Kuu ambayo iliwavua uanachama.

Pia amedai kuwa maneno ya Mnyika aliyozungumza mbele ya waandishi wa habari kabla ya kikao cha Kamati Kuu ndiyo yaliyowahukumu na kusababisha wasipewe haki ya kusikilizwa.

Pareso alidai hayo jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam, alipokuwa akihojiwa na Wakili wa CHADEMA, Peter Kibatala, kutokana na kiapo chake alichokiwasilisha katika kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama.

Pia alidai ana uhakika Mnyika alihusika katika kikao cha Kamati Kuu Novemba 27, 2020 kwa sababu yeye ndiye mtendaji mkuu wa masuala yote ya chama na kwamba Novemba 24, 2020 alifanya mkutano na waandishi wa habari na kutoa maneno ya kuwahukumu yeye na wenzake 18.

Alidai kuwa waliofanya uamuzi katika kamati hiyo ndiyo hao hao waliokuwapo kwenye Baraza Kuu ambalo walilikatia rufani kutokana na uamuzi uliotolewa na wao kutokupewa nafasi ya kusikilizwa.

Kuhusu uthibitisho kama Mnyika alikuwapo kwenye kamati kuu, Pareso alidai nyaraka inayoonyesha kwamba alishiriki katika kikao hicho ni kiapo chake alichokiwasilisha mahakamani pamoja na Katiba ya Chadema.

Pia alidai kuwa barua ya wito wa kuitwa kwenye Kamati Kuu aliipata Novemba 25, 2020 kwa njia ya WhatsApp kwamba anahitajika kwenye kikao hicho Novemba 27,2020.

Alidai kuwa kwa sababu CHADEMA waliamua kumtumia wito huo kwa njia hiyo na yeye alimjibu Mnyika kwa barua yake ya Novemba 26, 2020 kwa njia ya WhatsApp kwa kumwomba amwongezee wiki moja kutokana na mazingira aliyokuwapo.

Pareso alidai kuwa kipindi anapata wito huo alikuwa mkoani Dodoma na CHADEMA walikuwa wanajua hilo lakini katika kiapo chao kinzani hakikueleza kwamba wakati wanatumia wito huo alikuwa wapi.

Pia alidai Mnyika kwa nafasi yake, alikuwa na uwezo wa kutoa ahirisho la kikao hicho kwa niaba ya Kamati Kuu ili na yeye apate muda wa kuhudhuria kwa sababu yeye ndiye kila kitu ndani ya chama.

Akiendelea kuhojiwa na Kibatala, Pareso alidai suala lao halikuwa na ulazima wa kikao cha dharura cha Kamati Kuu hadi wao kutokupewa nafasi ya kusikilizwa na kuongeza kuwa ni kweli kiapo kinzani cha CHADEMA kinapinga yeye kuteuliwa, lakini katika hali ya kawaida hawezi kujiteua.

Mdee na wenzake 18 walifungua kesi Julai 21, mwaka huu, katika Mahakama Kuu dhidi ya CHADEMA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wakipinga uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kuwavua uanachama, Mei 11, mwaka huu.

Katika shauri hilo, wabunge hao pamoja na mambo mengine, wanaiomba mahakama ipitie mchakato na uamuzi wa CHADEMA wa kuwafukuza, kisha itoe amri tatu.

Wabunge hao wanaomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza na amri ya zuio dhidi ya Spika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kutokuchukua hatua yoyote mpaka malalamiko yao yatakapoamuriwa.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Mamlaka mnawasaidiaje wasiopata huduma ya maji*

**KILA** siku kilio ni maji, hasa kwa wakazi wanaoishi maeneo ambayo hayapati huduma hiyo.

Kuna watu wana zaidi ya mwezi hawajapata maji ya bomba na tangu taarifa rasmi ya mgawo wa maji ilipotangazwa, hawajawahi kukumbukwa.

Hali inasikitisha sana kwa sababu baadhi ya watu inawabidi kuamka usiku mwingi kuyavizia pengine yatatoka, lakini wanaambulia patupu.

Ingawa kuna baadhi ya maeneo katika Jiji la Dar es Salaam, hayajaguswa na tatizo hilo, lakini maeneo mengine limekuwa tatizo la kudumu.

Zaidi ya wiki mbili zilizopita Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipokwenda Kigamboni, alitoa matumaini ya kusambazwa kwa maji yanayozalishwa eneo hilo yaweze kusaidia maeneo yenye shida hiyo, lakini utekelezaji wake haujaonekana.

Sehemu zingine maji yanaweza kutoka nyumba jirani tena usiku wa manane, lakini kwa msukumo mdogo ambao hauwezi hata kujaza ndoo moja ya lita 20. Nyumba nyingine hayajawahi kutoka kabisa.

Wakati Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, akitangaza rasmi kuwapo kwa mgawo wa maji katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, alitahadharisha mgawo huo usiwe wa upendeleo. Wananchi wameshaanza kulalamika kuwa kuna upendeleo.

Inaeleweka kuwa vyanzo vinavyozalisha maji vinaupungufu mkubwa kutokana na ukame uliosababishwa na kukosekana kwa mvua.

Pia, inaeleweka hilo ni tatizo la kimazingira ambalo hata mamlaka zinazosimamia huduma hiyo ziko nje ya uwezo wao, lakini zitafutwe njia mbadala kuwanusuru wale ambao hawapati kabisa maji.

Kuna watu wanaoishi maeneo ambayo nguvu ya kusukuma maji imeongezwa ili mabomba yote yaweze kutoa nishati hiyo, kwanini kwenye maeneo kama ya Boko ambako yanatoka kwa nadra baadhi ya nyumba tena yasiyokuwa na nguvu yasiongezewe nguvu hiyo hata kwa siku moja ili watu wajaze kwenye matangi yao ya akiba na kuondokana na adha hiyo?

Haiingii akilini kuona baadhi ya maeneo maji yanafunguliwa hadi kupotea ovyo, huku sehemu zingine yakikosa huduma hiyo kwa zaidi ya mwezi sasa.

Tafadhali, suala hili liangaliwe ili kuwanusuru watu na adha hiyo. Ikiwezekana hata magari ya kusambaza maji yapelekwe kwenye maeneo yenye shida hiyo wanunue na kuwa na uhakika wa kupata majisafi na salama.

Tatizo hili ni la nchi nzima na linatoa funzo inapopatikana mvua ya kutosha la kuhifadhi maji yaweze kusaidia wakati wa kiangazi.

Maombi kwa waamini wa dini zote ni muhimu ili Mwenyezi Mungu asikie kilo na kushusha mvua.

Ukiangalia baadhi ya maeneo mbalimbali nchini hali inasikitisha kutokana na ukame ulivyokithiri na kusababisha mimea na wanyama kufa.


Hali hii inatoa fundisho kwa watu kuacha kufanya uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo ili kuchoma mkaa na shughuli zingine za kibinadamu.

Maji ni uhai, bila huduma hiyo chakula kitakosekana, njaa itatawala na matokeo yake ni vifo. Inashuhudiwa katika nchi nyingine hali hiyo ilivyoathiri mifugo na wanadamu.

Katika kukabiliana na tatizo la maji uwekwe utaratibu mzuri wa kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo muhimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com






Na Golden Kisapile, TUDARCO

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Tuondoe dhana potofu ili tufanye kilimo chenye tija*

**"KILIMO** ni uti mgongo wa uchumi wa taifa." Ni kauli inayoasisiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, akihamasisha umma kukipenda kilimo na kujizatiti kwenye uzalishaji mashambani.

Kilimo ni hazina kwa taifa kwa sababu huchangia kwa kiasi kikubwa mapato, fedha za kigeni kwa mfano kilimo cha korosho kina mchango mkubwa kwenye pato la taifa na uchumi wa nchi hii.

Kuna kilimo cha mwani kinachofanyika Zanzibar na zama hizi kilo moja imefikia Shilingi milioni 1.5. Ni habari njema kwa wakulima.

Kuna mengine mengi kama kahawa, mbaazi, alizeti, ufuta ambayo ni sehemu ya mazao lukuki ya chakula (mafuta) na biashara yanayoongeza mapato ya nchi na ya wakulima.

Tanzania ina ardhi kubwa yenye rutuba na mabonde yanayoweza kufanikisha kilimo cha umwagiliaji ambayo yanafaa kuzalisha chakula na biashara na mengine mengi kuanzia mtama, mihogo, mpunga, mahindi na ngano wakati ya biashara ni pamoja na pamba, korosho, kahawa na vanila.

Wizara ya Kilimo inatoa rai kwa Watanzania kujihusisha na kilimo, kwa sababu ni sekta yenye tija kwa taifa tena ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na kwamba sehemu kubwa ya ardhi takribani asilimia 90 hutumiwa na wakulima wadogo ambao wengi kati yao ni wanawake.

Ni sekta inayotoa ajira kwa asilimia 65.5 na kuchangia kwa asilimia 29.1 ya pato la taifa, aidha asilimia 30 ya soko la nje imejaa mazao yake wakati asilimia 65 ya malighafi za viwanda zinatoka kwenye kilimo.

Suala la ajira linahusisha watu kujiingiza kwenye mnyororo wa thamani kama kulima, kusafirisha, kuchakata, kufungasha na kuweka kwenye maghala hadi kuwafikishia walaji mezani.

**Kuendelea kudhani kuwa kilimo ni cha watu maskini kunapunguza mwamko na morali kwa watu kujihusisha na ukulima na inatakiwa kuiepuka fikra hiyo ili watu wengi wajiingize mashambani kulima.**

Lakini hapo kuna wazalishaji na wasambaza mbolea, mbegu na viuatilifu kwa wakulima.

Lakini kilimo wengi hawakifurahii. Kumekuwapo na dhana potofu kuhusiana na kilimo kwa hiyo wananchi hawana budi kupiga vita fikra hizo kama vile, ukulima ni kazi ya watu maskini hasa wasiosoma, huenda Watanzania walio wengi hawajishughulishi na kilimo kwa sababu wana taswira hiyo na mitizamo hasi akilini. Wengine wanapenda kukaa kijiweni kuliko kwenda shambani.

Kuendelea kudhani kuwa kilimo ni cha watu maskini kunapunguza mwamko na morali kwa watu kujihusisha na ukulima na inatakiwa kuiepuka fikra hiyo ili watu wengi wajiingize mashambani kulima.

Kilimo ni cha watu wa rika fulani kama vile wazee tu ndio wanatakiwa kulima kwa hiyo hii dhana inaondoa ari ya vijana kujihusisha na kilimo, hivyo kwa pamoja tuungane tupinge mtizamo huo ili tukikuze na kuuendeleza uchumi kwenye sekta hiyo.

Dhana nyingine zinazosambaa miongoni mwa vijana ni pamoja na ile isemayo kilimo ni cha watu waliofeli darasani, wengi wanaichukulia kuwa kulima ni kujitesa na ni jambo linalowahusu wasiofanikiwa hasa wale wenye maisha duni na wasioweza kuchangamkia fursa za maendeleo zilizoko mijini.

Lakini si kweli. Hata yule ambaye alifaulu maisha anaweza kufanya kilimo na kuna ugunduzi na matumizi ya vitu kama vitalu nyumba 'green houses' kulima kwenye maji 'hydroponics' vyote vikilenga kukuza na kuboresha kilimo ili kuinua uchumi wa nchi na kuwa na tija ili kufikia maendeleo.

Hivyo ni vyema kuanzia shuleni, vyuoni na ndani ya jamii watu waelimishwe umuhimu wa kuithamini sekta hiyo kuwa ni mwanzo wa chakula mezani, biashara endelevu na maisha bora kwa kila Mtanzania na kila anayeishi kwa kuwa chakula ni uhai na bila kula hakuna uhai.

## HABARI KITAIFA

# Walia na mgawo mkali wa maji

**Na Jenifer Gilla**

WAKAZI wa Kijiji cha Sindeni, Kata ya Sindeni, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni wameiomba serikali iingilie kati mgawo wa maji uliopitiliza kijijini hapo hali inayosababisha shida ya maji kuwa kubwa.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Haji Mhina alisema kabla ya kuanza mgawo huo walifanya kikao na Idara ya Maji Handeni (HTM), iliyoahidi kugawa maji mara moja kwa wiki, lakini utekelezaji umekuwa tofauti.

"Walituambia kuwa chanzo maji yamepungua Mto Pangani, lakini mitambo ya umeme ya kusukuma maji iliyopo Kwamatuku imepungua nguvu ndio sababu ya mgawo wa wiki, lakini sasa inakwenda wiki ya nne hakuna maji na hawasemi chochote," alisema.

Aliiomba Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kuingilia kati ili mamlaka irekebishe ratiba ya mgawo huo, itafute namna nyingine kwa wananchi kupata majisafi na salama.

Mkazi wa kijiji hicho, Saida Salehe, alisema kwa takribani miezi sita kumekuwa na mgawo hali inayosababisha kijiji kimoja kutegemea maji ya kisima kimoja pekee.

"Kuna wakati unakwenda unakuta foleni unaamua kurudi tu nyumbani, wanaojiweza wanaamka saa kumi alfajiri ili kukwepa hiyo foleni, lakini ni hatari kwa sisi wanawake," alisema.

Alisema wanalazimika kutumia maji hayo na mifugo kutokana na ukame ambao umekausha mabwawa ya kunyweshea mifugo hali inayochangia kisima kukauka maji haraka.

"Kama unavyotuona hapa, kuna foleni ya wanaopeleka nyumbani na wanaonywesha mifugo, wote tunategemea kisima hichi kimoja, hili nalo linachangia maji kuwa ya shida, tunaiomba serikali itusaidie," alisema.

Mfanyabiashara wa chakula, Mwanahawa Omari, alisema adha wanayopitia inawarudisha nyuma kimaendeleo kwa kuwa wanatumia fedha nyingi kununua majisafi ya kupikia.

"Huwezi kupikia maji ya kisima chakula au kukandia unga, inabidi kuagiza maji kutoka kijiji cha jirani ambapo mpaka yanifikie hapa dumu nanunua Sh. 500 hivyo natumia Sh. 2,000 kwa siku, ambayo naitoa kwenye faida kwa hiyo inaniathiri kipato changu," alisema.



Wanawake wa Kijiji cha Mgome, Kata ya Mpapayu, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakichota maji kijijini hapo juzi. Kijiji hicho na vingine vya Kwamnyefu, Kigongomawe, Magoda na Mpapayu, vinakabiliwa na shida kubwa ya maji. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yataja vipaumbele vya maendeleo 2023/24

**Na Richard Makore,** DODOMA

SERIKALI imewasilisha bungeni mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/24, ulioweka kipaumbele kwenye utekelezaji miradi ya maendeleo inayogusa maisha ya wananchi.

Akiwasilisha mapendekezo hayo jana bungeni, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema mapendekezo hayo yameangalia mpango wa tatu wa maendeleo wa mwaka 2021/22.

Maeneo hayo ni pamoja na kuchochea uchumi shindani na shirikishi kwa kuimarisha utulivu wa uchumi jumla, kuboresha uzalishaji na kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji, umeme na TEHAMA.

Aliongeza kuwa eneo lingine ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma kwa kuwezesha ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana nchini na kuendelea kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, uhifadhi wa mazao, masoko, mifugo na uvuvi; ikiwemo kuwezesha wananchi kushiriki katika uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa hasa zile za kilimo kupitia viwanda vidogo vidogo.

Kukuza biashara na uwekezaji kwa kujiikita katika kusimamia utekelezaji wa mpango kazi wa kuboresha mazingira ya biashara na mifumo ya uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji, biashara na masoko.

Kuchochea maendeleo ya watu kwa kuimarisha utoaji wa huduma za jamii ikiwemo afya, maji, elimu, utambuzi, upangaji, upimaji na urasimishaji wa ardhi nchini; na kuimarisha huduma za maendeleo ya jamii na makundi maalumu.

Dk. Nchemba alisema serikali inatarajia kuendeleza rasilimali watu ili kukuza ujuzi kwa vijana, kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo; na kutoa mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi kwa wahitimu wa elimu ya juu.

Alisema mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024 ni ukamilishaji wa miradi ya kielelezo yenye matokeo makubwa katika ukuaji wa uchumi inayojumuisha, ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (SGR).

Mengine ni kukamilisha mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere - MW 2,115, kuboresha shirika la ndege la taifa (ATCL), ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga.

Aidha, alisema mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika Lindi na ujenzi wa madaraja makubwa na barabara za juu ikiwamo la Kigongo - Busisi mkoani Mwanza.

Alisema katika kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu taifa linahitaji ushiriki wa sekta binafsi yenye uwezo wa kuchangia katika utekelezaji wa mpango.

Kwa msingi huo, serikali imesema tutaendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi kwa kufanyia kazi maoni na ushauri wa kukabiliana na changamoto za sekta binafsi katika utekelezaji wa mpango na miradi ya maendeleo.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma - Liganga pamoja na bandari ya Bagamoyo inatarajiwa kutelekezwa kwa kushirikisha sekta binafsi.

Waziri huyo alisema Mapendekezo ya Mwongozo na Mpango yatawezesha kukamilika kwa maandalizi ya Bajeti za Mafungu kwa wakati na kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Alisema mpango huo pia utasaidia kuimarika kwa utawala bora unaozingatia misingi ya sheria, kuongezeka kwa uwajibikaji na ushiriki wa wadau mbalimbali katika uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti.

## KABWELA



# Visima vyafufuliwa kuongeza maji Dar

Na Beatrice Shayo

SERIKALI imesema tayari imefufua zaidi ya visima 12 vilivyokuwa havitumiki, sasa vimeanza kutoa maji lengo ni kukabili tatizo la upatikanaji wa maji.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Bodi ya Maji la Bonde la Wami Ruvu, Mhandisi Elibariki Mmasi, wakati wakifufua kisima cha maji kinachotoa lita 100,000 kwa saa moja eneo la Komakoma Mwananyamala, kilichokuwa hakitumiki kwa zaidi ya miaka mitatu.

Alisema wanachokifanya ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kufufua visima 197 na hadi sasa sasa wamefufua zaidi ya visima 12.

Mmasi alisema kwa sasa kisima hicho wanakisafisha kwa sababu kimekaa muda mrefu bila kutumika na wapo na watu wa maabara ambao wataenda kupima ubora wa maji, ili wananchi waanze kuyatumia.

"Baada ya kukisafisha kisima hiki ripoti itakabidhiwa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) na kuingiza maji katika mfumo kwa ajili ya kupunguza hali ya upungufu wa maji hiki tunachokifanya ni endelevu tuna visima zaidi ya 197 na vina wingi wa maji tofauti tofauti,"alisema Mmasi.

Alisema kisima walichokifufua kina uwezo wa kuzalisha maji lita 100,000 kwa saa moja ni kisima kikubwa ndani ya muda wa siku 10 watakuwa wamekamilisha visima vyote.

Mmasi alisema maji hayo yana uwezo wa kusaidia watu zaidi ya 10,000, hivyo yatapunguza tatizo la maji kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

"Tumeona hiki kisima kina maji mengi tunaendelea kupampu kwa saa 24. Kama hakijatumika zaidi ya miaka miwili hadi mitatu vingine unakuta vina mawe tunavisafisha ili viwe salama kwa ajili ya matumizi,"alisema Mmasi.

Naye, Meneja wa Mawasiliano DAWASA, Everlasting Lyaro, alisema wanatekeleza agizo la Waziri Mkuu kufufua visima hivyo vitakavyoingizwa kwenye mfumo wa mamlaka hiyo.

Alisema ufufuaji wa visima itasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya maji kuna uwezekano wa ratiba ya maji ikabadilika kutokana na wingi wa maji katika visima vinavyofufuliwa.

Naye, Fundi Sanifu Maabara ya Maji Ubungo, Zairun Mbaga, alisema wataenda kuyahakiki maji hayo kama yapo katika ubora unaotakiwa kwa matumizi ya binadamu.

"Kisima hiki ni miongoni mwa visima vinavyotoa maji mengi na ni mkombozi kwa jiji la Dar es Salaam ndani ya wiki moja watakuwa wamekamilisha vipimo ili kuanza kutumika,"alisema.

Alisema vipimo vya awali tayari wamefanya katika eneo la kisima na vingine wanaenda kuvipeleka katika maabara yao, ili wananchi hao wapate maji safi na salama.

Wananchi wa eneo hilo walishangilia kuona maji yanatoka katika kisima hicho na kueleza yatawasaidia katika kukabiliana na tatizo la maji kwani wanateseka katika kupata huduma hiyo.



Meneja wa Programu ya Afya ya Uzazi ya Mama na Mtoto kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, Felista Bwana (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kuhusu hali ya vifo vya mama na mtoto nchini. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Morogoro yapokea bil. 5/- za miamala ya simu

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwassa, amesema kuwa mkoa huo umepokea Sh. bilioni 5.5 za mgawo wa miamala ya simu kwa kipindi cha 2021/2022 kwa ajili ya ujenzi wa vituo 11 vya afya.

Akizungumza wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), kilichofanyika mjini hapa, alisema kutokana na mgao huo sasa ujenzi unaendelea lengo ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma muhimu.

Akifafanua zaidi, Katibu Tawala Msaidizi Idara ya Mipango na Uratibu mkoa huo, Anza -Amen Ndossa alisema wanasimamia kwa karibu ujenzi wa majengo husika.

Ndossa alifafanua kuwa hali ya utekelezaji kwa vituo hivyo vilivyopata fedha awamu ya kwanza ilifikia asilimia 95 na kwa vituo vya awamu ya pili umefikia asilimia 25 na ujenzi wake bado unaendelea na kwamba kila kituo kimepatiwa Sh. milioni 500.

Aidha, alisema kata zilizochaguliwa baadhi zinaidadi kubwa ya wakazi na nyingine zipo pembezoni kutoka makao makuu ya halmashauri husika na kutokuwa na vituo vya afya kwa ajili ya huduma za wananchi.

Ndossa alizitaja halmashauri zilizopatiwa fedha na idadi ya vituo kwenye mabano na kata zake ni Malinyi (1) Ulanga (1), Mlimba (1) na Mji Ifakara (1).

Nyingine ni Kilosa (2), Gairo (1) Mvomero (1), Manisapaa ya Morogoro (1) na Morogoro (2).

Katika hatua nyingine, alisema halmashauri za mkoa huo zilitekeleza agizo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutenga Sh bilioni 2.6 kutokana na fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya.

Alisema kati ya fedha hizo, halmashauri ya wilaya ya Malinyi ilitenga kiasi cha Sh. milioni 574 za ukamilishaji hospitali ya wilaya na kituo cha afya Ngoheranga na Halmashauri ya Ulanga ilitenga Sh. milioni 100 za ujenzi wa zahanati mbili.

Ndossa alizitaja nyingine na kiasi kwenye mabano kuwa ni Mlimba (milioni 500), Mji Ifakara (milioni 410), Mvomero (milioni 200), Morogoro (milioni 310) na Manispaa ya Morogoro (milioni 570) huku Kilosa haikutenga na Gairo haikupangiwa mradi.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Mikumi, Dennis Londo akichangia katika sekta ya afya aliushauri mkoa na wilaya ya Kilosa kuweka mipango ya kujenga kituo cha afya kata ya Ruaha ,tarafa ya Mikumi.

Mbunge huyo alisema kata hiyo ina idadi kubwa ya watu na shughuli nyingi za uwekezaji kikiwemo kiwanda cha Sukari Kilombero ambacho kinapokea watu wengi ambao wanaishi kwenye kata hiyo ambayo haina kituo cha afya.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa mkoa huo, Mwassa alimwagiza mganga mkuu wa mkoa kulifanyia kazi jambo hilo, ili katika kata hiyo kijengwe kituo cha afya cha kisasa cha kutoa huduma za afya kwa wananchi na wageni.

# Serikali yadhamini vijana 400 kwenda Saudi Arabia

Na Beatrice Shayo

SERIKALI imewadhamini vijana 408 wa kitanzania kwenda kufanya kazi katika kiwanda cha Almarai nchini Saudi Arabia ambao watalipwa mshahara sio chini ya Sh. 1,000,000 na stahiki zao nyingine.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Jamal Katundu, wakati wa hafla ya kuwaaga Watanzania hao, alisema wataondoka kwa awamu tofauti na leo (kesho) watasafiri vijana 50.

Aidha, aliwataka vijana hao watumie vizuri fursa hiyo kwa kuhakikisha wanafanya kazi kwa uadilifu, ili Watanzania wengine waweze kupata ajira katika nchi hiyo.

Katundu alisema ofisi yake ina wajibu wa kutengeneza fursa za ajira milioni nane ifikapo mwaka 2025 ambayo ni maelekezo ya Chama cha Mapinduzi (CCM) katika ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020.

Alisema kinachofanyika ni mwendelezo huo na serikali wanalifanya kwa ufanisi hivi karibuni wanatarajia kukamilisha mkakati wa kitaifa wa kutengeneza fursa za ajira nchini.

Katibu Mkuu huyo alifafanua hivyo, baada ya Mkurugenzi wa Kampuni ya Wakala ya Bravo ambaye ni Mbunge Mstaafu wa Temeke, Mtevu, kueleza kuwa mwaka 2017 serikali ilizuia vijana wasisafiri licha ya kiwanda kuwalipia gharama zote vijana 160.

Kitundu alisema Desemba 31 mwaka jana Rais Samia Suluhu Hassan aliridhia uongozi huo kwa ajili ya kuratibu ajira za nje ya nchi Tanzania uwekwe hadharani na kufunguliwa rasmi.

Katundu alisema serikali ipo pamoja na vijana hao katika kuhakikisha usalama wao na haki zao zinalindwa wanapokwenda kufanya kazi nje ya nchi na sio vinginevyo.

**HABARI KITAIFA**

# Washauri sheria kulinda uharibifu mazingira

**Na Beatrice Shayo,** MPWAPWA

SERIKALI imeshauriwa kuweka sheria kali zitakazosaidia utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi yaliyoleta madhara ikiwamo ukosefu wa maji.

Akizungumza na Nipashe wakati wa mahojiano na Mwenyekiti wa Wilaya ya Mpwapwa, George Fuime, alisema mabadiliko ya tabianchi yanasababishwa na watu kuharibu mazingira.

Fuime alisema uharibifu wa mazingira utungiwe sheria ngumu kwa sababu wanapokwenda mahakamani bado kuna faini za zamani mtu anaona ni bora afyeke misitu na kulipa faini.

Alisema sheria zinazotumika ni za zamani ambazo zinatoa mwanya kwa wananchi kuendelea kuharibu mazingira na kusababisha kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Adhabu ni bora wakaiangalia upya, nashauri ingekuwa kubwa zinazotumika ni za zamani hatuwezi kwenda kwa namna hii tukafanikiwa katika janga hili mabadiliko ya tabianchi yanatokana na uharibifu wa mazingira leo hii mpaka muda huu mvua za vuli hazijanyesha ni kutokana na uharibifu wa mazingira," alisema. "Watendaji wetu wanapokwenda kule kazi ya usimamizi wa mazingira haifanyiki mtu ana fyeka misitu watu wanaona, mtu anachoma moto msitu anaachwa kuna kufichana mambo fulani matokeo yake kilio chake maji hakuna hii inatuathiri mahali pakubwa," alisema.

**Kosa kubwa ni kwenye mazingira mtu anafyeka hapa analima mwaka mmoja anaacha anaenda kufyeka eneo jingine analima na kuacha hili hatuwezi kukubaliana nalo tumekubaliana katika Wilaya ya Mpwapwa lazima tupambane ili kukomesha uharibifu wa mazingira.**

Alisema viongozi wake wameanzisha operesheni kwa watakaovamia maeneo yaliyohifadhiwa na serikali wachukuliwe hatua za kisheria.

Alisema utunzaji wa mazingira utasaidia kutokuwapo kwa mabadiliko ya tabianchi.

"Kosa kubwa ni kwenye mazingira mtu anafyeka hapa analima mwaka mmoja anaacha anaenda kufyeka eneo jingine analima na kuacha hili hatuwezi kukubaliana nalo tumekubaliana katika Wilaya ya Mpwapwa lazima tupambane ili kukomesha uharibifu wa mazingira," alisema.

Aidha, aliiomba serikali katika jambo hilo kuwa makini la sivyo katika vizazi vijavyo havitakuja kuambulia hata miti.

Fuime alisema maskini rafiki yake wa kwanza ni mazingira akiamka asubuhi anajiuliza wapi pa kupata fedha anaona ni bora kukata mti ama kuchoma mkaa ili apate fedha.

"Anatengeneza urafiki na mazingira huku akiharibu mazingira, serikali yetu itafute kitu mbadala tulisema tumepata gesi ya Mtwara tuliona nishati hii imekuja kutukomboa Watanzania tusisitize katika hiyo nishati wapunguze bei ili tuokoe uharibifu wa miti hata ukame utapungua," alisema.

Alieleza kuwa gesi ikiendelea kuwa bei kubwa watakwama na kuendelea kupata madhara kwenye matumizi ya mkaa kama watu watakuwa wanakata mikaa na kukosa watumiaji misitu haiwezi kuendelea kukatwa.

Aidha, alisema ukame pia umeathiri upatikanaji wa chakula kwa sasa debe la mahindi linazwa Sh. 20,000 ikifika Februari mwakani hali itakuwaje hata maji ni shida vyanzo vinakauka.

Fuemi alisema misitu ikiota itasaidia kurejesha uoto wa asili ndio maana wanawaondoa wote waliovamia milima na kupanda miti ambayo itachipua na misitu kurudi katika uoto wa asili.

Naye Mkazi wa Kijiji cha Sazima, Rebeka Masaweni, alisema kikubwa kilichowaathiri katika mabadiliko ya tabianchi ni maji na akiba yao ya chakula inakaribia kumalizika kutokana na ukame wameshindwa kupata mazao.

Alisema wapo ambao wanatumia zaidi ya kilometa saba kufuata maji na kujikuta shughuli zingine za kiuchumi zikiwashinda kutekeleza kwa wakati kutokana na tatizo hilo.

Diwani wa Kata ya Mima, Kijiji cha Sazima, Bezarery Mnyambwa, alisema ukame unasababisha shughuli nyingine za kiuchumi watu kushindwa kupiga hatua kwa sababu muda mwingi wanatafuta maji.

"Sehemu kubwa kwa sasa wananchi wangu ni kuhangaika kutafuta maji serikali itusaidie kuweka kisima kingine katikati ili kuwawezesha vitongoji vilivyo mbali kupata maji kwa ukaribu," alisema.

Pia alisema ukame umewasababishia upungufu wa chakula wanachokitumia sasa ni cha mwaka jana na wengine hawana.

## RC: Wakurugenzi wanaotuhumiwa ubadhirifu wahojiwe

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Qeen Sendiga amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri mkoani humo kuwarudisha watendaji wa serikali waliohama vituo vya kazi wakituhumiwa kufanya ubadhirifu katika miradi ya maendeleo iliyokuwa inatekelezwa katika maeneo hayo.

Agizo hilo alilitoa jana wakati akihutubia mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Kabwe wilayani Nkasi kuwa wananchi walilalamika kuwa Mtendaji wa Kijiji amehamishwa baada ya kuharibu mradi wa zahanati unaotekelezwa kijijini hapo.

Akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo, Sengida alijionea kijiji hicho kukwama kwa ujenzi wa jengo la mama na mtoto ambalo linadaiwa kupatiwa vifaa vya mabati na saruji toka kwa wafadhili mwaka 2020, lakini halijakamilika mpaka hivi sasa.

Baada ya kuhoji sababu za kutokamilika kwa ujenzi wa zahanati hiyo mpaka hivi sasa wananchi walimwambia kuwa Mtendaji wa Kata ndiye aliyesababisha hali hiyo na amehamishwa kituo kutokana na kufanya ubadhirifu wa fedha za ujenzi wa zahanati hiyo.

Sengida aliagiza mtendaji huyo arudishwe katika kituo hicho mara moja ili akajibu tuhuma zinazomkabili pamoja na watendaji wengine wanaotuhumiwa kwa sababu mbalimbali warudishwe kwenye vituo vya kazi walipo na tuhuma ili wakawajibike.

"Mtendaji wa kata aliyekuwa hapa arejeshwe kuja kutoa majawabu ya tuhuma za kutokamilika zahanati ya kijiji cha Kabwe wakati vifaa vya ujenzi vilitolewa na wafadhili na watendaji wanaotuhumiwa maeneo mengine nao warudishwe ili wakajibu tuhuma, hakuna kukimbia bali toa majibu," alisema Sendiga.



Imamu wa Msikiti wa Kichangani Magomeni, Sheikh Walid Alhad Omary, akizungumza wakati wa Sherehe ya Maulidi ya kuzaliwa Mtume (SAW) katika Msikiti wa Nnabiy Temboni jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Viongozi Msikiti wafanya maombi ya mvua

**Na Elizabeth Zaya**

VIONGOZI wa dini katika Msikiti wa Nnabiy ulioko Kimara Temboni, Mkoa wa Dar es Salaam, wamefanya maombi maalumu kumwomba Mungu ashushe neema ya mvua nchini.

Imam wa Msikiti huo, Mursalina Mavere, alisema wanaamini kwamba Mungu atawasikia na atajibu na kuwaomba viongozi wa dini mbalimbali kuitisha maombi maalumu katika nyumba zao za ibada kwa ajili ya kuomba neema hiyo ya mvua kwa Mungu.

"Tunawaomba viongozi wa dini kuitisha maombi maalumu katika nyumba zao za ibada ili kumuomba Mungu kwa ajili ya mvua, iwe misikitini, makanisani na penginepo, tunaomba wafanye hivyo, tunaamini katika maombi atatusikia na atatujibu," alisema Mavere.

Pia aliliomba Bunge kufanya dua ya kuomba mvua hiyo kila siku wanapoanza vikao vyao kwa kuwa wanaamini kila pembe ya nchi kuanzia kwenye vitongoji wakiomba kuhusu suala hilo, Mungu atasikia na atajibu.

Aliziomba mamlaka zinazohusika na usambazaji wa maji katika kipindi hiki ambacho kuna upungufu wa maji, kuhakikisha zinatenda haki ili kila kaya ipate huduma hiyo na kuepusha magonjwa ya milipuko ambayo yanaweza kusababishwa na ukosefu wa maji hayo.

"Unajua katika kipindi ambacho unaona wananchi wanapata tabu ni vyema wakati mwingine kuwa na roho ya huruma kutoa mchango hata mara chache, kwa mfano hawa wanaouza maji kwa sasa nao Mungu awaguse wapunguze bei ya maji kuwasaidia wananchi ili kila mmoja apate hasa katika kipindi hiki cha mpito na kufanya hivyo watakuwa wanaisaidia nchi," alisema Mavere.

Kwa upande wake, Shekhe wa Msikiti wa Kichangani, Walid Omari, alisema kuna haja ya kuitisha maombi ya kitaifa kwa kumuomba Mungu neema ya mvua na kuliepusha taifa na janga la ukame.

"Historia inaonyesha hata katika vitabu vya dini kwamba kunapotokea masuala muhimu kama haya yanayofanana na ukame, viongozi wa dini walikuwa wanawaita waumini wao na kumuomba Mungu ili awatatulie matatizo yanayowakabili," alisema Shekhe Omari.

"Na maisha siku zote huwa yana vitu viwili ambavyo ni Mungu na juhudi. Juhudi tumeona viongozi wa kitaifa wanawaambia wananchi wao wasikate miti au wachimbe visima, lakini kwa Mungu inabidi tumuombe kama tulikosea atusamehe na atuletee mvua ili tupate maji."

# Mkakati waja kuongeza matumizi ya gesi ya kupikia ifikapo 2030



Jacqueline Msongozi



Stephen Byabato




Habari na Augusta Njoji

SERIKALI imesema inaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha nchi inafikia zaidi ya asilimia 80 ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2032.

Aidha, kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), serikali inatarajia kutekeleza mradi wa majaribio kwa kutoa ruzuku ya asilimia 50 ya gharama zote kwenye jiko, gesi, mtungi pamoja na vifaa vinavyohusiana na awamu hii vifaa vipatavyo laki moja vitasambazwa katika mikoa 25 ya Tanzania Bara.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alibainisha hayo bungeni jijini hapo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jacqueline Msongozi.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali wa kuweka ruzuku kwenye majiko madogo ya gesi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Byabato alitaja mikakati hiyo kuwa ni kufanyika kwa mjadala wa kitaifa wa nishati safi ya kupikia, kuunda kikundi kazi kwa ajili ya uratibu, kutenga fedha katika bajeti ya 2023/2024, kwa ajili ya shughuli za nishati safi ya kupikia.

"Mkakati mwingine ni kuanzisha mfuko wa nishati safi ya kupikia pamoja na kuzitaka taasisi zote zenye watu zaidi ya 300 kama vile shule, vyombo vya ulinzi na usalama, magereza kutumia nishati mbadala kupikia ikiwamo gesi na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa," alisema.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati), akifurahia jambo na Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo (kulia) na Mbunge wa Singida Mjini, Musa Sima, walipokutana Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Udahili wanafunzi sayansi kufikia 160,000



Omary Kipanga



Zuberi Kuchauka

SERIKALI inatarajia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma programu za sayansi katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kutoka wanafunzi 40,000 kwa mwaka 2020 hadi kufikia 106,000 mwaka 2026.

Ongezeko hilo linatokana na kujengwa na kukarabati miundombinu mbalimbali kazi inayofanyika kupitia Mradi wa Higher Education for Economic Transformation (HEET).

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alieleza hayo jana bungeni jijini hapo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Liwale (CCM), Zuberi Kuchauka.

Mbunge huyo alitaka kujua ni kwa kiasi gani vyuo vya serikali vimejiandaa kupokea wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi.

Akijibu swali hilo, Kipanga alitaja miundombinu hiyo inayotarajiwa kujengwa na kukarabatiwa ni ujenzi wa maabara, karakana za kufundishia 108, vyumba vya mihadhara na madarasa 130, kumbi za mikutano ya kisayansi 23, mabweni 34, miundombinu ya shambani na vituo atamizi 10 kwa ajili ya kuendeleza ubunifu.

Aidha, alisema mradi huo pamoja na kuboresha mitaala zaidi ya 290 pia utasomesha wahadhiri 831 katika programu za kipaumbele.

Naibu Waziri huyo alisema kwa mwaka wa masomo 2022/23, serikali kupitia Samia Scholarship imetoa ufadhili wa asilimia 100 kwa wanafunzi 640 wenye ufaulu wa juu waliodahiliwa katika Vyuo Vikuu kusoma Programu za Sayansi, Teknolojia, Hisabati na Tiba.

## Mbunge ataka riba malipo malimbikizo

SERIKALI imetakiwa kulipa malimbikizo ya wanataaluma kwa riba kama inavyofanya kwa makandarasi wanavyocheleweshewa fedha zao.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Pauline Nahato, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akiuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Dk. Nahato alisema serikali kuwalipa wahadhiri malimbikizo hayo kwa riba.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema serikali haina utaratibu huo na kwamba hulipa malipo hayo kwa kanuni, sheria na miongozo na kanuni.

"Taratibu na kanuni hizi haziony esh i sehemu ya kulipa kwa riba, serikali tutaweka bajeti toshelezi ili tulipe kwa wakati," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji lini serikali itawalipa wanataaluma wote nchini malimbikizo yao ya miaka ya nyuma.

Akijibu swali hilo, alisema serikali hulipa malimbikizo ya watumishi wote wa serikali wakiwamo wanataaluma baada ya mtumishi husika kukamilisha taratibu muhimu zilizowekwa na serikali.

"Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Septemba, 2022 serikali imelipa Sh. bilioni 1.17 kwa ajili ya malimbikizo ya wahadhiri. Serikali itaendelea kulipa malimbikizo ya wahadhiri kulingana na bajeti ya fedha kwa mwezi na mwaka husika," alisema.

## Matumizi ya tozo maua barabarani hadharani

WAFANYABIASHARA wanaoweka bustani kando ya barabara hutozwa Sh. 4,639.5 kwa mita ya mraba kwa mwaka na hupelekwa Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara, Bunge lilielezwa jana mjini hapo.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Chwaka (CCM), Makame Mlenge Haji.

Mbunge huyo alihoji kwa nini wafanyabiashara wanaoweka bustani kando ya barabara hulipishwa fedha nyingi na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Naibu Waziri huyo alisema tozo kwa wafanyabiashara wanaoweka bustani kando ya barabara hutozwa kulingana na Mwongozo wa Udhibiti wa Uwekaji Huduma ndani ya eneo la hifadhi ya barabara.

"Mwongozo huu unatokana na Kanuni ya 3(1) ya Kanuni za Barabara ya Fedha na Ushirikishwaji wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi za mwaka 2011 zilizotolewa chini ya Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji kama wizara hiyo ina mpango wowote wa kutengeneza bustani kando ya barabara hasa mjini na inashirikiana vipi na ofisi ya Makamu wa Rais kulinda mazingira hasa kandokando ya barabara.

**HABARI KASKAZINI**

## DC akemea ufujaji fedha mbichi kwenye vijiji, kata

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera, amekemea ufujaji na ubadhirifu wa matumizi ya fedha mbichi kwenye vijiji na kata.

Fedha hizo ni taslimu zinazokusanywa na kutolewa benki kwa malengo ya kuhifadhiwa au matumizi mbalimbali.

Dk. Serera, akizungumza jana na watumishi wa serikali, wakiwamo maofisa tarafa, madiwani, watendaji wa vijiji na kata, wenyeviti wa vitongoji na vijiji, alisema matumizi ya fedha mbichi yanapaswa kuangaliwa vizuri.

Alisema fedha zote zinazokusanywa na kutolewa benki, kwenye vijiji na kata zote zinapaswa kutumika kwa malengo husika na si vinginevyo.

Kadhalika, alitoa onyo kwa wenyeviti wa vitongoji na vijiji, kwa kuwataka kuwa waadilifu na kuwajibika ipasavyo, kwa kuwa hata wakistaafu na ikitokea kama walifuja fedha watashtakiwa na kufungwa.

"Kuna mwenyekiti wa kijiji mstaafu ambaye aliuza ardhi na kufuja fedha, akafikishwa mahakamani na kuhukumiwa miaka minne kwenda jela hivyo kuweni makini," alisema Dk. Serera.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer, aliwataka wenyeviti wa vitongoji na vijiji, kuwa waaminifu na kuacha mara moja suala la uuzaji wa ardhi kiholela.

Kiria alisema, chama hicho hakitamuonea huruma kiongozi yeyote, atakayehusika kuuza ardhi na kusababisha migogoro isiyokuwa na tija.

**Kuna mwenyekiti wa kijiji mstaafu ambaye aliuza ardhi na kufuja fedha, akafikishwa mahakamani na kuhukumiwa miaka minne kwenda jela hivyo kuweni makini.**

# Mbunge aomba wanawake kumuunga mkono Rais

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MBUNGE wa Viti maalum wa Mkoa wa Manyara, Regina Ndege, amewaomba wanawake wote nchini, kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na jitihada zake za utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alitoa ombi hilo jana wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Wanawake wa Jumuiya ya Chama cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Simanjiro, kilichofanyika mji mdogo wa Orkesumet.

Alisema wanawake wanapaswa kumuunga mkono Rais Samia kwa kuwa amefanikiwa kujenga miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo katika sekta ya afya, elimu, maji na barabara.

**Kwa kweli nampongeza rais wetu, kwakuwa amefanya kazi kubwa, amegusa kila sekta na dhamira yake ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora na uhakika.**

"Tumeona miradi mingi ilivyotekelezwa ikiwamo ya ujenzi wa vituo vya afya kujengwa vipya, hospitali, ujenzi wa vyumba vya madarasa mapya katika shule za msingi na sekondari na miradi mingi ya maji," alisema Ndege.

Aidha, alisema wanawake hawana budi zaidi ya kukubaliana na kazi zilizofanyika kwa muda tangu ameingia madarakani kwa kuwa amekuwa na malengo ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za uhakika.



"Kwa kweli nampongeza rais wetu, kwakuwa amefanya kazi kubwa, amegusa kila sekta na dhamira yake ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora na uhakika," aliongeza.

Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Simanjiro, Anna Shinini, alisema Rais Samia (pichani), amewaheshimisha wanawake kwa namna anavyoongoza nchi na kwamba wanawake wanapaswa kuungana naye katika hatua ya utendaji kazi.

Shinini alisema, Jumuiya ya wanawake wilayani humo, itamuunga mkongo kiongozi huyo mkuu wa chama kwa vitendo kwa kazi nzuri alizofanya.



Diwani wa Viti Maalumu, Tarafa ya Kwekivu, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, Habiba Mnguya, akizungumza na wananchi wa Mji wa Songe jana, kuhusu mradi wa ujenzi wa daraja linalounganisha mji huo na huduma mbalimbali za jamii. **PICHA: DEGE MASOLI**

# '75% ukuaji ubongo wa mtoto hutegemea malezi'

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

OFISA Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Manyara, Lilian Bujune, amesema ukuaji wa ubongo kwa watoto wadogo wanapozaliwa unakuwa umekamilika kwa asilimia 25 na kiwango kilichobaki kitategemea malezi wakati wa ukuaji wao.

Ofisa huyo,alisema hayo jana wakati akizungumzia suala la malezi na makuzi ya mtoto kuanzia miaka sifuri hadi miaka minane kwa kuwa inalenga kwenye utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM).

Alisema malezi na makuzi si jukumu la serikali pekee bali linaihusisha jamii nzima ambayo inatakiwa kuwalea tangu wakiwa tumboni mpaka wanapokuwa kwa kushirikiana na wazazi.

Aliwaomba wananchi kutekeleza jukumu la malezi na makuzi vizuri ili kusaidia watoto kukua katika utimilifu wao.

Alisema ili wakuwe katika utimilifu mzuri wanatakiwa kupata lishe bora, kuwa na afya, elimu ya awali, malezi yenye mwitikio, ulinzi na usalama wa watoto.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Cosita, Patrice Gwasma, alisema wananchi wakizingatia suala la lishe kwa watoto wataepukana na kuwa na watoto wenye udumavu.

Alisema wazazi na walezi wakizingatia vizuri malezi na kuutumia utandawazi vizuri watoto watalelewa katika maadili na kuwa msaada kwa taifa.

Oktoba 28, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, alisaini mkataba wa lishe na kusema kuna tatizo katika halmashauri kutenga fedha na namna ya kuzitumia na kuwaagiza wakuu wa wilaya kusimamia mkataba huo, kwa kila kijiji ili kutokomeza udumavu.

PJT-MMMAM ilizinduliwa Desemba 13, mwaka jana na aliyekuwa Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima na inaeleza kuwa ingawa huduma za malezi yenye mwitikio inaweza kuonekana mbinu mpya ni muhimu kutambua mila na desturi nzuri zilizoko ikiwamo za malezi ya watoto kwa kuwa inaweza kuendelezwa na kuboreshwa inapowezekana.

Vilevile, inaeleza kuwa wazazi, walezi na familia washawishiwe kutumia stadi na uwezo wa kutengeneza vifaa vya michezo vinavyopatikana kwenye jamii kwa kutumia malighafi zenye gharama ya chini.

# Akumbusha uwekezaji mzuri vyanzo vya maji

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MKUU wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa, amesema endapo hakutakuwa na uwekezaji mzuri kwenye vyanzo vya maji kuna uwezekano mkubwa kwa siku zijazo kukakosekana huduma hiyo.

Mgandilwa aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa wadau juu ya uanzishwaji kwa mfuko wa maji Tanga.

Alisema kupitia elimu hiyo, ni vyema wakarudi kwenye taasisi zao wakashauri namna ya kuwekeza kwenye vyanzo hivyo.

Alisema ni muhimu kwa wamiliki wa viwanda na wawekezaji kuangalia namna nzuri ya kutumia sehemu ya faida zao, kuwekeza kwenye miradi ya maji ambayo itasaidia kutunza vyanzo.

Alisema kwa kuwa hakuna kiwanda bila rasilimali maji, kila mmoja kwenye kampuni na taasisi yake, wawekeze kusaidia jamii.

**Shughuli za utunzaji wa vyanzo hivyo inahitaji uwekezaji mkubwa na ushiriki wa wadau hao, utatoa matokeo chanya na kumaliza tatizo la uharibifu.**

"Naombeni mkitoka hapa mkaangalie namna ya kwenda kuongeza ujuzi wa kutunza vyanzo vya maji kwa lengo la kuvilinda viwe endelevu kwa maslahi ya vizazi vya sasa na baadaye mkashirikiane kuwekeza miradi ya maji," alisema.

Alisema sasa hivi kuna matatizo mbalimbali hasa ya ulimaji usio endelevu pamoja na ufugaji wa mifugo holela na utiririshaji wa maji machafu kwenye vyanzo vya maji jambo alilosema lina athari na kutaka wananchi kubadilika.

"Tatizo lingine ni wananchi bado wana tabia ya kuoga na kufua kwenye vyanzo, haya yote yanatokea kwa kuwa Watanzania wengi wao sasa hivi ni wabinafsi tofauti na zamani tulikuwa tunaangalia ya taifa," alisema.

Aliwataka kupitia umoja wao, kuweka mikakati ya kukabiliana na uharibifu wa vyanzo ili viendelee kuwa endelevu kwa maslahi ya wananchi.

"Nasisitiza suala la uhifadhi wa vyanzo vya maji ni mtambuka kwa kuwa Watanzania wengi, wanaona utunzaji wa maji sio wajibu wao," alisema.

Alisema kutokana na dunia inavyoelekea miaka michache baadaye rasilimali maji itakuwa mtihani kwa kuwa itakuwa na thamani kubwa kwa kila mtu ambaye anatumia.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maji Tanga (UWASA), Dk. Ally Fungo, alisema mfuko huo, utawezesha kuongeza nguvu katika jitihada za utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kuwapatia shughuli mbadala wananchi wanaoishi kando ya vyanzo hivyo.

Alisema, shughuli za utunzaji wa vyanzo hivyo inahitaji uwekezaji mkubwa na ushiriki wa wadau hao, utatoa matokeo chanya na kumaliza tatizo la uharibifu.

# Serikali kuendelea kutoa fedha upanuzi miradi ya maji

**Na Allan Isack,** ARUMERU

KAIMU Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini(RUWASA) wilayani Arumeru, Peter Maina, amesema serikali inaendelea kutoa fedha za upanuzi wa miradi ya miradi ya maji iliyoanza kutekelezwa ili kufika kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya maji.

Aliyasema hayo juzi wakati akijibu swali la Diwani wa Kata ya Kisongo, kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani, aliyeomba kupewa ufafanuzi wa hatima ya mradi wa maji Lesira, kuwafikia wananchi wa kitongoji cha Bwawani kilichoko ndani ya kijiji hicho. Alisema, tayari huduma ya maji imeshafika Kijiji cha Lesiraa na baadhi ya maeneo hayajafikiwa hasa Kitongoji cha Bwawani.

Alisema kitongoji hicho hakijafikiwa kwa kuwa ujenzi unafanyika kadri walivyopokea fedha zitakavyotolewa na serikali kupanua mradi ili kuwafikia wananchi.

Alisema serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji na upanuzi wa miradi ya maji ambayo imeanza kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji katika jamii.

Akiwasilisha taarifa yake, Kaimu Meneja huyo amebainisha kuwa katika kipindi cha robo ya kwanza, RUWASA, imeendelea kutekeleza miradi kupitia fedha za Mfuko wa Maji (NWF), za UVIKO-19 na malipo kwa matokeo (PbRV).

Aidha, alisema Sh. milioni 801.1 za NWF, zinatekeleza mradi wa maji Losikito, ukijumuhisha ujenzi wa nyumba ya pumpu, tangi la kukusanyia maji na uzio, Sh. milioni 376 za PbRV, zitatumika kwenye mradi wa maji Manyire, Marurani na Majimoto, Sh. milioni 200 na mradi wa maji Old Nduruma kwa Sh. milioni 176, miradi yote imefikia asilimia 90 ya utekelezaji.

"Tutaendelea na upanuzi wa miradi kadiri watakavyopokea fedha kwa kuwa malengo yao ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya maji na ya uhakika," alisema.



Wanafunzi wa Shule ya Awali na Msingi New Light ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakinawa mikono wakati wakijifunza usafi kwa vitendo shuleni hapo juzi, wakiongozwa na mwalimu wao Daniel Peino. **PICHA: GIFT THADEY**

# Huduma ya maktaba mbioni kutolewa kielektroniki

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BODI ya Huduma za Maktaba Tanzania, iko mbioni kutengeneza sera hizo ikiwamo kufanya marekebisho ya Sheria ya Mwaka 1975, ili kuendana na kasi ya utoaji huduma hizo kwa njia ya kielektroniki kitaifa na kimataifa.

Akizungumza jana katika mafunzo ya siku tano yanayofanyika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) na kukutanisha wataalamu wa maabara za kisayansi kupitia Shirikisho la Maktaba na Vyuo vya Utafiti (COTUL), Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Dk. Mboni Ruzegea, alisema sera hizo na sheria zikirekebishwa, itatoa wigo mpana wa kazi zinazofanywa na watunzi wa vitabu ikiwamo wahadhiri na watafiti, kutambulika zaidi kupitia maktaba za kielektroniki.

Pia wanafunzi kuanzia ngazi za chini hadi vyuo vikuu watasoma mambo mbalimbali kupitia maktaba hizo, katika viganja vyao vya simu au kompyuta mtandao, sehemu yoyote watakapokuwa wakihitaji kujisomea vitabu au vitu mbalimbali vilivyotungwa na Watanzania na watunzi wengine kimataifa.

"Huduma za maktaba ni bure, lakini tukiungana kwa pamoja na vyuo vikuu mbalimbali, wasomi watasoma vitabu kupitia mfumo wa kielektroniki ambao ni rafiki kwa kila mtu na sheria hii ikirekebishwa pamoja na sera, tutafika mbali kupitia maktaba za kielektroniki," alisema.

Kaimu Mkuu wa Chuo cha Uhasibu (IAA), Dk. Cairo Mwaitete, alisema vyuo vikuu vikiungana kwa pamoja na mfumo huo wa kielektroniki ukianza kazi, watu mbalimbali watasoma vitabu ikiwamo tafiti za wahadhiri na maprofesa na kupata ufumbuzi wa jambo husika.

Alisema endapo COTUL na Wizara ya Elimu zikiungana, gharama za uchapishaji vitabu zitapungua ikiwamo kila vyuo kuwa na maktaba za kisasa, ili kuongeza wanachuo, wanafunzi na watu mbalimbali kusoma vitabu kwa ajili ya manufaa yao.

Awali, akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Richard Ruyango, alisisitiza Watanzania kupenda kusoma vitabu ili kujifunza mbinu mbalimbali za kimaisha ikiwamo wanafunzi na wanachuo katika vyuo mbalimbali.

Ruyango, alisema maabara hiyo ya kielektroniki, itasaidia watunzi wa vitabu kujulikana ndani na nje ya nchi, kutokana na utunzi wa vitabu vitakavyosomwa kwa njia ya elektroniki.

Ukurasa 15




**Ajali ya ndege Bukoba isaidie kuwapo mbinu zaidi za uokoaji**

Ukurasa 16



Ni Ulaya ya kinamama uelekeo usawa kijinsia

Ukurasa 19



**JENERALI MUHOOZI KAINERUGABA Mwanawe Museveni aliyesheheni vijimambo**

siasa
JUMATANO NOVEMBA 9, 2022
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

# Shaka ajigamba uchaguzi CCM, makada kibao wameingia ulingoni

## •Dar wapo 30, ataja kupanuka demokrasia sababu ya mafuriko

**Na Sabato Kasika**

MWISHONI mwa mwezi huu, wanachama wa CCM wanatarajia kufanya uchaguzi wa viongozi wa ngazi za juu ambao ni wenyeviti wa mikoa na pia watakaoongoza jumuiya za chama hicho kama za vijana (UVCCM), wanawake (UWT) na Wazazi ni baada ya kukamilisha kuwachagua wale wa mashina, matawi, kata na wilaya.

Ni mwaka wa uchaguzi wa chama tawala na wakati kikielekea katika uchaguzi huo, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, anasema hajjawahi kutokea makada kujitokeza kwa wingi kuwania uongozi kama ilivyotokea mwaka huu.

Katika mazungunzo yake na gazeti hili jijini Dar es Salaam, anasema tofauti na uchaguzi wa ndani ya chama uliopita, wa mwaka huu umetia fora makada wamekuwa ni wengi zaidi kuwania nafasi za uongozi hasa kwenye ngazi ya mkoa.

"Unakuta nafasi moja wanajitokeza makada kuanzia 30 hadi 80. Haijawahi kutokea, na inaonyesha ni jinsi gani chama kimeimarisha demokrasia ya ndani na kudhibiti vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili ," anasema Shaka.

Anafafanua kuwa chini ya Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, ndani ya kipindi kifupi alichoshika nafasi hiyo, kumekuwapo na uwazi na kupanuka kwa demokrasia ili



Shaka Hamdu Shaka. **PICHA: MAKTABA**

kumpa nafasi kila mwanachama kuomba nafasi ya uongozi anapokuwa na sifa, tofauti na kupanga safu za uongozi.

"Nakupa mfano, kwa mkoa wa Dar es Salaam pekee, wamejitokeza makada 30 watakaowania nafasi ya Mwenyekiti wa CCM wa mkoa, lakini miaka sita iliyopita haikuwa hivyo, tumejipanga na tunaendelea kujiimarisha," anasema.

Baadhi ya waliochukua fomu ni viongozi wa sasa wa Dar es Salaam, mwenyekiti Kate Kamba na Katibu Mwenezi Simon Mwakifamba, wengine ni mwenyekiti wa zamani Wilaya ya Kinondoni, Salum Madenge, mbunge wa zamani wa Temeke, Abbas Mtemvu na mwenezi mstaafu Wilaya ya Kinondoni, Peter Konisaga.

Shaka anaongeza kuwa tangu uchaguzi wa ngazi ya shina, CCM ilikuwa macho kukabiliana na watoa rushwa hadi kufikia kufuta baadhi ya uchaguzi baada ya kubaini kuwapo kwa vitendo hivyo.

Anafafanua kuwa kutokana na hatua hizo, makada wameendelea kuwa na imani na viongozi wa chama chao hadi kujitokeza kwa wingi kusaka nafasi moja katika uchaguzi ndani ya chama hicho.

"Jambo la muhimu ni kuwaomba wana CCM kuendelea kuwaamini viongozi wao kwa jinsi ambavyo wanaendelea kuimarisha demokrasia ndani ya chama chao na kupambana na vitendo vya rushwa," anasema.

**SERA ZA SAMIA**

Shaka anasema sera za Rais Samia anazoendelea kuzitekeleza tangu ameingia madarakani, zimetoa mwelekeo chanya wa kuimarisha na kuboresha ustawi wa maisha ya Watanzania katika kila sekta, huku amani ikipewa kipaumbele pamoja na kuongeza kuaminiana na kushirikiana kwa kuwa Tanzania ni ya watu wote.

"Utaratibu wake wa kuamua kuwapatia mrejesho wa kazi za maendeleo ambazo serikali yake imekuwa ikifanya tangu ashike madaraka, ni uwazi na uwajibikaji ambavyo wanachama wamekuwa wavitamani," anasema.

Anasema chini ya uongozi wake serikali ya CCM inazidi kujipambanua katika misingi ya utawala bora na demokrasia inapotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya 2020 - 2025, kwa kuzingatia uwazi na uwajibikaji.

Shaka anasema ni vyema wana CCM na Watanzania kwa jumla kuendelea kumuunga mkono kwa kazi nzuri anayofanya ya kuwaletea maendeleo ya kweli ikiwamo kusogeza karibu huduma mbalimbali za kijamii.

**JICHO PANA**

Wakati huu wa kuelekea uchaguzi katika ngazi ya mkoa, Katibu Mkuu wa chama hicho, Daniel Chongolo, anasema macho ya viongozi wote yako wazi wakifuatilia mchakato mzima kwa karibu ili kudhibiti wanaovuruga na kwenda kinyume

**INAENDELEA UK. 20**

# Wanasiasa walia na kura ya mapema Zanzibar wakitaka ifutiliwe mbali

## • CHADEMA ikihoji watu 500,000 siku mbili za uchaguzi kwanini?



Rais wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi, pamoja na Kamati Maalum ya Kikosi Kazi ya Kuchambua Maoni ya Washiriki wa Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa, baada ya kukabidhiwa ripoti ya maoni ya wananchi . **PICHA: IKULU.**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAAMUZI ya Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuunda kikosi kazi cha kuchakata maoni ya wadau walioshiriki mkutano mahsusi wa demkorasia na hatimaye timu hiyo kuwasilisha ripoti yake kwa Rais, yanaungwa mkono na wanasiasa visiwani hapa.

Kikosi kazi hicho kilichokuwa na wajumbe 11 kikiongozwa na mwenyekiti Dk. Ali Uki , kinawasilisha ripoti yao hiyo ambayo mjadala mkubwa uliibuka kuhusu kura ya mapema ambayo hupigwa siku moja kabla ya uchaguzi mkuu Zanzibar.

Mweyekiti wa kamati hiyo anasema suala la kura ya mapema kamati imeamua kumuachia Rais ili kujadiliana na Makamu wa kwanza Othman Masoud na kulitafutia majibu jambo hilo.

Anasema wapo ambao walipendekeza kura hiyo iendelee lakini kuna baadhi wanaopinga wakipendekeza kuwa ifutwe, isiwepo na badala yake kuwepo na siku moja pekee ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu na si vinginevyo.

Anaongeza kuwa wapo wanaopendekeza kura hiyo iendelee kuwepo wakishauri kuwe na uadilifu katika upigaji wake yote hayo yakiachwa mikononi mwa Rais na Makamu kuamua hatma yake.

Salum Mwalimu ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), anasema chama hicho kilishirikishwa katika kutoa maoni yao kwenye kikosi kazi hicho na kikawasilisha mambo tisa ambayo yakifanyiwa kazi wana imani yataondoa vikwazo vya haki na maendeleo ya Wazanzibari.

Anasema mambo hayo endapo Rais Dk. Mwinyi, atayasimamia kwa dhati yanakwenda kutengeneza Zanzibar mpya ambayo ni tunu na imani ya kila mwananchi.

Anaongeza kuwa wanahitaji kushughulikia changamoto za kiuchaguzi ikiwamo pia makandokando yote yanayotokana na uchaguzi na uminywaji wa haki wakati wa zoezi hilo visiwani hapo.

Aidha, anasema uminywaji wa haki za wagombea, kuweka mawakala, haki za wagombea kupewa fomu za matokeo zilizorasimi, uhuru wa kufanya kampeni na uhuru wa Wazanzibar kuandikishwa katika daftari la wapiga kura na haki za vyama vya siasa kusimamisha wagombea ni suala wanaloliibua.

Mambo hayo yanatakiwa kufanyiwa kazi na kwamba yapo yanayohitaji mabadiliko ya kisheria , na mengine ya kiutawala na yapo ambayo ni utashi wa mwenyewe Rais wa Zanzibar kuona ni njia ya kuwapitisha watu kuelekea uchaguzi wa mwaka 2025, anasema Mwalimu.

Naibu Katibu Mkuu anaongeza kuwa wameridhishwa na ripoti ya awali iliyotolewa na kamati maalum ambayo imegusia mambo muhimu kadhalika CHADEMA nayo imeyazungumzia.

Anapozungumzia kura ya mapema anasema kwa mujibu wa idadi ya watu wa Zanzibar iliyotolewa hivi karibuni na ripoti ya Sense ya Watu na Makazi 2022 , visiwani humo kuna watu milioni 1.8 , hivyo hakuna haja ya kuwepo kwa kura hiyo ya kabla .

“Katika uchaguzi wa mwaka 2020 waliopiga kura Zanzibar hawafikii hata 500,000 , mbona haiwi Tanzania Bara ambako wana idadi kubwa ya wapiga kura na wanapiga kura siku moja”anahoji Mwalimu.

Aidha, anasema kura ya mapema haionyeshi ustarabu wa kisiasa hivyo anamshauri Rais aikatae na kurudi katika siku moja ya upigaji wa kura, ambayo ni suala linalofanyika ndani ya Muungano.

Anasema Chadema ina imani kuwa yale ambayo walimueleza Rais katika mkutano wa kujadili masuala ya demokrasia na mfumo wa vyama vingi atayafanyia kazi na hana shaka busara zitawaongoza kuduri katika siku moja ya kupiga kura.

Akizungumzia kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), Mwalimu anasema isiishie katika baraza la mawaziri na isiishie katika vyama viwili bali ishuke mpaka katika kamati za sheha zikiwa na sura za umoja wa kitaifa ili kuendelea kuijenga nchi kwa pamoja.

Salum Bimani ni Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Umma wa ACT -Wazalendo, anayesema chama hicho kimebariki yaliyoelezwa katika ripoti ya kikosi kazi hicho ambapo mmoja ya kiongozi ndani ya chama hicho ambaye ni Ismail Jussa alikuwa ni miongoni mwa wajumbe wa kikosi kazi.

“Tunakipongeza kikosi kazi kwa kuwasilisha ripoti yao mbele ya Rais wa Zanzibar na endapo Rais atayafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na wajumbe atazidi kuivusha Zanzibar katika siasa za chuki na uhasama,”anasema Bimani.

Akizungumzia kuhusu kura ya mapema Bimani anasema, hakuna haja ya uwepo wa kura hiyo na badala yake kurejea katika mfumo wa awali wa siku moja ya upigaji wa kura.

Bimani anasema bado chama kinaendelea na vikao vyake na hivi karibu kitazungumzia zaidi maoni yao kuhusu ripoti hiyo na mambo yote yaliopendekezwa.

Katibu mkuu wa chama cha UPDP, Hamad Muhammed Ibrahim, anasema chama hicho kimeyaridhia mapendekezo yote yaliotolewa na kikosi kazi na kukipongeza kwa kufanya kazi nzuri na kwa weledi ambayo Wazanzibari ndicho wanachohitaji.

Akizungumzia kuhusu kura ya mapema, anasema kuwa ni vyema kura hiyo kuendelea kuwepo lakini yaongezwe makundi mengine yenye mahitaji maalum ambayo hayakuorodheshwa.

Anayataja makundi hayo ambayo wangependa kuorodheshwa katika kupiga kura hiyo ya mapema inayopigwa siku moja kabla ya uchaguzi mkuu kuwa ni wajawazito, wazee wenye umri mkubwa, wagonjwa na watu wenye ulemavu na mahitaji maalumu.

“Uwepo wa kura ya mapema ni muhimu ili kuwapa nafasi wale ambao wanamahitaji maalum nao kupata haki yao hiyo mapema, ”anasema Ibrahim

Aidha, anazungumzia suala la matokeo ya urais kuhojiwa mahakamani akisema wanaunga mkono hilo pamoja na SUK ianzie katika ngazi za chini katika ugawanyo wa nafasi za uongozi badala ya mgawanyo huo kuwepo katika uongozi wa juu pekee.

Pia, anaeleza kuwa wanaunga mkono hoja ya Muungano iliyoelezwa katika ripoti hiyo ikiwemo mikataba inayopangwa katika Jamuhuri yaMuungano itekelezwe ili Wazanzibar wafaidike na yale ambayo viongozi wanakubaliana kwa maslahi ya taifa.

Anasema kwa muda mfupi Rais Dk Mwinyi aliokaa madarakani amefanya mambo mengi mazuri ikiwamo la kuona Wazanzibari wanahitaji kuendesha nchi yao kwa mustakbali bora bila ya kujali itikadi za kisiasa.

“Kikosi kazi kilichoundwa kilijumuisha vyama vyote vya siasa na kilizingatia ushirikishwaji wa vyama vya siasa kwa hiyo matarajio yetu ni kwamba yaliyozungumzwa na kikosi kazi tutayaunga mkono kwa dhati tukijua ya kwamba kuipa nafasi serikali kutekeleza mapendekezo hayo”anasema.

Wakati akipokea ripoti ya kikosi kazi hicho, Rais Dk Mwinyi, anaahidi kuhakikisha katika kipindi cha uongozi wake anatekeleza na kusimamia maridhiano ya kisiasa ambayo ndiyo yatakayoihakikishia Zanzibar kuwepo kwa amani ya kudumu na wananchi kufanya shughuli zao za ujenzi wa taifa na kukuza uchumi.

# Ajali ya ndege Bukoba isaidie kuwapo mbinu zaidi za uokoaji

NA GAUDENSIA MNGUMI

WATU 19 waliofariki kwenye ajali ya ndege ya Precision Air, Jumapili iliyopita, wanaleta tafakari mpya , pengine kuwa ujuzi mdogo na au ukosefu wa mafunzo ya kitaalamu katika kuokoa maisha na kutoa huduma ya kwanza na ya dharura kwa waathirika wa majanga kama ajali za barabarani, ndege, moto na majini ni tatizo kubwa.

Kinachoonekana ni kukosekana ujuzi na maarifa pamoja na vitendea kazi.

Tena huenda hata kikosi cha uokoaji kilichotegemewa kutoa msaada pengine kilipata mafunzo miaka mingi iliyopita, na kwamba kisingeweza kufanya kazi ya uokoaji kwa weledi.

Hilo limepita na serikali inalichunguza, lakini ni vyema kuangalia wapi taifa lilipokosea au kuanguka, ili lisimame na kujisahihisha.

La muhimu, ni kumaanisha na kuchukua hatua kuhusu kufanikisha operesheni za uokoaji na mafunzo ya huduma ya dharura ajali zinapotokea.

Ukiangalia ajali za barabarani hata gari linapoanguka au lori kubwa lenye shehena, tena jijini Dar es Salaam, eneo lenye maendeleo zaidi kuliko mkoa mwingine, hali ni mbaya.

Kazi ya kulisogeza pembeni kutoka barabarani inakuwa ngumu, na matokeo yake ni kuongezeka foleni na misururu mirefu ya vyombo vya moto baada ya kuziba njia.

Ni hatari mno gari lenye kontena linapoangukia daladala au gari lenye abiria, kinachotokea kinajulikana ni hukumu ya kifo. Hakuna msaada. Wakala wa Taifa wa Barabara -TANROADS hauna miundombinu kama magari maalumu ya kuondoa magari yaliyopata ajali, yaliyoanguka au kuzimika barabarani.

Kwa miaka 61 ya Uhuru inayotimia mwezi ujao, Tanzania haina 'truck' la kuondoa magari makubwa yanayoanguka barabarani? Ni mpaka kuomba msaada Mamlaka ya Bandari, au kampuni binafsi za ulinzi au kutegemea wasafirishaji binafsi, kwa hilo nalo taifa lingetafakari.

Lakini lililotokea Bukoba liitafakarishe TANROADS kuimarisha huduma za uokoaji kwenye ajali za barabarani.

Vifo vingi vya abiria wa ajali ya ndege ya Bukoba, pengine vingeweza kuzuilika kama kikosi cha uokoaji kingekuwapo na kuwasili kwa wakati na kutoa huduma za dharura kabla ya hali kuwa mbaya na waathirika kukaa saa nyingi bila msaada.

Lakini kwanini kusiwe na huduma ya dharura ya uokoaji kwenye uwanja wa Bukoba? Kiwanja hicho kiko karibu na ziwa Victoria, inakuwaje hakuna timu ya uokoaji uwanjani hapo iliyojiandaa au kukaa 'standby'?

Katika masuala ya ajali 'wataalamu wa kiwewe au kufadhaika' au 'trauma experts' wanaeleza kuwa ndani ya dakika 60 za mwanzo ambazo kwa lugha yao huziita 'the golden hour" baada ya ajali kutokea ndizo za muhimu mno kuokoa maisha.

Si zaidi ya hapo, hata kama nguvu gani zitatumika kunusuru majeruhi haiwezekani kuwa na mafanikio ya kuokoa.

Ndiyo maana wavuvi hasa Jackson Majaliwa na wenzake walifanya kazi yenye mafanikio kwa kuzingatia muda wa ndani ya dakika 60 za kwanza au muda wa dhahabu" baada ya ajali hiyo ambacho ndicho kipindi muhimu cha kuokoa maisha.

Wataalamu wanaamini kuwa uwezekano wa kufa au majeraha kuwa makubwa unaoongezeka baada ya kipindi hicho.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akitoa salamu za mwisho kwa miili ya watu waliofariki kwa ajali ya ndege ya shirika la Precision , wakati wa kuwaaga katika Uwanja wa Kaitaba, mjini Bukoba, mkoani Kagera juzi. **PICHA: OWM**

### KUFUNZA RAIA

Katika mazingira kama ya viwanja vya ndege vya Bukoba, Kigoma, Musoma na Mwanza ambavyo viko karibu na ziwa au maji, ni vyema serikali kufikiria kuwafundisha mafunzo ya kutoa huduma za dharura na uokoaji wananchi wa kawaida kama wavuvi na vijana wanaoishi jirani.

Hawa ni wale wanaokaa mialoni au dagoni ama kambi za wavuvi zilizo karibu na bahari au ziwani kuwapa mbinu za kuokoa na kunusuru maisha iwe wakati wa ajali za boti, vivuko, meli na ndege, ili kupunguza athari mbaya kama hizi za ndege ya Precision iliyotokea Jumapili.

Ni vyema hatua ya kwanza na muhimu iwe kuunda mifumo ya huduma za dharura katika mazingira hayo ya uokoaji au kuwapo kwa jeshi la uokoaji na zima moto hazijafanikiwa, lakini pia hakuna hospitali jirani.

Inawezekana kama kungekuwapo na vijana wenye mafunzo ya namna ya kuokoa abiria ndege inapoangukia baharini au ziwani, huenda tatizo lisingekuwa kubwa. Lakini pia, waokoaji hao wapewe maelekezo ya kukaa kwenye maeneo yao hasa nyakati za mvua na dhoruba kali ili linapojitokeza tatizo wawe wa kwanza kusaidia.

Wakati mwingine kuna taarifa kuwa kwenye mikondo mikali iwe ziwani au baharini kuna matatizo ya ajali, hivyo ni vyema maeneo hayo yakatazamwa, taifa lisijisahau, kwa sababu meli kama MV Sikirgit ilitumbukia kwenye mkondo wa Nungwi, ni vyema kama maeneo yanafahamika kuwa ni hatarishi yasisahaulike.

### MBINU MCHANGANYIKO

Dunia ya sasa ni ya teknolojia za kielektroniki na mbinu mbalimbali za uokoaji ni za kisasa, lakini Tanzania haijafika huko ni vyema zikatumiwa hata za kiasili.

Vijana hawa watakaopewa mafunzo waruhisiwe pia kutumia mbinu za uokoaji za kiasili wanazozijua katika kunusuru maisha ya waathiriwa wa ajali.

Inawezekana wavuvi wanafahamu utaalamu wa asili, wasipuuzwe kwani katika kusaidia majeruhi kilichozoeleka ni "kumchukua majeruhi na kumkimbiza" kwenye hospitali au kwa wahudumu wa msaada wa kwanza kabla ya hospitali.

Wafundishwe namna ya kudhibiti kiwewe au kufadhaika miongoni mwa wathirika na mwisho kushirikiana na huduma rasmi ya kitaifa ya zimamoto, uokoaji na 'ambulensi' kuwasaidia.

Ni vyema pia serikali ikafikiria kuweka vitu kama 'kraine' kuinua ndege, boti au meli ziwani na 'ambulensi', vituo vya afya vya kisasa kwenye viwanja hivyo, ili kukoa maisha na kuongeza usaidizi kwenye matukio ya ajali.

Uwezo wa Tanzania kuokoa waathirika wa ajali si mkubwa na wa kisasa, lakini ni vyema kubadilika na kujiongeza. Ni wazi kuwa hata zinapotokea ajali za magari yaliyoanguka uokoaji hutegemea kiwango cha uharibifu wa gari.

Lakini mara nyingi, waokoaji wanakosa vifaa muhimu vya kukata magari yaliyopata ajali. Kwa mfano mara nyingi, watu hutumia shoka, mapanga na chochote kinachoweza kupatikana kukata gari ili kuwaokoa waathirika.

Wakati mwingine watu wanaweza kuwaumiza zaidi majeruhi kwenye mchakato huo. Hali ni mbaya ajali inapotokea gari likashika moto ni vigumu kuwaokoa majeruhi inakuwa ngumu sana kwa sababu watu hawajafunzwa kuzima moto kwenye gari linalowaka, hivyo vijana na vikundi jamii vingepewa mafunzo kama itakavyokuwa kwa wavuvi baharini au ziwani.

Kilichoonyeshwa na Jackson Majaliwa kwenye ajali ya Bukoba kimedhihirisha kuwa ingawa watu wengi hawajafunzwa kutoa huduma ya kwanza na uokoaji kupitia juhudi wanazofanya wenyewe, wameweza kuwaokoa manusura wengi na hilo limewapatia uzoefu, kwa hiyo serikali sasa ingeanza kushirikiana na jamii kuokoa iwe baharini, ziwani, mitaani na barabarani.

# Ni Ulaya ya kinamama uelekeo usawa kijinsia,

## • Ni viongozi wakuu, kuanzia EU hadi serikalini



Rais wa Kamisheni ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen



Magdalena Andersson Waziri Mkuu wa Sweden

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

KUTOKA Liz Truss wa Uingereza aliyeng'oka karibuni hadi Sanna Marin , Waziri Mkuu wa Finland kuanzia 2019 hadi leo ndiyo wanawake walio madarakani kote Ulaya, wakiongoza serikali na mataifa yenye changamoto kubwa kuanzia vita ya Ukaraine, mabadiliko ya tabianchi na midororo ya kiuchumi.

Kiongozi wa siasa kali za mrengo wa kulia wa Italia Giorgia Meloni, kadhalika anaongoza Italia akiungana na kundi la wanawake viongozi wanaoshikilia nyadhifa za juu za kisiasa kwenye mataifa yao.

Orodha ya marais na mawaziri wakuu wanawake, inaanza na Ursula von der Leyen, ambaye amekuwa Rais wa kwanza mwanamke wa Tume ya Ulaya (EU) jukumu alilolianza Desemba 2019.

Uingereza, ambayo ni sehemu ya Umoja wa Ulaya lakini si mwanachama wa EU tena, Liz Truss alikuwa Waziri Mkuu kuanzia Septemba 6, lakini sasa amejiuzulu na nafasi yake inabebwa na Rishi Sunak.

Anachukua nafasi hiyo kutokana na Boris Johnson kujiuzulu Julai mwaka huu baada ya Theresa May kutakiwa kuachia ngazi na baraza lake la mawaziri, lililomfanyia uasi.

Lizz anakuwa waziri mkuu wa tatu mwanamke wa nchi hiyo baada ya "Iron Lady" Margaret Thatcher, aliyeongoza tangu 1979 hadi 1990 na Theresa May, ambaye aliongoza kuanzia 2016 hadi 2019 , wote wa ni wa chama cha Conservatives.

Nchini Denmark, kiongozi wa chama cha Social Democrat Mette Frederiksen, anakuwa Waziri Mkuu mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kutokea nchini mwake akianza kazi Juni 2019 alipochaguliwa akiwa na miaka 41.

Waziri mkuu mwanamke wa kwanza wa Denmark alikuwa Helle Thorning-Schmidt, pia kutoka chama cha Social Democrats, akiongoza kutoka mwaka 2011 hadi 2015.

Nchini Estonia, mhariri wa zamani wa EU Kersti Kaljulaid (52), ni rais wa kwanza mwanamke wa jimbo la Baltic la Estonia, jukumu analolianza Oktoba 2016. Nafasi hiyo ni ya kiheshima zaidi siyo kuwa na majukumu mazito ya kiserikali ya kutekeleza.

Kaja Kallas mnamo Januari 2021 alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza mwanamke wa Estonia, baba yake Siim Kallas, alishika wadhifa huo kuanzia 2002-2004.

Finland Desemba 2019, ilimpata Sanna Marin, Mwanademokrasia wa Kijamii, alikuwa waziri mkuu mdogo kabisa duniani akiwa na umri wa miaka 34.

Anakuwa Waziri Mkuu wa tatu wa kike nchini humo na amekuwa kwenye vichwa vya habari kuhusu picha zake akicheza dansi na karamu na marafiki zake wakijirusha na 'kula bata'.

Ufaransa haijaachwa, Elisabeth Borne, mhandisi mwenye umri wa miaka 61, akiteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Ufaransa Mei mwaka huu.

Akiwa mwanamke wa pili kushika wadhifa huo baada ya Edith Cresson, Msoshalisti, ambaye alishikilia kazi hiyo chini ya mwaka mmoja mwanzoni mwa miaka ya 1990.



Rais wa Ugiriki Ekaterini Sakellaropoulou

Nchini Ugiriki Katerina Sakellaropoulou, wakili mkali, alichaguliwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke wa Ugiriki Januari 2020.

Wakati urais ni jukumu la heshima nchini Ugiriki, Sakellaropoulou tayari alikuwa amevunja msingi mpya katika mahakama kwa kuwa rais wa mahakama kuu ya nchi hiyo mwaka 2018.

SWEDEN ILIJISAHAU

Licha ya kuwa nchi ambayo inatetea usawa wa kijinsia, haikuwahi kuwa na mwanamke kama waziri mkuu kabla ya Magdalena Andersson ambaye ni wabmrengo wa wanademokrasia wa kijamii, akishinda nafasi ya juu ya uongozi wa serikali Novemba 2021.

Lakini akajiuzulu Septemba 14, 2022 baada ya kambi ya mrengo wa kulia na ya mrengo mkali wa kulia kushinda kwa kiasi kidogo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huo.

Nchini Hungary yuko Katalin Novak, mshirika wa karibu wa Waziri Mkuu Viktor Orban, na waziri wa zamani wa sera ya familia, ni rais wa kwanza mwanamke wa Hungary akiingia ikulu rasmi Machi 2022. Hata kwake urais ni jukumu la kiheshima na si kazi ya kuiongoza nchi kwa kutekeleza mikakati ya kiuchumi na kijamii ili kufikia maendeleo.

**BARANI AFRIKA**

Kwa sasa bara hilo lina viongozi wawili wanawake ni Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa Raia kuanzia Machi 19, 2021 akiongoza awamu ya sita. Ndiye Rais wa kwanza mwanamke wa Tanzania, lakini pia kwa Afrika Mashariki.

Ethiopia yuko mwanamama Sahle-Work Zewde ni Rais wa Ethiopia kuanzia Oktoba 2018 hadi sasa, Rais wa Ethiopia ndiye mwanamke pekee kati ya Marais 54 barani Afrika waliochaguliwa kwa kura.

Anachukua wadhifa huo Oktoba 25, 2018 baada ya kuchaguliwa kwa kauli moja na wajumbe wa Bunge la Kitaifa, kabla ya kuchaguliwa kuwa Rais, alikuwa Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres katika Umoja wa Afrika Ofisi ya Umoja wa Mataifa UN.

**WALIOSHIKA WADHIFA**

Yupo Meenah Gurib-Fakim, Rais wa Mauritius kuanzia Juni 2015 hadi Machi 2018. Ameenah alikuwa Rais wa kwanza mwanamke wa Mauritius kuanzia 2015 hadi 2018. Alichaguliwa kuwa mgombea urais mwaka wa 2014 kufuatia kujiuzulu kwa Rais wa wakati huo Kailash Purryag.

Catherine Samba, Kaimu Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kati (Januari 2014 - Machi 2016)

Catherine Samba Panza alikuwa Kaimu Mkuu wa Nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati kuanzia 2014 hadi 2016. Alikua Rais wa mpito wakati kiongozi wa waasi Michael Djotodia alipojiuzulu urais wake aliojiteua. Kabla ya kuchukua jukumu hili, alikuwa meya wa mji mkuu wa Bangui kuanzia 2013 hadi 2014.

Kutoka Malawi yuko Joyce Hilda Banda, kuanzia Aprili 2012 hadi 2014, alichukua uongozi kufuatia kifo cha Rais Bingu wa Mutharika. Joyce Alikuwa Rais wa nne wa nchi. Pia alikuwa Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke nchini humo kuanzia Mei 2009 hadi Aprili 2012.

Mwaka 2014, jarida la Forbes lilimtaja Rais Banda kuwa mwanamke wa 40 mwenye nguvu zaidi duniani na mwenye nguvu zaidi barani Afrika.

***MITANDAO***

# Maulid Mtulia, anapotangaza kuona pambazuko jipya la kidemokrasia

## •Ipo mikutano ya vyama vya siasa, asema bado yupo CCM

**Na Sabato Kasika**



Maulid Mtulia (katikati) alipoibuka mshindi wa ubunge, katika uchaguzi mdogo wa marudio Kinondoni. **PICHA: MTANDAO**

"NINAONA dalili njema za kuimarika kwa utengamano, demokrasia, utulivu wa kisiasa, huenda miezi michache ijayo tukashuhudia vyama vya upinzani vikiendelea na mikutano ya hadhara iliyozuiwa miaka sita iliyopita".

Huo ni utabiri wa mbunge wa zamani wa Kinondoni (CCM), Maulid Mtulia, wakati akizungumza na gazeti hili baada ya kumsaka kufuatia ukimya na hasa kutoonekana kwenye anga na majukwaa ya kisiasa, tangu alipoachia ubunge wa jimbo hilo 2020.

Kwanza Mtulia anasema, hajaachana na siasa ni mwana CCM, bali ukimya wake unatokana na majukumu mengine ya kuitumikia jamii kwa njia nyingine ambayo yamesababisha asisikike kama ilivyokuwa kwenye nyanja hiyo.

"Bado nipo CCM na nitaendelea kuwapo kwenye siasa ila si ubunge, kwani sina mpango wa kuwania ubunge uchaguzi ujao, kwa sababu ni mchakato unaohitaji maandalizi na ukwasi, lakini sijafanya maandalizi yoyote," anasema mwanasiasa huyo.

Anafafanua kuwa mwisho wa uchaguzi ni mwanzo wa uchaguzi mwingine, na kwamba baada ya uchaguzi wa mwaka 2020, hakufanya maandalizi, hivyo hali hiyo inatosha kutambua kuwa hana mpango wa kuwania ubunge tena jimboni humo.

Aidha, Mtulia aliyejiuzulu ubunge wa Kinondoni kupitia CUF na kujiunga CCM kuungana mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano ya John Magufuli katika kuwaletea wananchi maendeleo, anaona kuwa kuna badiliko linalotarajiwa kuruhusu vyama vingine kuwa na uhai kwenye jamii , baada ya serikali aliyoiunga mkono ya awamu ya tano kuvipa likizo ya kufanya mikutano ya kisiasa.

Mbunge huyo aliwekwa kando na nafasi yake ilichukuliwa na Abbas Tarimba, ambaye ndiye chaguo la ubunge wa Kinondoni mwaka 2020, anasema kuna mabadiliko yanatokana na msimamo wa sasa wa kisiasa na uongozi akieleza kuwa hali ya demokrasia nchini imebadilika kuliko ilivyokuwa miaka sita iliyopita.

### KIPYA ANACHOOONA

Mtulia anasema, miaka sita iliyopita hakukuwa na mahusiano ya karibu kati ya viongozi wa vyama vya upinzani na serikali, na kwamba kwa sasa yapo hali ambayo mwanasiasa huyo anabainisha kuwa hizo ni dalili njema kuwa milango ya kuruhusu mikutano ya kidemokrasia inafunguliwa.

"Ni kwamba, hali ya kisisa imekuwa tofauti kabisa katika kipindi ambacho Rais Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani. Kuna utulivu wa kisiasa na tunategemea miezi michache ijayo, vyama vya siasa vitaanza kufanya mikutano ya hadhara ambayo ilizuiwa miaka sita iliyopita," anakumbusha Mtulia.

Anaongeza kuwa kitendo cha Rais kuunda kikosi kazi cha kukusanya maoni ya wananchi kuhusu jinsi ya kuendesha siasa, kinaonyesha amedhamiria kuwaunganisha Watanzania bila kujali itikadi za vyama vyao na kuipa demokrasia uwanja mpana zaidi . "Ninaona dalili za utangamano, kwani kwa sasa wanasiasa wanaaminiana, siyo kama miaka iliyopita, hivyo tuendelee kumuombea Rais wetu aendeleze maono hayo ya kuwaunganisha Watanzania," anasema.

Mwanasiasa huyo pia anaamini kwamba, kwa hatua ambazo Rais anachukua za kuimarisha demokrasia, uchaguzi wa mwaka 2025 utakuwa wa amani, huru na haki pamoja na kukubalika ili Watanzania wapate viongozi wanaowataka.

"Ninakubaliana na kauli ya Rais kwamba, Tanzania ni yetu sote tunapaswa tuijenge kwa pamoja bila kutengenishwa na itikadi za vyama. Hivyo tumuunge mkono afanye kazi ya kutuletea maendeleo," anaongeza.

### CHANZO UKIMYA

Mwanasiasa huyo anasema kwa sasa ni mjumbe wa taasisi ya Munazamat Al Daawa Al Islamia (MDI), ambayo inafanya kazi ya kujenga shule na kuziendesha, kuchimba visiwa vya maji na kujenga misikiti.

> "Tunafundishaa somo la dini shuleni, kufuturisha wanafunzi, wafungwa na wasiojiweza mwezi wa Ramadhan, kugawa sadaka kwa watu wenye mahitaji wakati wa Idi Eli Haji au ya kuchinja," anasema.

Anasema taasisi hiyo pia inajenga vyuo vya afya, vyuo vya ualimu na ufundi na kuviendesha, kutafsri vitabu vya dini, kuvigawa, kufundisha, kuendesha semina na makongamano ya kitaifa na kimataifa.

Mtulia anaendelea kutaja majukumu ya taasisi hiyo kuwa ni kujenga maadili ya dini na kuyasimamia, kuwafadhili masomo wanafunzi wa ngazi zote ndani na nje ya nchi, kufadhili ibada ya hija kwa waislam wasio na uwezo wa kifedha.

"Tunafundishaa somo la dini shuleni, kufuturisha wanafunzi, wafungwa na wasiojiweza mwezi wa Ramadhan, kugawa sadaka kwa watu wenye mahitaji wakati wa Idi Eli Haji au ya kuchinja," anasema.

### AKUMBUSHIA YA 2017

Desemba 2 mwaka 2017 Mtulia wakati huo akiwa mbunge wa Kinondoni kupitia CUF, alijiuzulu nafasi hiyo na kukihama chama hicho akijiunga na CCM, huko akateuliwa kuwania nafasi hiyo katika uchaguzi mdogo wa marudio uliokuwa na vurugu zilizosababisha kifo cha Akwilina Akwiline

mwanfunzi wa Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam.

Alipigwa risasi wakati wa vurumai za kupinga mwenendo wa uchaguzi katika jimbo la Kinondoni.

Katika uchaguzi huo, Mtulia aliibuka mshindi na kutumikia nafasi hiyo hadi mwaka 2020 alipoangushwa kwenye kura za maoni na tangu wakati huo amekuwa hasikiki tena kwenye majukwaa ya siasa.

Wakati anajiuzulu, alisema alifanya hivyo kwa utashi wake bila shinikizo la mtu, na kudai kuwa uzoefu aliokuwa ameupata kwa miaka miwili ya ubunge, alibaini kuwa serikali ya CCM inafanya kazi kubwa katika mambo mengi ambayo upinzani uliahidi kuytekeleza.

Aidha, akafafanua kuwa nia yake ni kuwatumikia wananchi, na haoni sababu ya kuendelea kuwa upinzani na badala yake anaona ni vyema aungane na juhudi za serikali, kwa kumuunga mkono Rais wa awamu ya tano John Magufuli na serikali yake katika kuwaletea wananchi maendeleo.

# JUKATA: Mikutano ya hadhara vyama vya siasa si ya kusubiri majadiliano, ipo kisheria

**Na Sabato Kasika**


Bob Wangwe

TANGU mwaka 2016, serikali ilivielekeza vyama vya siasa vya upinzani kuwa ni wakati wa kukaa kimya na kuachana na majukwaa ya mikutano ya hadhara na maandamano, kwa sababu, uchaguzi umemalizika na kinachobaki ni kujenga nchi.

Ni tamko linalotolewa na serikali baada ya Rais John Magufuli, kuchukua usukani, akisisitiza kuwa uchaguzi ukimalizika, kinachofuata ni kujenga taifa tena kwa kutumia kauli mbiu kuwa 'hapa kazi tu.'

Kuanzia hapo lilianza katazo la kufanya mikutano ya hadhara na maandamano ya kisiasa, hata vikao vya ndani ilikuwa vigumu kuvifanya, ikielezwa kuwa taarifa za kiintelijensia zimebaini uwepo wa mambo ya uvunjifu wa amani.

Hata hivyo, tangu wakati huo kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wanasiasa na wadau wa watetezi wa masuala ya kidemokrasia kuhusu maelekezo hayo na kwamba yanakwenda kinyume na Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 na katiba pia.

Malalamiko hayo ya vuta nikuvute, yalihitimishwa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuunda kikosi kazi kwa lengo la kuja na maoni ya jinsi ya kufanya mikutano hiyo pamoja na mambo mengine.

Miongoni mwa mambo hayo yenye lengo la kuimarisha demokrasia ya siasa ya vyama vingi, ni kuwapo kwa katiba mpya na tume huru ya uchaguzi, ambapo kikosi kilikusanya maoni ya watu na kumkabidhi Rais Samia huku, baadhi ya mapendekezo yakiwa ni kutaka kuwapo kwa mikutano ya hadhara na matokeo ya uchaguzi wa rais kuhojiwa mahakamani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, anasema suala la mikutano ya hadhara, halihitaji mjadala, kwa maelezo kwamba lipo kisheria na kwamba kinachofanyika ni kuvuta muda bila sababu.

"Kuzuia mikutano hiyo ya vyama vya siasa kunasababisha vishindwe kutimiza majukumu ya kuendesha shughuli za siasa, hivyo hili jambo lisingesubiri uamuzi kwani lipo kisheria kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa ya mwaka 1992 na marekebisho yake," anasema Wangwe.

**MAZINGIRA MAGUMU**

Wangwe anasema, vyama makini vimebanwa kufanya mikutano ingawa sheria namba tano ya vyama siasa ya mwaka 1992 iliyorekebishw mwaka 1999 inaviruhusu kuendesha shughuli za kisiasa.

"Vyama vya siasa vimeruhusiwa kwenye sheria mama ambayo ni katiba ya nchi na hata sheria namba tano ya vyama vya siasa ya mwaka 1992, lakini imewekwa pembeni na sasa vyombo vya dola haviizingatii," anakumbusha.

Anasema, vyama vya siasa vinapotaka kufanya mkutano, vinatakiwa kutoa taarifa polisi ili kuweka ulinzi, na kwamba badala yake vinazuiliwa kufanya mikutano kwa madai ya sababu za kiusalama.

"Kama polisi wanaona kuna tatizo la kiusalama, ni vyema wakaongeza ulinzi kulikabili kuliko kuzuia mkutano, hali ambayo inachangia kuvifanya vyama vya siasa vishindwe kujinadi kwa Watanzania," anasema.

Mkurugenzi huyo anaongeza kuwa, wakati vyama vya upinzani viwekewa masharti, chama tawala kinaendelea kufanya ziara na mikutano na hadhara, bila kuwekewa mizengwe na vyombo vya dola.

Anasema, kwa mazingira kama hayo, vyama vya upinzani hawezi kujitanua, kutokana na ukweli kwamba vinabanwa na hata vikisajiliwa vipya, vitajikuta vikibaki bila kuwa na wanachama.

"Kwa mtazamo huu suala la mikutano hiyo liachwe kama lilivyo, ili wanasiasa waendelee na kazi zao ikiwamo kutafuta wanachama, kuwapa Watanzania elimu ya uraia na mambo megine muhimu," anasema.

**VYAMA HAVIJIIMARISHI**

Wangwe anasema mojawapo ya mambo ambayo huzingatiwa

> "Kama polisi wanaona kuna tatizo la kiusalama, ni vyema wakaongeza ulinzi kulikabili kuliko kuzuia mkutano, hali ambayo inachangia kuvifanya vyama vya siasa vishindwe kujinadi kwa Watanzania," anasema.

wakati Msajili wa Vyama vya Siasa anapofanya ziara ya kukagua vyama hivyo, ni kama vina ofisi Bara na Zanzibar.

"Sasa kama chama hakifanyi mikutano kinawezaje kujitanua na kupata wanachama wa kukiwezesha kujiimarisha? Mikutano ya ndani haiwezi kuimarisha chama cha siasa," anaeleza Wangwe.

Anafafanua kuwa mikutano ya aina hiyo huwa ni ya viongozi, na kwamba kuwapo kwa mikusanyiko ya hadhara ya vyama kunaweza kuvisaidia kupata wanachama wengi zaidi kuliko kuliko kuwa kimya.

Mkurugenzi huyo anasema mazingira ya sasa ya kisiasa yameifanya Tanzania kuwa na vyama 19 vya siasa kama CCM, CHADEMA, NCCR-Mageuzi, ACT-Wazalendo, CUF na CHAUMMA,

"Vimebakia 19 baada ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kufuta vitatu vya Jahazi Asilia, Chama cha Haki na Ustawi (CHAUSTA) na APPT- Maendeleo," anasema.

Msajili huyo anatoa sababu mbalimbali za kufuta vyama hivyo, ikiwamo kutotimiza masharti ya kuwa na ofisi ya chama Tanzania Bara na Zanzibar kwa mujibu wa kifungu cha 10(d) na pia kutokuwa na wanachama Zanzibar kwa mujibu wa kifungu cha 10(b).

"Hapa ndipo kwenye tatizo hasa kutokana na utaratibu wa sasa wa vyama kuzuiliwa kuendesha shughuli za siasa, hali ambayo ninaamini inachangia kuvifanya vidumae na visiwe na ofisi."

Anasema, chama ni wanachama, na kwamba kama wanachama hawapo, inakuwa ni vigumu chama kujiendesha au kuwa na ofisi, ambapo anashauri sheria namba tano ya vyama vya siasa ifuatwe, kwa ustawi wa vyama hivyo.

Anaeleza kuwa wakati msajili akitekeleza takwa hilo la kisheria kwa kufanya ukaguzi na uhakiki wa vyama, ni vyema pia takwa hilo la kisheria likazingatiwa kwenye upande wa kuruhusu vyama kufanya mikutano ya hadhara.

"Sheria namba tano ya vyama vya siasa ikizingatiwa tutavijua vyama makini vinavyokubalika kwa wananchi, kwani ni ukweli usiofichika kwamba, vina mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi hii," anasema.

JUKWAA LA VIONGOZI

JENERALI MUHOOZI KAINERUGABA

# Mwanawe Museveni aliyesheheni vijimambo

- Yuko na Urusi vita Ukraine, adai kuiteka Nairobi
- Ana mahaba na waasi wa Tigray Ethiopia
- Atia nia kumuondoa babake Ikulu kisa ...



Baba Yoweri Museveni (kushoto) na mwanaye Muhoozi Kainerugaba , aliyetangaza kumrithi. **PICHA: MTANDAO**

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

MTOTO wa Rais Yoweri Museveni wa Uganda Jenerali Muhoozi Kainerugaba Museveni (48) mwenye cheo kikubwa kuliko yeyote kwenye jeshi la nchi hiyo, amemaliza mwezi kwa kuibua mjadala , akitangaza kutia nia ya kumrithi baba yake.

Ni baada ya kutangaza rasmi kuwa anaazimia kuwa rais wa Uganda, au kupokea kijiti kutoka kwa Museveni, akieleza kuwa atafanya hivyo kwa heshima ya mamake mzazi.

Muhoozi, asiyeishiwa vituko, taarifa yake inapokelewa na wachambuzi mbalimbali wa masuala ya kisiasa, wanaosema ujumbe huo unaiweka Uganda katika joto la kisiasa , ikiwa imebakia miaka 3.6 kabla ya kufanyika uchaguzi wa rais na wabunge.

Miaka ya nyuma dalili za Jenerali Muhoozi kuonyesha nia ya kuwa rais wa Uganda zilipuuzwa, lakini safari hii kufuatia ujumbe wake kwenye mtandao wa Twitter ni dhahiri kwamba azma hiyo imekuwepo na anaizingatia kwa dhati.

Katika ujumbe huo ametaja sababu kuwa anataka kuwa rais wa Uganda na hilo litatokea 2026.

**KINACHOMSUKUMA**

Jenerali Muhoozi anaongeza kusema kuwa hii itakuwa ni kwa heshima ya mama yake mpendwa Janet Museveni, ambaye katika ujumbe uliotangulia wa kutangaza nia, alimtaja mama yake kuwa kama malaika wake asiye na mfano. Ujumbe huu umewaingiza raia mbalimbali katika mjadala kuhusu nini anachopanga Rais Jenerali Yoweri Museveni kuhusiana na urithi kwa wadhifa wa urais.

Hivi karibuni makundi mbalimbali ya vijana yameshuhudiwa yakifanya maandamano ya kumuunga mkono Muhoozi kuwania urais. Waandmanaji wanavalia fulana na kuonyesha mabango yenye ujumbe huo wakipitia barabara za miji mbalimbali.

Licha ya kwamba Rais Museveni mwenyewe hajataja nia yake kuwania urais mwaka 2026, anaweza kufanya hivyo baada ya kufuta kipe ngele cha ukomo wa umri wa kugombea urais nchini Uganda.

Lakini pia hakuna ukomo wa kukaa ikulu, wakati nchi nyingi za Afrika Mashariki ikiwamo Kenya na Tanzania kuna ukomo ni miaka 10 kwa mihula miwili ya miaka mitano.

**MUSEVENI AGWAYA**

Kuna methali kuwa mkuki kwa nguruwe mtamu lakini kwa binadamu mchungu, ni kwa sababu ,hapo awali maofisa wa jeshi walioonyesha nia ya kushiriki siasa walichukuliwa hatua za kisheria.

Aidha, walifunguliwa mashtaka au kuwekwa katika vizuizi na baadhi yao ni Jenerali Henry Tumukunde na David Sejusa.

Hata hivyo, kwa Muhoozi mkuki, umekuwa mchungu hakuna hatua za kisheria zilizochukuliwa kwa jenerali huyo ambaye ni ofisa mwenye cheo cha juu zaidi jeshini. Wafuatiliaji wanasema ukimya huo unaleta mtazamo kuwa hali hiyo inaleta mkanganyiko katika taasisi hiyo kuhusiana na uhusika wao katika siasa za nchi kuwa kuna wasiosemeshwa na wanaokemewa.

Licha ya Rais Museveni kumtaka mwanawe asiendelee kutumia mitandao ya kijamii kusambaza ujumbe wenye hisia za kisiasa, ujumbe huo wa hapo wa safari hii unaonyesha kuwa Jenerali Muhoozi hajazingatia ushauri wa baba.

**VIJIMAMBO VYA AJABU**

Ujumbe wa tweeter wa Jenerali Muhoozi ulianza kuzusha hasira nchini Kenya, ni baada ya kusema itamchukua yeye na jeshi lake wiki mbili kukamata Nairobi jijini na makao makuu ya serikali ya Kenya.

Matamshi hayo kwenye maandishi yaliyotolewa mwezi uliopita yalizusha hisia kali zikiwamo poa shutuma nyingi miongoni mwa rai hata na viongozi si Kenya pekee bali hata Uganda kwenyewe.

Kufuatia tambo hizo , Rais wa Uganda Yoweri Museveni, alimuondoa mwanae, Jenerali Muhoozi kwenye nafasi ya kuwa Kamanda wa Kikosi cha Jeshi la Ardhini-nchi kavu, baada ya kutuma ujumbe kwenye Twitter kwamba atauteka mji mkuu wa Kenya Nairobi baada ya wiki mbili.

Na kuondolewa kwa Museveni mtoto madarakani kwenye kamandi ya ardhini, kulikuja na kupandishwa cheo na kuwa jenerali wa nyota nne, cheo cha juu zaidi katika jeshi la Uganda.

Ujumbe huo wa kuiteka Nairobi ulianzisha msururu wa mikutano ya kidiplomasia kati ya nchi zote mbili katika miji mikuu, Kampala na Nairobi.

Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uganda ililazimika kuingilia kati na kutoa taarifa ikisema bado ni majirani wema na Kenya na kufafanua kuwa serikali ya nchi hiyo haifanyi sera za kigeni kupitia mawasiliano ya mitandao ya kijamii.

Msamaha wa umma kutoka kwa rais kwa mwenzake wa Kenya, William Ruto, ulifuata baada ya muda mfupi.

Kwa upande wake, Muhoozi Kainerugaba alikuwa kimya, akisema alipigiwa simu na baba yake na kwamba 'tweets' zake "zimewaogopesha Wakenya sana", lakini hakuomba msamaha hasa.

**MAHABA NA TIGRAY**

Wakati huo huo, kabla mawimbi hayajatulia bahari iliyochafuliwa na kitisho kwa Kenya, Muhoozi, alitangaza kuwaunga mkono waasi wa jimbo la Tigray wanaopambana na serikali ya Ethiopia.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Uganda pia alifanya mkutano na Balozi wa Ethiopia kufuatia ujumbe mwingine wa Twitter wa Muhoozi akielezea kuwaunga mkono waasi eneo la kaskazini la Tigray.

Anasema kwenye ujumbe: "Tigray is always in my heart! It was an order from my God, Jesus Christ, to love and defend Tigray. Greetings to my tribe."

Unaotafsirika "Tigray daima iko moyoni mwangu! Ilikuwa ni agizo kutoka kwa Mungu wangu, Yesu Kristo, kumpenda na kumtetea Tigray. Salamu kwa kabila langu."

Kwa miaka mingi, jenerali huyo, ambaye wengi wanaamini kuwa anaandaliwa kumrithi babake kama rais mtarajiwa wa Uganda, amekuwa mtumiaji wa Twitter kwa bidii kwa namna ambayo imewahi kulinganishwa na Rais wa zamani wa Marekani Donald Trump.

Museveni, amekuwa madarakani tangu 1986 anasubiriwa atafanya nini kwenye uchaguzi mkuu wa 2026 , baada ya kuondoa kipengele cha ukomo wa madaraka ya rais kwenye katiba ya Uganda.

**MUHOOZI ALIKOANZIA**

Ilianza mwaka 2013, wakati huo Rais wa Uganda alifanya mabadiliko makubwa katika jeshi, na kumuondoa Mkuu wa Jeshi kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani kisha kumpa kazi hiyo jenerali mwingine anayesimamia vikosi vya ardhini.

Yoweri Museveni alimteua Jenerali Katumba Wamala kuwa Mkuu mpya wa Majeshi ya Ulinzi (CDF) na Jenerali Aronda Nyakairima kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani katika mabadiliko ambayo pia yaliathiri baraza la mawaziri.

Marekebisho hayo yalifanywa baada ya kuibuliwa madai kuwa kulikuwa na barua iliyovuja iliyochapishwa na gazeti la Daily Monitor , ikisema kuwa serikali inapanga kuwauwa majenerali wakuu jeshini wanaompinga mtoto wa Rais Museveni Muhoozi kumrithi baba yake kama kiongozi wa nchi.

Aronda alikuwa mmoja wa maofisa waliotajwa kwenye barua hiyo iliyovujishwa na Jenerali David Sejusa, ambaye alikuwa akiongoza kitengo cha jeshi kinachoratibu ujasusi wa kitaifa na kimataifa ambaye wakati huo alikuwa nje ya nchi.

Gazeti la Daily Monitor, limevamiwa na vikosi vya usalama ambavyo viliwazuia wafanyakazi kuingia katika majengo yake kwa siku kadhaa na kuendesha upekuzi kusaka ukweli wa taarifa hizo.

***MITANDAO***

# Shaka ajigamba uchaguzi CCM, makada kibao wameingia ulingoni

INATOKA UK. 13

kwenye uchaguzi.

"Hatutasita kuchukua hatua popote tutakapoona kuna jambo lisilokuwa na heri kwenye chama chetu, hivyo ni muhimu walioomba nafasi za uongozi ngazi ya mkoa kufuata kanuni na taratibu za chama," anasema Chongolo.

Akiwa Kigamboni Dar es Salaam, nakemea rushwa ndani ya chama na kusema walishabaini baadhi ya watu kufanya rafu kwa kukiuka taratibu na kusababisha kufutwa kwa uchaguzi katika wilaya 21 na kurudiwa upya.

"Niwatadharishe kuwa katika ngazi ya mkoa macho yetu yako wazi, tunatazama mchakato kwa karibu na hatutasita kuchukua hatua popote tutakapoona kuna jambo lisilokuwa na heri kwa chama chetu," anaonya.

Aidha, anasema kumekuwapo na baadhi ya wanachama ndani ya CCM wanaotengeneza miundombinu haramu ya kuwadhibiti watu wazuri wasipate nafasi za uongozi katika uchaguzi.

"Nitoe angalizo kwao waache mara moja vitendo hivyo, kwani idadi ya mikoa 32 iliyopo ni michache na haitawashinda kupitia jina mojamoja katika orodha ya walioomba kuchaguliwa kubaini ujanja huo," anasema.

Komredi Chongolo anasema yeye na viongozi wenzake watapitia maelezo binafsi na mengine, kwa ajili ya kujiridhisha kwa kila mtu, ili wapate viongozi ambao wanafanana na mazingira na wana dhamira ya kweli ya kuendeleza utumishi na uhai wa chama hicho mbele, na siyo bora viongozi.



Abbas Mtemvu



Kate Kamba




Salum Madenge

"Hivyo niwaambie kuwa katika hilo wala nisiwadanganye, kwani hatutaacha kulifanya mara tu tutakapoona kuna jambo lisilokuwa na heri kwenye chama chetu, ikiwamo rushwa," anaonya

**MALAIKA WASHUKE**

Makamu Mwenyekiti wa CCM, Tanzania Bara, Abdulraman Kinana, anatamani malaika washuke, ili wajumbe wasishawishike kuchukua rushwa kutoka kwa makada wanaowania uongozi katika nafasi mbalimbali..

Ni katika ziara yake katika mikoa mbalimbaali anaonyesha kukerwa na vitendo vya rushwa katika uchaguzi unaoendelea na kuzitaka kamati za siasa kutofumbia macho watakaobainika kufanya vitendo hivyo, badala yake wawakate kwenye kinyang'anyiro cha kugombea.

"Kiongozi anayesaka madaraka kwa nguvu mpaka kutoa hela, huyo hafai kuwa kiongozi, msitafute viongozi kwa umaarufu au fedha zao, kura hazinunuliwi, msikubali kuuza utu wenu, kwa ajili ya pesa," anasema.

Anasema viongozi wa aina hiyo siku zote huwa hawawatambui wapigakura, hadi uchaguzi mwingine unapowadiwa ndipo wanaanza kupitapita na kuwalaghai. "Natamani malaika awashukie wajumbe, ili msishawishike."

"Katiba ya CCM iko wazi, kila mwanachama ana haki ya kugombea, kuchagua, siyo kununuliwa. Hakuna mwenye hatimiliki ya uongozi, ikiisha miaka mitano mtu yeyote anaweza kugombea,"anasema Kinana.

Anawakumbusha wajumbe kuwa kura ni siri, wasikubali kuuza kura zao kwa vipande vya fedha, watakuwa wameuza uhuru wao, utu wao, na kwamba mtu anayetumia pesa kusaka uongozi wasimchague.

## CHEMSHABONGO NA -00 19 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. wingi wa neno jibu
6. Ubinadamu
8. kitu cha thamani kubwa
10.toa fedha kupata kinachouzwa
11.shauku ya jambo
12.tafuna kitu kigumu
14.kasirika ghafla
16.yenye bei ndogo 18.kibua
19.New Delhi ni mji mkuu
21.mmea wenye mizizi inayofanana na viazi vyeupe
22.mwanzo 23.chukuliwa 24.ugwe

Chini:
1. jina la jadi la watawala wa kichaga 2. kata shauri
3. mahali pasipo na mimea na pia penye uhaba wa maji 4. nyanyua
5. sehemu ya vitu au watu
7. uchepe, ukora 9. wekea ahadi mtu kuwa atatimiza jambo fulani
13.uvunjaji wa kanuni za nchi
15.sarenda 16.fanywa tena
17.vazi la mwanaume la kitambaa la kichwani 20.Sadiki 22.toka

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | | ■ | 6 | | 7 |
| 8 | | | | | ■ | 9 | ■ | ■ | |
| 10 | | | | | ■ | 11 | | | |
| 12 | | | | | 13 | | ■ | ■ | |
| | ■ | | ■ | 14 | | | | 15 | |
| ■ | 16 | | 17 | | | | ■ | | ■ |
| ■ | 18 | | | ■ | 19 | | | | 20 |
| 21 | | | | | ■ | | ■ | ■ | |
| ■ | | ■ | | ■ | 22 | | | | |
| 23 | | | | | | | ■ | ■ | |
| ■ | | ■ | | ■ | | ■ | 24 | | |

## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

ALFABETI
MAPATO
KARAKANA
BANDAMA
UNABII
MLANGO
GHANA
GUNA
ADUI
DHAKA
NAFUU
AMANI
MKOA
EBOLA

ABA
ABU
NAI
AMA
ATIA
GIZA

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ■ | | ■ | |
| | ■ | | ■ | | | | | |
| | | | | | ■ | | ■ | |
| | | | | | ■ | | ■ | |
| ■ | | | | ■ | M | K | O | A |
| | ■ | | | | | | ■ | |
| | | | | ■ | | | | |
| | | | | ■ | | | | ■ |
| ■ | | ■ | ■ | ■ | | ■ | | ■ |
| | | | | | | ■ | | ■ |

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | A | N | A | K | A | ■ | U | M | A |
| A | M | A | L | I | ■ | ■ | ■ | W | ■ |
| R | I | K | A | B | U | ■ | K | A | A |
| A | N | A | S | A | ■ | K | I | N | U |
| O | I | L | I | ■ | M | ■ | F | A | A |
| ■ | ■ | A | R | U | S | H | A | ■ | ■ |
| M | ■ | ■ | I | G | A | ■ | R | A | I |
| I | ■ | U | ■ | A | F | Y | A | ■ | S |
| K | U | R | A | N | I | ■ | N | ■ | H |
| O | ■ | D | ■ | D | R | O | G | B | A |
| A | ■ | U | H | A | I | ■ | A | ■ | ■ |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | B | U | B | U | ■ | ■ | M |
| U | M | A | T | I | ■ | ■ | ■ | K |
| K | A | R | A | B | A | T | I | A |
| U | L | A | F | I | ■ | O | ■ | A |
| ■ | I | ■ | I | ■ | A | K | A | ■ |
| U | ■ | M | T | I | H | A | N | I |
| M | A | L | I | ■ | A | ■ | U | ■ |
| I | G | A | ■ | A | ■ | T | A | I |
| M | A | J | O | S | H | O | ■ | L |
| I | ■ | I | ■ | I | ■ | A | W | A |





# Wananchi 600 kupima magonjwa yasiyoambukiza

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIKA kukabiliana na magonjwa yasiyoambukizwa nchini, Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mbeya inatarajia kutoa huduma ya upimaji wa magonjwa hayo kwa wananchi 600 kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya.

Kwa mujibu wa Mratibu wa magonjwa yasiyoambukizwa Mkoa wa Mbeya, Dk. Deogratius Magongwe, wameandaa wiki ya upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza kwa wananchi ili kutoa matibabu bure kwa wananchi.

Alisema lengo la wiki ya upimaji wa magonjwa yasiyoambukizwa ni kutoa elimu kwa wananchi namna ya kuepukana pamoja na kukabiliana na magonjwa kama vile kisukari, shinikizo la damu, tezi dume, ini pamoja, figo na magonjwa ya afya ya akili.

"Tumeamua kuwa na wiki ya upimaji wa magonjwa yasiyoambukizwa kwa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mbeya, dhumuni letu ni kutoa elimu kwa wananchi kukabiliana na kisukari, moyo, presha figo, shinikizo la damu pamoja na tezi dume magonjwa haya yamekuwa yakigharimu maisha ya watu wa rika zote," alisema Dk. Magongwe.

Aliongeza kuwa miongoni mwa magonjwa 10 yanayosumbua mkoa huo ni shinikizo la damu ambayo husababishwa na mambo mbalimbali kama ulaji wa vyakula usiofaa na msongo wa mawazo.

Alisema awali magonjwa yasiyoambukizwa yaliripotiwa kwenye nchi zilizoendelea, lakini kwa sasa mambo yamebadilika nchi zinazoendelea zimekuwa waathirika wa magonjwa hayo kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), asilimia 70 ya vifo vinatokana na magonjwa yasiyoambukizwa ikiwamo saratani, moyo, tezi dume, figo, ini na presha.

Kutokana na hali hiyo serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kutoa elimu kwa wananchi, kuepukana na magonjwa hayo ambayo yamekuwa yakitumia fedha nyingi kuyatibu na hutumia asilimia 30 ya fedha za matibabu.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya wameishukuru hospitali ya mkoa kuandaa wiki ya upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza kwa kuwa itawasaidia kuokoa gharama za matibabu.

Jesca Ambakisye, alisema magonjwa yasiyoambukiza hutumia gharama kubwa kuyatibu na kwa fursa hiyo ni muhimu wananchi wakashiriki ili kupata ushauri na matibabu.

**Lengo la wiki ya upimaji wa magonjwa yasiyoambukizwa ni kutoa elimu kwa wananchi namna ya kuepukana pamoja na kukabiliana na magonjwa kama vile kisukari, shinikizo la damu, tezi dume, ini pamoja, figo.**

# Wapewa tahadhari kuingia kipindupindu Kyela

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MKUU wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, amewataka wananchi wa wilaya hiyo kuchukua tahadhari dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu ambao tayari umeripotiwa nchi jirani ya Malawi.

Mlawa alitoa tahadhari hiyo juzi, kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kuwa madiwani wana jukumu la kuhamasisha wananchi kuchukua tahadhari ili kuepukana na ugonjwa huo.

Alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa maeneo kila mwaka hukumbwa na ugonjwa wa kipindupindu ambao husababisha watu kuhara, kuumwa tumbo na kutapika.

"Tuchukue tahadhari mapema maana tayari ugonjwa wa kipindupindu umeripotiwa kwa majirani zetu hapo Malawi na sisi tumekuwa waathirika, mwaka huu tujitahidi usiingie maana tayari msimu wa maembe umeanza," alisema Mlawa.

**Ni muhimu wananchi wakazingatia usafi wa mazingira na kanuni bora za afya ikiwamo kuchemsha maji ya kunywa, kuosha matunda na usafi wa mwili.**

Aliiagiza timu ya wataalamu wa afya kuzunguka maeneo yote kutoa elimu kwa wananchi kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo hasa maeneo ya Kata ya Bujonde, Isanga na Ngonga.

Alisema ni muhimu wananchi wakazingatia usafi wa mazingira na kanuni bora za afya ikiwamo kuchemsha maji ya kunywa, kuosha matunda na usafi wa mwili.

Aidha, alisema uongozi wa halmashauri utapita nyumba kwa nyumba kufanya ukaguzi wa ujenzi bora wa vyoo kama agizo la serikali lilivyotaka kwamba kila kaya ijenge choo bora na kisasa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, alisema madiwani wamejipanga kuelimisha wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema moja ya majukumu watakayofanya ni pamoja na kuandaa mikutano ya hadhara ambayo itahusisha wataalamu wa afya kuanzia ngazi ya kijiji, kata kutoa elimu namna ya kuepukana na ugonjwa huo.

"Mwaka huu tumejipanga kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu kila mwaka tumekuwa waathirika wa ugonjwa huo maeneo kama ya Bujonde na Ngonga yanaripotiwa tunawaomba wananchi wetu wazingatie usafi wa mazingira," alisema Kingamkono.



Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mwanza ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini wa Vyuo Vikuu vya Kikatoliki Tanzania, Renatus Nkwande (kushoto), akiweka baraka kwenye majengo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikatoliki Mbeya (CUCoM), kuashiria ufunguzi wa mwaka mpya wa masomo 2022/2023 jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbeya yafanikiwa kupunguza vifo vya uzazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKOA wa Mbeya, umefanikiwa kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na matatizo ya uzazi kutoka 133 kati ya vizazi 100,000 kwa mwaka 2015 na kufikia vifo 102 kwa mwaka 2021.

Pia imepunguza idadi ya vifo vya watoto wachanga kutoka 14 hadi kufikia vinane.

Kadhalika idadi ya wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya huduma za afya imeongezeka kutoka asilimia 77 ya mwaka 2015 na kufikia asilimia 85 kwa mwaka 2021 na kufanya idadi ya wajawazito 70,404 kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma kati ya 83,058 waliolengwa.

Kwa mujibu wa Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga, ambaye ni Ofisa Lishe wa Mkoa alipozungumza na Nipashe, idadi hiyo inatokana na jitihada za serikali kujenga vituo vya huduma za afya, hospitali pamoja na zahanati.

Alisema miongoni mwa mafanikio katika sekta ya afya ni pamoja na ongezeko la vituo vya afya vinavyotoa huduma za dharura kwa wajawazito kutoka vituo viwili kwa mwaka 2015 hadi 11 mwaka 2021.

"Licha ya serikali kuendelea kuboresha huduma za afya kwa kujenga miundombinu rafiki, vilevile imefanikiwa upatikanaji wa dawa muhimu 30 katika mkoa huo, awali ulikuwa asilimia 93.2 na hadi kufikia Desemba mwaka 2021 hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma ulikuwa asilimia 94.6," alisema Sanga.

Kadhalika, serikali kupitia Wizara ya Afya, imetoa Shilingi bilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya mwezi Septemba 2021.

Hivi karibuni Mbunge wa Jimbo la Mbeya vijijini, Oran Njeza, kupitia kikao cha kamati ya ushauri ya mkoa aliomba serikali kuajiri watumishi katika vituo vya afya na zahanati ambavyo alisema kuna upungufu mkubwa.

Alisema serikali imejitahidi kujenga miundombinu rafiki ya kutolea huduma lakini kikwazo ni kukosekana kwa wataalamu wa afya kwa madai kuwa maeneo mengi kuna mhudumu mmoja tu hali inayopunguza ufanisi katika kuwahudumia wagonjwa.





# Maabara Veterinari yajivunia mafanikio

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania, Dk. Stella Bitanyi, amesema wameongeza mapato ya ndani yatokanayo na utoaji wa huduma na usambazaji wa bidhaa kutoka Sh. milioni 200 mwaka 2013/14 hadi kufikia Sh. bilioni 3.1 mwaka 2021. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 1,409.

Dk. Bitanyi alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya wakala huo tangu kuanzishwa kwake.

Alisema, mafanikio mengine ni kutoka kuzalisha chanjo moja ya mdondo mwaka 2013/14 na hadi sasa inazalisha aina saba za chanjo.

"Kiwango cha uzalishaji kimepanda kutoka dozi milioni 21 mwaka 2013/14 na kufikia dozi milioni 65 mwaka 2021/22.

**Kutokana na ongezeko la mapato mwaka hadi mwaka wakala imeendelea kuviimarisha vituo hivi kwa kukarabati majengo na kurahisisha utoaji wa huduma.**

"Matumizi ya chanjo zinazozalishwa na wakala yameonyesha mafanikio makubwa hapa nchini. Mfano, katika Kanda ya Kati hususani mkoa wa Singida na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, imedhibiti ugonjwa wa mdondo wa kuku kwa zaidi ya asilimia 95 kutokana na matumizi makubwa ya chanjo ya mdondo ya matone," alisema.

Pia alisema mafanikio mengine kwa wakala ni kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kuanzisha vituo 11 kutoka vituo viwili vilivyoko katika miji ya Sumbawanga na Meatu, kutoka vituo tisa vilivyokuwapo mwaka 2012/13.

"Vituo hivi vimegawanywa kikanda na vinatoa huduma za uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya mifugo, usambazaji wa chanjo na utoaji elimu juu ya mbinu za kupambana na magonjwa na kuongeza tija katika ufugaji.

"Kutokana na ongezeko la mapato mwaka hadi mwaka wakala imeendelea kuviimarisha vituo hivi kwa kukarabati majengo na kurahisisha utoaji wa huduma," alisema.

Katika kuwasaidia watengenezaji wa vyakula vya mifugo kuzalisha vyakula bora ambavyo vitatoa lishe kamili kwa wanyama, alisema wakala imenunua mashine za kisasa na kuongeza uwezo wa kupima aina na kiwango cha madini kilicho katika vyakula hivyo.

"Maabara inayofanya kazi hii imekarabatiwa na kuwekewa miundombinu muhimu na kuiongezea ufanisi ambapo sasa majibu ya sampuli zinazopimwa hupatikana ndani ya muda mfupi, hivyo kumwezesha mteja kupata majibu ndani ya siku moja baada ya kuwasilisha sampuli yake," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisikiliza maelezo kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya LG Electronics (LG), William Cho, walipokutana jijini Dodoma hivi karibuni. Cho alisisitiza kuwa kampuni hiyo itaendelea kuimarisha shughuli zake za kibiashara katika nchi za Afrika Mashariki, ikiwa ni sehemu ya harakati zake za kukuza mauzo na mapato katika masoko yanayoibukia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafikishwa mahakamani madai ya ufujaji wa mamilioni halmashauri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imewafikisha mahakamani watu 15 kwa madai ya ufujaji fedha za mapato kwa kutumia mashine za POS katika maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema watendaji hao 15, wamefikishwa katika mahakama tofauti ili kujibu mashtaka yanayowakabili.

Alisema hivi sasa taasisi hiyo imebadili mtazamo wa ufuatiliaji wa fedha hizo huku ikiwasisitiza kila mmoja aziwasilishe mara anapokusanya ili kuepuka kuzitumia.

"Sasa hivi tunafuatilia kila mahali kuhakikisha mali ya serikali inakuwa salama ndio maana tunawatembelea kila iitwapo leo," alisema Kibwengo.

Hata hivyo alisema ili kubadili mtazamo wa wana Dodoma ni lazima wote kushiriki kukemea rushwa mitaani.

Alifafanua kuwa hakuna sababu ya watu kufumbia macho suala hilo bali kinachotakiwa ni kila mmoja kupambana ili kuitokomeza rushwa.

Kwa mujibu wa Kibwengo, katika kuchochea mapambano, waliandaa mashindano ya insha mkoani Dodoma kwenye kila wilaya na washindi walikabidhiwa zawadi za fedha kama motisha ya kupambana na rushwa.

Kibwengo alisema wamefanya hivyo ili kutoa hamasa kwa jamii kupambana na rushwa.

Alisema wataendelea kuandaa mashindano kama hayo sehemu mbalimbali lengo ni kuona rushwa inapigwa vita kila mahali na jamii yote na siyo TAKUKURU peke yake.

Kadhalika, alisema wameongeza uandaaji wa mikutano ya hadhara yenye kufundisha na kujenga uelewa dhidi ya mapambano ya rushwa katika mitaa ya mjini na vijijini.

Alisema lengo lao ni kuona wananchi wanapata uwelewa kuhusu kupambana na rushwa katika maeneo wanayoishi.

Pia alisema wataendelea kuzindua klabu za wapinga rushwa ambazo nazo zinasaidia kupambana na rushwa katika maeneo mbalimbali.

# Wapongeza kuhamia soko jipya machinga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

IKIWA ni takribani wiki moja toka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuwaondoa mtaani Machinga na kuwapeleka katika soko la kisasa la wazi, baadhi yao wamemwomba mkuu wa wilaya ya Dodoma kuhakikisha hakuna hata mmoja wao anayebaki mtaani.

Mmoja wa machinga hao, Ramadhan Hussein, akizungumza na Mkuu wa Walaya, Jabiri Shekimweri, alipofanya ziara katika soko hilo, alimwomba kuhakikisha kuwa anasimamia agizo la jiji ili kila mmoja wao aondoke mtaani.

"Tunaomba kila machinga aondoke mtaani ili kuwapo haki kwa kila mtu kutii amri ya jiji ya kuondoka wote mtaani na kuja katika soko hili la kisasa la Machinga Open Market," alisema.

Akizungumza na machinga hao, Shekimweri alisema ameridhishwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa namna ilivyowahamisha kwa kutoa elimu badala ya nguvu.

Alisema hatua ya Jiji la Dodoma la kuwaelimisha machinga hao na kuondoka wenyewe, ni jambo la kupongeza kwa kuwa hakuna nguvu yoyote iliyotumika na kuleta vurugu.

"Nikiwa mkuu wa wilaya ya Dodoma ninawapongeza machinga wenyewe wa jiji la Dodoma kwa hatua ya kuondoka wenyewe kwenye maeneo bila kubughudhiwa ambayo walikuwa wakifanya biashara na kuamua kwenda soko la machinga," alisema.

Pia aliwataka machinga kuhakikisha wanaondoa vibanda vyote ili maeneo hayo yawe wazi na safi badala ya kusubiri kuharibiwa mali zao na mgambo wa jiji.

"Bado kuna maeneo ya mitaa kuna vibanda havijaondolewa niwaombe wahusika waondoe wasisubiri viondolewe na Jiji wakati soko letu la machinga lipo tayari kwa kufanya biashara," alisema.

Shekimweri aliutaka uongozi wa jiji kushirikiana na machinga wa soko hilo kwa kutatua kero mbalimbali zitakazojitokeza na zile zilizoko.

**Hatua ya Jiji la Dodoma la kuwaelimisha machinga hao na kuondoka wenyewe, ni jambo la kupongeza kwa kuwa hakuna nguvu yoyote iliyotumika na kuleta vurugu.**



## Mahakama yatakiwa kusikiliza kesi kujenga imani kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

WATENDAJI wa Mahakama Kisiwani Pemba, wametakiwa kuongeza kasi ya kusikiliza mashauri yanayofikishwa ili kujenga imani kwa wananchi.

Hayo yalisemwa jana visiwani humo na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdalla, wakati alipofanya mazungumzo na watendaji wa Mahakama za Pemba ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kuangalia ufanisi wa utendaji wa taasisi hizo.

Alisema Mahakama Kuu ya Zanzibar ipo katika maboresho makubwa ya kiutendaji ambayo lengo lake ni kuleta ufanisi wa kazi na kuwatumikia wananchi kwa uadilifu.

Aliyataja miongoni mwa maboresho makubwa yaliyofanywa na Mahakama Kuu ya Zanzibar, ni kuongeza kasi ya kusikiliza mashauri mbalimbali yanayofikishwa mahakamani hapo kwa kusajiliwa na kupangiwa mahakimu.

Aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuongeza nafasi za ajira kwa mahakimu wapya pamoja na majaji ili kuongeza ufanisi.

"Hayo ndiyo maboresho makubwa tuliyoyafanya ambayo lengo lake kubwa ni kusikiliza kesi kwa wakati na kutolewa hukumu zake hatua ambayo tunaamini itaongeza ufanisi na kujenga imani kwa wananchi," alisema.

Naye Mrajisi wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Valentina Andrew Katema, alisema wamejipanga vizuri katika utaratibu wa kusikiliza mashauri yanayofikishwa na wananchi na kuwapangia mahakimu watakaosikiliza kesi hizo.

"Tumeanza kuyatekeleza na kuyasimamia maboresho ya mahakama ambapo mashauri yanasajiliwa na kupangiwa mahakimu kwa ajili ya kusikilizwa haraka," alisema.

Kwa upande wake Naibu Msajili wa Mahakama Pemba, Faraji Juma Shomari, alisema kasi ya kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia zinaendelea pamoja na kutolewa hukumu inayostahiki.

Alisema changamoto kubwa bado ni suala la ushahidi kwa wananchi ambao wameshuhudia matukio mbalimbali kutokuwa tayari kutoa mashirikiano kwa mahakama.

# Uzalishaji matango bahari kunufaisha Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, amesema uzalishaji wa matango bahari na uboreshaji wa ukulima wa mwani una manufaa makubwa kwa Zanzibar na nchi za pembezoni za ukanda wa Bahari ya Hindi.

**Nchi za ukanda wa pembezoni kwa Bahari ya Hindi watajifunza mambo mengi ya Zanzibar katika masuala ya uchumi wa buluu.**

Alisema hayo jana wakati akifungua semina ya siku tano kwa nchi za ukanda huo juu ya namna bora ya uzalishaji wa vifaranga vya matango bahari na ukulima bora wa zao la mwani.

Alisema mkutano huo kufanyika Zanzibar ni moja ya mafanikio kwa kuwa wajumbe watapata nafasi ya kujadiliana namna bora ya kuzalisha mazao ya baharini ikiwamo vifaranga vya matango hayo.

Alisema nchi za ukanda wa pembezoni kwa Bahari ya Hindi watajifunza mambo mengi ya Zanzibar katika masuala ya uchumi wa buluu.

Alisema mkutano huo wa wataalamu utafungua milango kuona namna gani Zanzibar ilivyojiandaa kwa uchumi wa buluu na uvuvi.

Naye Mratibu nchi za pembezoni mwa Bahari ya Hindi, Agnes Kayola, alisema nchi hizo zinaushirikiano wa pamoja kujifunza ubora wa uzalishaji wa vifaranga vya matango bahari na ukulima bora kilimo chenye faida kwa nchi wanachama.

Alisema mkutano huo utakuwa na tija kubwa kwa wanachama waliotoka nje ya Tanzania kwa kuwa watapata muda wa kuangalia jinsi ya wananchi walivyofanikiwa kilimo cha mwani.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Aboud Suleiman Jumbe, alisema mkutano huo kufanyika Zanzibar unatoa fursa ya kuboresha uzalishaji mzuri wa vifaranga vya matango bahari na namna bora ya kulima kilimo cha mwani.

Alisema Zanzibar imejipanga kuhakikisha mazao ya bahari kuwa moja ya kuzalisha uchumi wake, kwa sasa zao la mwani ni tofauti na lilivyokuwa awali.

Alisema Idara ya Uvuvi inafanya kazi kubwa ya kuwaelimisha wananchi namna ya kulima mwani na uboreshaji wa uzalishaji wa vifaranga vya matango bahari.




Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, akizungumza wakati akifungua semina ya siku tano kuhusu namna bora ya uzalishaji wa vifaranga vya matango bahari na ukulima bora wa zao la mwani, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mecco yatakiwa kuongeza kasi ujenzi barabara Chake Chake

**Na Mwandishi wetu**

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi Nishati, Ardhi na Mawasiliano imeutaka uongozi wa kampuni ya ujenzi ya Mecco inayojenga barabara ya Chake Chake hadi Wete kuongeza kasi ili ikamilike kwa wakati na kutumika kutoa huduma za usafiri.

Hayo yalisemwa jana kisiwani Pemba na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Yahya Rashid Abdalla, akiwa na wajumbe wa kamati hiyo walipofanya ziara ya kuangalia ujenzi ambao umeanza kwa kusuasua.

Alisema barabara ya Wete hadi Chake yenye urefu wa kilomita 22.2 ni muhimu kutokana na kuunganisha mikoa miwili ya kisiwa cha Pemba katika miundombinu ya barabara.

Aidha, alisema ujenzi wa barabara hiyo unakwenda sambamba na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya kuona kisiwa cha Pemba kinaunganishwa na miundombinu ya barabara ikiwa ni sehemu ya juhudi za kukifungua katika uwekezaji na sekta ya utalii.

"Kamati yangu ya Baraza la Wawakilishi haijaridhishwa hata kidogo na ujenzi wa barabara ya Chake Chake hadi Wete ambayo ni sehemu ya kimkakati yenye lengo la kuiunganisha mikoa mwili ya Pemba na uwekezaji," alisema.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Rajab Ali, alisema ujenzi wa barabara hiyo uliokwama kwa muda mrefu ni miongoni mwa vipaumbelele vya wizara hiyo kuona kisiwa cha Pemba kinafunguka na miundombinu yake ili kurahisisha shughuli za mawasiliano na uchukuzi.

Alikiri kuwapo kwa changamoto za kuchelewa kuanza kwa mradi wa ujenzi wa barabara hizo ikiwamo kampuni kudai kuchelewa kuwasili kwa vifaa vyake kamili kwa shughuli za matengenezo ya barabara.

Aidha, alisema kwa sasa wanashughulikia suala la kulipa fidia kwa wananchi ambao wamepisha ujenzi wa barabara na baadhi ya mali zao ikiwamo nyumba kuathirika kwa ajili ya ujenzi huo.

"Kwa upande wa wizara tupo katika hatua za mwisho za kukamilisha utaratibu wa kulipa fidia wananchi wote ambao wanastahili kulipwa ikiwamo waliopisha ujenzi wa barabara na hivyo mali zao kuathirika," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo, waliitaka wizara na mkandarasi kukaa pamoja kuzipatia ufumbuzi changamoto zote na kuona ujenzi wa barabara hiyo unafanyika na kukamilika kwa wakati.

"Wananchi wanachotaka kuona ujenzi wa barabara hii unafanyika na kukamilika kwa wakati, kwa hivyo changamoto zote zilizopo zinatakiwa kukamilishwa kwa wakati," alisema Suleiman Makame Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Mkoa wa Kusini Pemba.





# Kikongwe akutwa amefariki dunia ndani nyumbani kwake

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KIKONGWE aliyefahamika kwa jina la Lucia Masanja (78) mkazi wa Kijiji cha Nduguti Kata ya Nyida wilayani Shinyanga, amekutwa ndani kwake amefariki dunia na mwili wake ukiwa tayari umeharibika huku chanzo cha kifo chake kikiwa bado hakijafahamika.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii juzi, Mwenyekiti wa Kijiji cha Nduguti, Saleh Manota, alisema tukio hilo lilitokea Novemba 3 mwaka huu huku taarifa za kifo hicho akieleza kuzipata kwa wananchi na majirani zake.

**Tumemkuta bibi huyu Lucia Masanja nyumbani kwake akiwa amefariki dunia na ameoza kabisa.**

Alisema alipofika eneo la tukio hali ile, ikabidi wapige simu polisi nyumbani kwa bibi huyo baada ya kupokea taarifa za kifo chake alikuta kuna harufu kali huku mlango ukiwa umefungwa kwa ndani.

Manota alisema baada ya kuona hali ile, ikabidi wapige simu polisi na walipofika askari ndipo ikabidi wavunje mlango na kumkuta bibi huyo akiwa ameshafariki dunia siku nyingi na mwili wake ukitoa harufu kali huku ukiwa umeshaoza.

"Tumemkuta bibi huyu Lucia Masanja nyumbani kwake akiwa amefariki dunia na ameoza kabisa. Inaonekana alifariki dunia siku nyingi na wananchi wamemgundua mara baada ya kusikia harufu kali ikitoka ndani ya nyumba yake," alisema Manota.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa Jeshi la Polisi bado linaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha kifo hicho.



Mwenyekiti wa Manispaa ya Kahama, Yahaya Bundala (kushoto), akikabidhi viuatilifu vya mazao kwa mkulima, Matha Mwandiki kutoka Kata ya Mwendakulima, wakati wa ugawaji wa pembejeo za kilimo bure zenye thamani ya Sh. milioni 66.8 kwa wakulima vijana 71 kutoka kata 12 kwenye viwanja vya manispaa hiyo, jana. Katikati ni Katibu wa Mbunge wa Kahama, Abdull Mpei. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Madiwani waituhumu Manispaa Kahama kujimilikisha majengo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wanaituhumu Manispaa ya Kahama kujimilikisha majengo yao bila ridhaa yao hali ambayo imesababisha baraza hilo kupitisha maadhimio na kuweka mkakati wa kuyarejesha mara moja.

Majengo hayo ni waliyoyatumia awali kabla ya kuhamia katika mapya ya makao makuu katika Kata ya Ntombo nje ya mji na mpaka sasa yanatumika kama soko kuu la madini ya dhahabu Kahama na kuwapatia fursa wachimbaji wadogo kuuza madini yao.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mibako Mabubu, aliyabainisha hayo jana katika kikao cha kwanza cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 na kusema kuwa majengo hayo ni mali ya halmashauri yao na waliondoka kutekeleza agizo la serikali kuhamia makao makuu yao mapya.

Alisema, watakapokabidhiwa majengo hayo hawatazikodisha taasisi za serikali zilizoko kwa sasa ikiwamo Jeshi la Zimamoto, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na TAMESA isipokuwa za binafsi zitalazimika kuondoka na majengo kurudi halmashauri kuyatafutia matumizi mengine.

Mabubu alidai, wapangaji wanalipa kodi katika Manispaa ya Kahama wakati mwenye mamlaka ya kukusanya kodi ni Halmashauri ya Msalala ambayo ndiyo mmiliki halali wa majengo hayo na wangeweza kuyafanya kama sehemu ya chanzo cha mapato yao.

"Sisi tuliandikiwa barua na Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga tukitakiwa tuondoke twende makao makuu yetu na tuliondoka bila kukabidhi hayo majengo ingawa barua ilisema mali zote zilizoko zitakuwa mali za halmashauri inayobaki ambayo ni Kahama hali ambayo sisi tulipingana nayo na ndiyo maana tuliondoka bila kukabidhi," alisema Mabubu.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Leonard Mabula alisema, tayari ofisi ya Rais TAMISEMI ilishaunda tume ya kuchunguza na ilishafanya kazi ya ugawanaji wa mali hizo yakiwamo majengo hayo, lakini haijatoa majibu ya kurejeshwa na kuwasihi kusubiri majibu ya tume.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, alisema upo waraka wa kutoka ofisi ya Waziri wa TAMISEMI ambao umekabidhi majengo hayo kwa halmashauri yake na hana namna nyingine ya kuzungumza nje ya waraka huo.

Halmashauri ya Msalala ilianzishwa mwaka 2013 ikigawana mali na Halmashauri ya Ushetu ambayo Ushetu ndiyo ilitangulia kugawana mali mwaka 2012 na iliyokuwa Halmashauri ya Mji wa Kahama kabla ya kupandishwa hadhi na kuwa manispaa.

# Watuhumiwa mauaji wanaswa na silaha

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

JESHI la Polisi Mkoa wa Geita limekamata silaha moja ya kivita aina ya AK 47 na watuhumiwa wanne, mmoja akiwa raia wa Burundi anayedaiwa kuingia na silaha hiyo nchini.

Silaha hiyo inadaiwa kutumiwa kumtishia mfanyabiashara Tegemeo Rashidi (38) mkazi wa kijiji cha Ihanga kata ya Buziku Wilayani Chato Mkoani hapa kabla ya kuuawa kwake kwa kukatwa na panga na watu wanaodhaniwa kuwa ni majambazi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, kamishna msaidizi (ACP) Safia Jongo, akizungumza na waandishi wa habari juzi, alisema mfanyabiashara huyo aliuawa kwa kukatwa panga sehemu mbalimbali za mwili baada ya kumfunga kwenye pikipiki aliyokuwa akiendesha.

Kamanda huyo alisema kuwa baada ya kupata taarifa ya mauaji ya mfanyabiashara huyo walianza msako mkali na kufanikiwa kuikamata silaha hiyo ambayo ilikuwa imefichwa kwenye shamba la mahindi .

Jongo aliongeza kuwa katika tukio hilo, jeshi linawashikilia watuhumiwa wanne, mmoja akiwa raia wa Burundi anaedaiwa kuingia na silaha hiyo nchini.

Katika hatua nyingine, Kamanda Jongo alisema katika kipindi cha Septemba Mosi hadi Oktoba 31, mwaka huu, katika usalimishaji silaha, mkoa wa Geita umepokea silaha zilizosalimishwa yakiwamo magobole 18 yaliyosalimishwa kwa hiari.

Vilevile magobole 16 na wamiliki wake walikamatwa baada ya kushindwa kusalimisha kwa hiari kwa kipindi kilicho kuwa kimetolewa na jeshi la polisi nchini.

Pia jeshi hilo limekamata magunia saba ya dawa za kulevya aina ya bangi katika operesheni iliyofanyika ndani ya kipindi kifupi pamoja na vitu mbalimbali vikiwamo redio, televisheni, simu, baiskeli, pikipiki, jiko la gesi la kupikia na nguo.

Aidha, jeshi la polisi linaendelea kutoa wito kwa wananchi kushirikiana na majeshi ya ulinzi na usalama ili kufichua vitendo vya uhalifu vinavyofanyika kwenye maeneo yao.

**Vilevile magobole 16 na wamiliki wake walikamatwa baada ya kushindwa kusalimisha kwa hiari kwa kipindi kilicho kuwa kimetolewa na jeshi la polisi nchini.**

HABARI KIMATAIFA

# Wanajeshi wapya 3,000 waanza mafunzo DRC

**KINSHASA, DRC**

ZAIDI ya wanajeshi wapya 3,000 wameanza mafunzo mwanzoni mwa wiki hii huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) huku jeshi la nchi hiyo likiimarisha mapambano dhidi ya waasi wa M23.

Serikali ya Rwanda, ambayo imekanusha mara kwa mara kuunga mkono kundi la M23, ilisema kuwa ndege ya kivita ya Congo imekiuka anga ya Rwanda kwa kutua kwa muda katika uwanja wa ndege wa Rubavu, huku Congo ikisema kwamba ndege hiyo iliyokuwa haina silaha ilitua kwa bahati mbaya katika anga ya Rwanda.

Waasi wa M23 walipata umaarufu zaidi ya muongo mmoja uliopita walipouteka mji mkubwa wa Goma uliopo mashariki mwa Congo ambao uko kwenye mpaka na Rwanda.

Pia ilielezwa kuwa baada ya makubaliano ya amani, wapiganaji wengi wa M23 walijumuishwa katika jeshi la kitaifa, lakini mwaka mmoja uliopita, kundi hilo liliibuka tena, likisema serikali imeshindwa kutimiza ahadi zake za muongo mzima.

Mvutano utatajwa kuongezeka huku waasi wa M23 wakisonga mbele katika wiki za hivi karibuni na kuteka miji kadhaa muhimu ikiwa ni pamoja na Kiwanja, kitendo ambacho serikali ya Congo imeilaumu Rwanda na kumfukuza balozi wa Rwanda takriban wiki moja iliyopita.

**VOA**

# Viongozi EAC wajadili hali ya usalama DRC

**SHARM EL SHEIKH, Misri**

VIONGOZI wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakiwamo Rais wa Tanzania, Burundi, Kenya na Rwanda pamoja na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wamekutana kando na mkutano wa COP 27 unaofanyika Sharm El Sheikh nchini Misri, kujadili hali ya usalama mashariki mwa DRC.

Mazungumzo hayo yaliyoongozwa na Mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, yanakuja baada ya mazungumzo yake na mpatanishi katika mchakato wa mazungumzo ya amani ya mashariki mwa Congo, Rais wa zamani wa Kenya Uhuru Kenyatta, yaliyofanyika mjini Bujumbura wiki iliyopita.

Hayo yanajiri huku hali ya wasiwasi ikiendelea kutawala baina ya DRC na Rwanda kila upande ukimshutumu mwenzake kuwaunga mkono wapinzani wake.

DRC inaishutumu Rwanda kuwaunga mkono waasi wa M23 walioteka hivi karibuni baadhi ya maeneo ya mashariki mwa Congo, huku Rwanda ikiishutumu DRC kwa kuunga mkono kundi la wapiganaji wa Kinyarwanda wa FDLR wanaoshutumiwa kufanya mashambulio kwenye maeneo yaliyo karibu na mpaka ndani ya Rwanda.

Aidha, inaelezwa kuwa kila upande unakanusha madai hayo.

Mwanzoni mwa wiki hii Rwanda iliishutumu DRC kwa kuingiza ndege yake ya kijeshi Rwanda na kulaani kitendo hicho ambacho walikichukulia kama cha uchokozi. Ambapo DRC ilikiri kuingiza ndege hiyo, lakini ikasema kuwa haikuwa na nia mbaya.

Burundi, Uganda na Kenya zimeyapeleka majeshi yake mashariki mwa Congo kukabiliana na makundi ambayo yamekuwa yakiyumbisha usalama katika eneo hilo kwa karibu miongo mitatu.

***BBC***



Jeshi la DRC likiwa katika doria eneo ambalo waliwatimua waasi wa M23 katika operesheni maalum. **PICHA: VOA**

# Mataifa kame yaungana kukabili uhaba wa maji

**SHARM EL SHEIKH, Misri**

MATAIFA yaliokumbwa na ukame, yakiongozwa na Senegal na Uhispania, yametangaza muungano kusaidiana kudhibiti uhaba wa maji kwa kubadilishana teknolojia na utaalamu.

Tangazo hilo lilitolewa jana pembeni ya mkutano wa mazingira wa Umoja wa Mataifa (UN) COP27, unaofanyika nchini Misri, baada ya kukosekana mvua kwa msimu wa tano mfululizo katika kanda ya pembe ya Afrika.

Akihutubia wawakilishi wa muungano huo, Gavana wa Kaunti ya Embu nchini Kenya Cecily Mbarire, alisema nchi yake inashuhudia ukame mbaya zaidi katika kipindi cha miaka 40.

Watabiri wa hali ya hewa wameonya juu ya uwezekano wa msimu usiokifani wa sita wa kukosekana kwa mvua mwaka ujao.

"Tumekuwa na misimu minne mfululizo bila mvua na kuna matarajio makubwa ya msimu wa sasa mfupi wa mvua kuwa wa tano," alisema na kuongeza:

"Kimsingi tunashuhudia ukame mbaya zaidi katika miaka 40 kama taifa." Alisema Mbarire.

Waziri Mkuu wa Uhispania, Pedro Sanchez, alisema ukame umekuwa na madhara yasiokifani, wakati wa uzinduzi wa muungano huo ambapo nchi yake inapanga kuchangia kiasi cha dola milioni tano katika mwaka wa kwanza.

Sanchez alisema mwaka huu Ulaya imeshuhudia ukame mbaya zaidi katika kipindi cha miaka 500, na Afrika na kanda nyingine za dunia zinakumbwa pia na uhaba mkali wa maji.

**UKAME WAONGEZEKA ASILIMIA 29**

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa lenye dhamana ya kuzuwia kuenea kwa jangwa (UNCCD), ukame umezidi kuikumba dunia kwa asilimia 29 tangu mwaka 2000, wakati ambapo joto likichochea ukataji misitu na usimamizi duni wa ardhi katika kukausha maeneo yaliokuwa na hali ya wastani.

Naibu Katibu Mtendaji wa UNCCD, Andrea Meza, alisema maandalizi zaidi yanahitajika kwa ajili ya ukame ujao.

"Tunachojua na inachotuambia sayansi ni kwamba tutakuwa na matukio zaidi ya ukame, makubwa na ya kujirudia na tunahitaji kujiandaa," alisema Meza.

Aliongeza kuwa dunia inahitaji kubadilisha mtazamo wake, huku akisisitiza kwamba wanahitaji kujiandaa kwa ajili ya ukame ujao.

Aidha, alieleza kuwa wanasayansi wanasema ukame utakuwa mbaya zaidi na wa kujirudia katika miaka ijayo, na pia utadumu muda mrefu zaidi pale ambapo joto la dunia likivuruga mienendo ya hali ya hewa.

**DOLA TRILIONI 5 ZAKADIRIWA**

Ripoti iliyotolewa mwezi Agosti na Shirika la Ushauri wa Uhandisi wa Kimazingira (GDH), ilionyesha kuwa kufikia mwaka 2050, usumbufu wa hali ya hewa, ikiwamo ukame pamoja na upepo mkubwa na mvua, huenda vikaugharimu uchumi wa dunia dola trilioni 5.6.

Katibu Meza, alisema hakuna nchi ina kinga dhidi ya ukame na watu walioathirika vibaya zaidi hawawezi kuzalisha chakula, umeme au kufanya biashara wakati mito ikikauka na kuzuwia usafirishaji.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu wa Uhispania, Sanchez, muungano huo unaoshirikisha mataifa 25 na mashirika yapatayo 20, utalenga kuhamasisha rasilimali kupambana na ukame pale utakapojitokeza, lakini hakutoa ufafanuzi kuhusu kiasi gani cha pesa kinaweza kutengwa.

***DW***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**DAVID F. KAPONGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0180-0007** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. FRANCIS DESALES SEMINARY October 2009.** Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0147-0575** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **PUGU SEKONDARI February 2012.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **DAR/URA/RB/434295/2022** na **DAR/URA/RB/434301/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WALID KHALID MERREY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA OPA** yenye usajili namba **T514 DDW.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/435856/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAHARI COSMETICS LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 377 BYA – TOYOTA NOAH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PWA/MLA/RB/371983/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIGIUS PAUL SARUNI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 615 DEV – TOYOTA PROBOX.** Chassis namba **NCP580044528.** Engine namba **1NZB824598.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MSI/RB/428848/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUHINA ALLY SAID** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 776 DUV – TOYOTA COROLLA SPACIO.** Chassis namba **NZE1213220741.** Engine namba **1NZA905928.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/KIJ/RB/428084/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**IBRAHIM ASHIRAF MRINDOKO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S0119/0051** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KIBAHA SECONDARY SCHOOL mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHA/RB/434813/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JELLE KRAMER MAXIMILLIAN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari ya **JELLE KRAMER** yenye NAMBA za usajili **T 621 CGG** chassis namba **HDJ810006144,** Engine namba **IHD0013128.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi **ARU/ARU/RB/424690/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JELLE KRAMER MAXIMILLIAN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari ya **OFF THE MAP SAFARIS LIMITED** yenye NAMBA za usajili **T 681 DXU,** Engine no **2AZ1991790,** Chassis namba **ANH100128506.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. **ARU/ARU/RB /388998/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NSUKIGWE M. MWASONYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CORONA** yenye usajili namba **T 930 CGJ,** chassis namba: **AT2110028412** na Engine namba: **7afe2369854.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI CONTROLL NUMBER: **9910834538959**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAMANI INVESTMENT LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina **RAV 4** yenye usajili namba **T633 DEL ,** CHASSIS namba **SXA110184235** na ENGINE namba: **3S2467727.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/435362/2022**

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

**PAUL KUNDAEL NDOSA** anatangaza kupotea kwa hati ya kiwanja yenye namba **43480/Plot namba 991 block J** kilichopo Njiro atakaeiona atoe taarifa kituo Cha polisi kwa namba **ARU/ARU/RB/435568/2022.**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## BURUDANI

# DAVIDO

## AFUTA INSTAGRAM YA MWANAWE




**LAGOS, Nigeria**

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Davido na mpenzi wake, Chioma wamefuta rasmi akaunti ya Instagram waliyomfungulia mtoto wao wa kike, Ifeanyi, mwenye umri wa miaka mitatu ambaye alifariki dunia wiki iliyopita.

Familia hiyo ilimfungulia akaunti ya Instagram mtoto wao huyo ambayo ilikuwa imekua kwa kasi, kwani hadi kifo chake tayari ilikuwa na wafuasi zaidi ya 50,000.

Baada ya kifo chake, wapenzi hao kwa uchungu mwingi wamelazimika kuifuta akaunti hiyo na kufuta picha zake zote, kama moja ya njia ya kujaribu kudhibiti jinsi watu wanasambaza picha za marehemu kijana wao, na pia kujaribu kupata faraja.


Ikumbukwe akaunti hiyo ilifunguliwa mapema mwezi uliopita wakati wakisherehekea kufikisha kwake umri wa miaka mitatu.

Maelezo yanaonyesha kuwa Davido na Chioma walikuwa katika Jimbo la Ibadan kwa ajili ya shoo wakati ajali hiyo ikitokea.

# AMBER LULU AKARIBIA KUFUNGA NDOA

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa kike wa muziki wa Bongo Fleva, Amber Lulu, ametangaza kwamba, anakaribia kufunga ndoa.



Amber Lulu ambaye ni mama wa mtoto mmoja aliyezaa na rapa, Emba Botion, ametangaza hatua hiyo baada ya kudaiwa kuwa kwenye uhusiano wa kimapenzi na mtu mpya.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, Lulu aliandika kuwa, ataolewa hivi karibuni na kwamba halikuwa jambo ambalo alidhani litatokea.

"Naolewa. Asante Mungu, sijatarajia hili," aliandika Amber Lulu anayetamba na ngoma yake ya Halichachi.

Hivi karibuni alidaiwa kuwa kwenye uhusiano mpya wa kimapenzi.

Hii ni baada ya kuposti picha ya kimahaba akiwa na msanii wa Bongo Fleva aitwaye The Dream na kunogesha tetesi za kuwa kwa sasa moyo wake umetulia kwa msanii huyo.

Kabla ya hayo, Lulu alikuwa ameposti picha yake na kudokeza kwamba alikuwa amepata mpenzi anayempenda mwanawe, Ariana.

Lulu alisema kuwa, kabla ya hapo alikuwa akipitia ukatili kutoka kwa baba wa mtoto wake licha ya kumuonyesha mapenzi.

"Kwako nimepumzika, nimechoka vipigo, dharau, napenda, unavyotupenda mimi na mwanangu Arina, tunakupenda sanaa."

# VANILLAH AZUNGUMZIA KUTUA KINGS MUSIC

**Na Mwandishi Wetu**



KWA mara ya kwanza baada ya kutambulishwa wiki iliyopita kama msanii mpya wa lebo kubwa ya muziki nchini Tanzania ya Kings Music Records, ambayo ipo chini ya Ali Kiba, Vanillah amezungumza alikopitia.

Vanillah amezungumza mengi sana kuhusu muziki wake namna alivyokutana na Kiba na muda aliokaa kabla ya kutambulishwa.

Ameeleza mambo mengi aliyoambiwa na bosi wake kabla ya kutambulishwa rasmi na namna atakavyokabiliana na changamoto hizo.

Ameongeza kuwa ukifika kwa Kiba unachoambiwa cha kwanza ni kufanya muziki mzuri halafu mambo ya mikataba yanakuja baadaye.

## HABARI MICHEZO

# REFA ALIYEIPA YANGA PENALTI MATATANI, CHAMA, AZIZ KI...

**Na Adam Fungamwango**

VIUNGO washambuliaji wa klabu za Simba na Yanga, Clatous Chama na Stephane Aziz Ki, wamefungiwa kucheza soka mechi tatu na kutozwa faini ya Sh. 500,000 kila mmoja kwa kosa la kukwepa kusalimiana na wachezaji wenzao pinzani kabla ya kuanza kwa mechi kati ya timu hizo mbili zilipokutana Oktoba 23, mwaka huu, zikitoka sare ya bao 1-1.

Pamoja na hilo, Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), pia imempeleka mwamuzi Florentina Zablon, kwenye Kamati ya Waamuzi ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa kosa la kushindwa kutafsiri sheria 17 za mpira wa miguu kwenye mechi namba 74 iliyochezwa kati ya Geita Gold na Yanga iliyochezwa Oktoba 26, mwaka huu katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Adhabu hizo na zingine, zimetolewa na kamati hiyo kwenye kikao chake cha Novemba 4, mwaka huu kupitia mwenendo na matukio mbalimbali ya Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Ligi ya Championship.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, ilisema kuwa Chama na Azik Ki, kwa nyakati na mazingira tofauti, walionekana kufanya hila kwa kusubiri nje ya uwanja hadi zoezi la kusalimiana lilipokamilika ndipo walipoingia uwanjani.

Kutokana na adhabu hiyo, Chama atau-kosa mchezo wa leo timu yake ikicheza dhidi ya Singida Big Stars, lakini pia atau-kosa mchezo wa Novemba 12, Simba itakaposhuka uwanjani dhidi ya Ihefu na ule wa Novemba 16 dhidi ya Namungo.

Aziz Ki hatokuwapo kwenye mechi ambayo Yanga itacheza dhidi ya Singida Big Stars Novemba 17, dhidi ya Dodoma Jiji, Novemba 22 na mechi ya mwisho ni ile ambayo timu yake itashuka dimbani dhidi ya Mbeya City Novemba 26, mwaka huu.

Kamati hiyo pia imemkuta Florentina na makosa ya kushindwa kutafsiri vema sheria 17 za soka. Imesema Kamati ya Waamuzi ya TFF italitazama kitaalamu tukio la pigo la penalti ya Yanga dhidi ya Geita Gold kwenye dakika ya 18 ya mchezo kwenye mechi hiyo kabla ya kurejea na kuishauri tena kamati hiyo nini cha kufanya.

Pia kamati hiyo imeitoza Yanga faini Sh. milioni tano kwa kuingia kwenye mlango usio rasmi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikicheza dhidi ya Simba huku mashabiki na wanachama wa klabu hiyo, Israel Suma, Kaisi Mwasongwe na Mohamed Mposo, wakifungiwa miezi mitatu kuingia uwanjani, baada ya kuwavamia waamuzi kwenye mechi hiyo ya watani wa jadi wakati wa mapumziko.

# Mpole atoweka Geita Gold

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA George Mpole anadaiwa kutoweka kwenye kambi ya timu ya Geita Gold na hajulikani alipo mpaka sasa huku uongozi ukitoa rai kumtaka arejee atakapopata taarifa hizi.

Mwenyekiti wa Klabu ya Geita Gold, Leonard Bugomola, amesema jana kuwa straika huyo ambaye ni mfungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, alitoweka baada ya mechi yao dhidi ya Coastal Union iliyochezwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Oktoba 13, mwaka huu na kumalizika kwa matokeo ya suluhu.

Hata hivyo, taarifa zimekuwa zikidai kuwa mchezaji huyo anadai mshahara wake wa tangu Septemba, lakini pia baadhi ya pesa za usajili ambazo hajamaliziwa. Mwenyekiti wa Geita Gold amepinga madai hayo na kusema kuwa mchezaji huyo hadai chochote, huku wakiwa hawajui sababu za msingi zilizosababisha kufanya kitendo hicho.

"Mwambieni aje kazini, hayupo Geita Gold sababu hatujui, baada ya mchezo wetu dhidi ya Coastal hajaonekana kambini, si kweli kwamba anadai, hadai chochote si pesa ya usajili au mshahara, mwambieni aje kupambania namba na wenzake, kuwa mfungaji bora mwaka jana hakumfanyi kushindwa kupambania nafasi ya kucheza uwanjani, hakumfanyi kushindwa kutimiza majukumu yake kwenye timu, aje afanye majukumu yake kulingana na jinsi alivyosaini mkataba wake, pia itamsaidia kulinda kipaji chake," alisema mwenyekiti huyo.

Alisema licha ya kutumia njia ya kutangaza kwenye vyombo vya habari ili arejee, lakini pia wamemuandikia barua ya kumkumbusha kuwa yeye ni mwajiriwa wa klabu hiyo, hivyo anahitajika muda huu awe kazini.

"Nakumbuka wakati wa maandalizi ya msimu huu hakuwapo, alikuja siku mbili kabla ya kucheza dhidi ya Simba, walimu wakamheshimu wakampa nafasi, leo hii hayupo tena, tunamuomba tu arudi, haiwezekani kuwa unapangwa wakati hufanyi mazoezi," alisema Bugomola.

Msimu uliopita alipachika mabao 17 na kutwaa Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu Bara akimshinda straika wa Yanga, Fiston Mayele kwa bao moja zaidi, na alianza kuingia kwenye rada za Klabu za Simba, Yanga na Azam FC, lakini dakika za mwisho akabaki na timu hiyo.

**MAZOEZI...**



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini kujiandaa na mechji ya Ligi Kuu dhidi ya Singida Big Stars itakayopigwa leo katika Uwanja wa Liti mkoani Singida. **PICHA: SIMBA**

# Azam, Dodoma Jiji kuwasha moto leo

**Na Saada Akida**

POINTI tatu ni kauli inayotolewa na makocha wawili, kocha wa Azam na Dodoma jiji FC kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa leo katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Azam FC wanashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 katika mechi ya mwisho waliyocheza dhidi ya Ihefu FC, uwanjani hapo.

Kwa upande wa Dodoma Jiji FC, wanacheza mchezo huo baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania, mchezo uliochezwa katika Dimba la Shekha Amri Abeid jijini Arusha.

Timu hizo mbili zinashuka dimbani zikijivunia kufanya maandalizi mazuri na kila mmoja kuhitaji alama tatu muhimu.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Azam FC, Aggrey Morris, alisema wamejipanga zaidi ili kufanikisha malengo yao ya kutafuta pointi tatu muhimu.

"Tumejiandaa vizuri na tutawakosa baadhi ya wachezaji akiwamo Price Dube, Kipre Junior na Selemani Sopu, lakini waliobaki wako tayari kwa ajili ya kupata pointi tatu muhimu," alisema Aggrey.

Nahodha wa Azam FC, Bruce Kangwa, alisema wamejipanga vizuri katika mchezo wa leo kwa ajili ya kuvuna pointi hizo tatu.

"Mechi ni ngumu kwa sababu ya matokeo ya nyuma ya wapinzani wetu, lakini kwa sababu tunahitaji kupata pointi muhimu ili kufikia malengo yetu, kukosekana kwa Dube hakutaathiri mipango kwa kuwa tuna kikosi bora na kuna mtu anaweza kucheza nafasi yake," alisema Kangwa.

Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji FC, Kassim Liogope, alisema maandalizi yako vizuri na wamefanyia kazi baadhi ya mapungufu ya kikosi chao.

Alisema pointi tatu ni sehemu ya mipango yao na wanaenda kwenye mchezo huo wa leo kwa tahadhari kubwa kwa kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu kulingana na ubora wa wapinzani wao.

"Tumefanya maandalizi mazuri , mechi iliyopita tulipata pointi moja na tunaendelea tulipoishia na ninaimani kubwa ya mchezo wa kesho (leo), tutapata ushindi," alisema Liogope.

Alisema kila mechi imekuwa na mipango yake na sasa wanaenda kucheza dhidi ya Azam FC tofauti na walivyoingia katika mchezo uliopita.

Nahodha wa Dodoma Jiji FC, Mbwana Kibacha, alisema: "Kazi ya benchi la ufundi imemalizika na jukumu kubwa liko kwetu wachezaji kupata matokeo ya pointi tatu katika mchezo huu wa kesho (leo), ambao utategemea mbinu na ufundi wa makocha wa timu zote mbili," alisema Kibacha.

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM KUTUA LIVERPOOL

WAMILIKI wa Liverpool, Fenway Sports Group watamsajili kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19, kutoka Borussia Dortmund kwa ada ya pauni milioni 87 kama zawadi ya kuagana na klabu hiyo baada ya kutangaza kuiuza. ***(Marca, via FourFourTwo)***

### UNITED NAO WAJITOSA

KLABU ya Manchester United ni miongoni mwa klabu zinazowania kuinasa saini ya Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, huku Chelsea ikiwa si miongoni mwa timu anazotaka kujiunga nazo. ***(TeamTalk)***

### RATCLIFFE KUINUNUA LIVERPOOL

BILIONEA wa England, Sir Jim Ratcliffe, ni miongoni mwa watu wanaoweza kuinunua Liverpool. ***(Liverpool Echo)***

### JONES KUINOA SOUTHAMPTON

KOCHA wa Luton Town, Nathan Jones, anatarajiwa kuwa kocha mpya wa Klabu ya Southampton baada ya Jumatatu kumfuta kazi Ralph Hasenhuttl. ***(Mirror)***

### EPL WALIMFUATILIA GAKPO

ZAIDI ya nusu ya wawakilishi wa Klabu za Ligi Kuu England, walifuatilia mchezo wa Ajax dhidi ya PSV Eindhoven Jumapili, huku winga wa PSV wa Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23, akiwa miongoni mwa wachezaji waliocheza. ***(90Min)***

### FSG FAIDA KUBWA LIVER

FSG watapata faida kubwa katika uwekezaji wao, lakini thamani ya Liverpool iko chini ya bei ambayo Roman Abramovich aliiuza Chelsea mapema mwaka huu. ***(Star)***

### FRANK NAYE ATAKIWA

KLABU ya Southampton inavutiwa na bosi wa Brentford, Thomas Frank na pia walimjadili kocha wa River Plate, Marcelo Gallardo. ***(Guardian)***

### LEAO HUYOOO CHELSEA

MATUMAINI ya Chelsea kumsajili mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao, mwenye umri wa miaka 23, yameongezeka kwa sababu ya matatizo yanayoendelea katika mazungumzo ya kuongeza mkataba wa mchezaji huyo. ***(Sky Italy, via Mirror)***

### DAVID ATAKIWA SPURS

KLABU ya Arsenal na Tottenham Hotspur zinafikiria kumnunua mshambuliaji wa Lille raia wa Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 22. ***(GiveMeSport, via TeamTalk)***

### ARSENAL KUTUMIA FEDHA

VINARA wa Ligi ya England, Arsenal wako tayari kutumia fedha katika dirisha la uhamisho la Januari ili kuendeleza changamoto yao ya kuusaka ubingwa msimu huu. ***(90Min)***

### CHOUPO-MOTING KUBAKI

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich na Cameroon, Eric Maxim Choupo-Moting Januari, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, anataka kusalia katika klabu hiyo ya Bundesliga. ***(Florian Plettenberg)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ALVES NDANI KIKOSI CHA BRAZIL KOMBE LA DUNIA

**Jesus na Martinelli wote kutoka Arsenal nao wajumuishwa huku Antony wa United naye...**

**SAO Paulo, Brazil**

DANI Alves atakuwa nyota mwenye umri mkubwa zaidi wa Brazil katika Kombe la Dunia baada ya kujumuishwa kwenye kikosi kinachokwenda Qatar, huku Roberto Firmino akitemwa.

Kocha wa Brazil, Tite ametangaza kikosi chake cha mwisho, akimjumuisha Gabriel Martinelli wa Arsenal.

Alves hivi sasa ana umri wa miaka 39 na alicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa mwaka 2006, lakini anaelekea Kombe lake la tatu la Dunia mwaka huu.

Beki huyo wa zamani wa kulia wa Barcelona ataweka historia kwa Selecao hao, huku Djalma Santos mwenye umri wa miaka 37, kwenye Kombe la Dunia la 1966 - hapo awali alikuwa mchezaji wao mwenye umri mkubwa zaidi kucheza michuano hiyo.

Wengi wamekosoa kujumuishwa kwa Alves, lakini Tite aliwajibu wakosoaji wake kuhusu mkongwe huyo.

"Sikuja hapa ili kuwafurahisha watu kwenye Twitter, ambayo hata sijui ni asilimia ngapi ya watu wa Brazili wanawakilishwa," alisema kocha huyo.

"Naheshimu maoni tofauti na siko hapa kumshawishi kila mtu, nataka tu kutoa habari ili watu watoe maoni yao kidemokrasia.

"Sasa, kila mtu ana maoni yake na kila mtu ana heshima yangu."

Kujumuishwa kwa Alves zilikuwa habari kubwa kwa tangazo la kikosi cha Tite Jumatatu.

Wachezaji wawili wa Arsenal, Martinelli na Gabriel Jesus wote wamejumuishwa, lakini Firmino wa Liverpool ametemwa.

Firmino hatarejea baada ya kutajwa katika kikosi cha Brazil kwenye Kombe la Dunia 2018 nchini Urusi, ingawa wachezaji wengine tisa aliokuwa nao wamejumuishwa tena.

Alisson na Ederson wanasalia kuwa miongoni mwa makipa, huku mabeki Thiago Silva, Marquinhos na Danilo wote wakirejea.


Wachezaji wawili wa Manchester United, Fred na Casemiro pia wametajwa.

**Kikosi kamili cha Brazil:**

Alisson (Liverpool), Ederson (Manchester City), Weverton (Palmeiras); Alex Sandro (Juventus), Alex Telles (Sevilla), Bremer (Juventus), Dani Alves (UNAM), Danilo (Juventus), Eder Militao (Real Madrid), Marquinhos (Paris Saint-Germain), Thiago Silva (Chelsea); Bruno Guimaraes (Newcastle United), Casemiro (Manchester United), Everton Ribeiro (Flamengo), Fabinho (Liverpool), Fred (Manchester United), Lucas Paqueta (West Ham); Antony (Manchester United), Gabriel Jesus (Arsenal), Gabriel Martinelli (Arsenal), Neymar (Paris Saint-Germain), Pedro (Flamengo), Raphinha (Barcelona), Richarlison (Tottenham), Rodrygo (Real Madrid), Vinicius Junior ( Real Madrid).

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,048,8
MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
CHELSEA
1 | 1.54
X | 4.24
2 | 5.28
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA KUSAINI MKATABA MPYA CITY



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City ina matumaini kwamba, Pep Guardiola, atasaini mkataba mpya kabla ya mwisho wa mwaka, kwa mujibu wa 90min.

Raia huyo wa Hispania, ambaye ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu England akiwa na City tangu achukue mikoba yake mwaka 2016, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2022/23, ingawa majadiliano ya kuongeza muda yamekuwa yakiendelea kwa miezi kadhaa.

Kwa mujibu wa 90min, tayari kuna 'makubaliano mapana' na wawakilishi wa Guardiola juu ya mkataba mpya ambao utamweka kwenye klabu hadi mwaka 2025.

Hata hivyo, 90min inaelewa zaidi kwamba City Group wameweka wazi kwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 51, kwamba angekuwa na nafasi katika klabu ya New York City FC ikiwa atataka.

Jina moja ambalo limejadiliwa ni Mikel Arteta, vyanzo vimeiambia 90min, anaonekana kuwa mshindani wa kweli wa kazi hiyo baada ya kuiongoza Arsenal kileleni mwa jedwali la Ligi Kuu.

Arteta anajulikana sana pale City baada ya kukaa miaka mitatu kama msaidizi wa Guardiola na maendeleo yake ya kushangaza katika Uwanja wa Emirates - ambayo yamemfanya ahusishwe na kazi ya juu huko Barcelona katika miezi ya hivi karibuni.

Julian Nagelsmann wa Bayern Munich na Marcelo Gallardo wa River Plate ni wengine wawili wanaoaminika kuwa kwenye rada za City, ingawa mabingwa hao wa Ligi Kuu wanatumaini kwamba Guardiola atasalia.

# Wamiliki wa Liverpool watangaza kuiuza

**LIVERPOOL, England**

WAMILIKI wa Klabu ya Liverpool ambao ni Fenway Sports Group (FSG), wametangaza kuiuza klabu hiyo.

Katika mabadiliko makubwa kwa wamiliki wa Marekani, ambao wamemiliki klabu hiyo tangu mwaka 2010, sasa wanakaribisha ofa kwa klabu hiyo.

FSG wamekuwa wamiliki wa klabu hiyo tangu Oktoba 2010, waliiponunua kutoka kwa George Gillett na Tom Hicks, lakini sasa inasemekana 'wanakaribisha ofa'.

Wakubwa wa benki za uwekezaji Goldman Sachs na Morgan Stanley wameripotiwa kuajiriwa kusaidia katika mchakato huo.

Katika taarifa iliyotolewa na Athletic, FSG ilisema "chini ya sheria na masharti sahihi" watakuwa tayari kuuza klabu hiyo.

"FSG imepokea mara kwa mara maneno ya nia kutoka kwa watu wengine wanaotaka kuwa wanahisa katika Klabu ya Liverpool," FSG iliandika.

"FSG imesema hapo awali chini ya sheria na masharti sahihi tutazingatia wanahisa wapya ikiwa ni kwa manufaa ya Liverpool kama klabu."



375,802/-

# CHAMA AZUIWA, KANOUTE KUIVAA SINGIDA STARS LEO

**Adam Fungamwango na Hadija Mngwai**

KIUNGO mkabaji Sadio Kanoute leo anatarajiwa kuwa dimbani kwa mara ya kwanza baada ya kuwa nje kwa mwezi mzima kutokana na kuumwa, wakati Simba ikiivaa Singida Big Stars kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, itakayochezwa Uwanja wa Liti mkoani Singida.

Wakati Msenegal huyo akirejea, timu hiyo itamkosa kiungo mshambuliaji wake, Clatous Chama, kutokana na kufungiwa mechi tatu na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), huko Kocha Juma Mgunda akisikitishwa na hilo kutokana na taarifa kuchelewa kutoka.

Pamoja na kuwa nje kwa mwezi mzima, Kanoute hajacheza Ligi Kuu kwa miezi miwili sasa, mara mwisho ikiwa ni Septemba 7, mwaka huu kwenye mechi dhidi ya KMC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu yake ikitoka sare ya bao 2-2.

Hakucheza tena mechi zilizofuata dhidi ya Prisons, Dodoma Jiji, Yanga, Azam FC na Mtibwa Sugar, ingawa alicheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika zote mbili dhidi ya Nyasa Big Bullets na Primeiro de Agosto za nyumbani na ugenini.

Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda amesema maandalizi ya kucheza mechi ngumu na timu bora ya Singida Big Stars, kwenye uwanja wake wa nyumbani yamekamilika.



"Tunajua mechi itakuwa ngumu kwa sababu Singida Big Stars ina wachezaji wazuri na benchi zuri la ufundi, lakini sisi tumeshajiandaa na hilo tunakwenda kutafuta ushindi," alisema kocha huyo huku akitangaza kuwakosa wachezaji wawili ambao ni Jimson Mwanuke na Israel Mwenda.

Hata hivyo, alisema Mwenda ameshaanza mazoezi mepesi kwa ushauri wa daktari, lakini Mwanuke ataanza mazoezi baada ya wiki mbili.

Kuhusu Chama alisema hapingani na kamati na wala kufungia wachezaji ambao wanakiuka sheria na kanuni, lakini wawe wanawafikiria makocha ambao wanakuwa wameshatengeneza mifumo ya uchezaji kwa wachezaji husika.

"Maamuzi kumbe yalikuwa yameshapatikana tangu tarehe nne mchana, kwa nini hawakutangaza? Unakuja kutangaza leo hii wakati tayari mchezaji umeshamuweka kwenye mipango na kutengeneza mfumo wa uchezaji, hii inatuumiza sana kama makocha, wangelisema mapema ili na sisi makocha tuangalie jinsi gani ya kubadilisha uchezaji, hii imetuathiri sana," alisema kocha huyo.

Naye mchezaji wa Singida United, Paschal Wawa, ameonyesha kufurahi kucheza dhidi ya timu yake ya zamani.

"Utakuwa mchezaji mzuri kwa sababu Simba ina wachezaji wazuri na sisi tuna wachezaji wazuri pia. Hatumuogopi mchezaji yeyote wa Simba, tutacheza ili kusaka ushindi na huwezi kusema mchezaji gani wa kumchunga kwa sababu ina wachezaji wengi wazuri na ni rafiki zangu, hivyo hatutakiwi kucheza kwa kumuogopa mtu, tunatakiwa kuwazuia na sisi kupata ushindi," alisema Wawa.

Timu hizo zinakwenda kucheza mechi hiyo zikiwa na pointi 17 kila moja, lakini Simba inashika nafasi ya pili kwa idadi kubwa ya mabao ya kufunga, Singida Big Stars ikiwa kwenye nafasi ya nne, lakini pia ikiwa imezidi mchezo mmoja.

# Simba Queens

INATOKA UK. 32

hisha mashabiki wote wa soka wa Simba na Tanzania.

" Tuko tayari, tunajua umuhimu wa mechi iliyoko mbele yetu, kila mchezaji anataka kuwa sehemu ya historia na mafanikio ya timu, tunaahidi kupambana mwanzo hadi mwisho wa filimbi," beki huyo alisema.

Timu zitakazoshinda zitatinga fainali itakayochezwa Jumapili na zitakazopoteza zitakutana kusaka mshindi wa tatu hapo Jumamosi.

# Yanga: Tutawashangaza

INATOKA UK. 32

Alisema presha ni kubwa lakini wachezaji wanapambana kutafuta ushindi katika mchezo huu jambo ambalo kwa pamoja wanaamini watafikia malengo.

Mchezaji muhimu wa kikosi cha kwanza ambaye Yanga itamkosa leo ni Shaban Djuma ambaye hakusafiri na timu kutokana na kuwa majeruhi, lakini Nabi amesema wana wachezaji wazuri sana akiwamo Kibwana Shomari anayeweza kucheza kwa ufanisi nafasi hiyo.

Alisema pia kwa upande wa kushoto anao Joyce Lomalisa na Faridi Musa, hivyo hana hofu yoyote kuhusu mtu sahihi katika nafasi hizo.

Kwa muda wote wakiwa kambini mjini Sousse, inaelezwa mbali na mbinu nyingine za kiufundi, Nabi alikuwa akisisitiza na kukifundisha kikosi chake kucheza kwa kasi kutokana na kufahamu uchezaji wa Club Africain ikiwa nyumbani.

Timu itakayosonga mbele itasubiri kujua wapinzani wake wengine watatu wakati hatua ya makundi itakapopangwa Jumatano ijayo katika Makao Makuu ya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), Cairo nchini Misri.

Yanga iliangukia katika michuano hiyo baada ya kutolewa Ligi ya Mabingwa Afrika raundi ya kwanza kwa jumla ya mabao 2-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Crystal Palace | 3.04 | 3.19 | 2.37 |
| 02. 12/11/22 | 18:00 | Bristol City vs Watford | 2.89 | 3.39 | 2.36 |
| 03. 12/11/22 | 18:00 | Bournemouth vs Everton | 2.78 | 3.23 | 2.53 |
| 04. 12/11/22 | 18:00 | Huddersfield vs Swansea | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 05. 12/11/22 | 18:00 | Preston vs Millwall | 2.41 | 3.13 | 3.03 |
| 06. 12/11/22 | 18:00 | Coventry vs QPR | 2.36 | 3.22 | 3.02 |
| 07. 12/11/22 | 20:00 | Basaksehir vs Galatasaray | 2.42 | 3.40 | 2.80 |
| 08. 12/11/22 | 20:00 | Sampdoria vs Lecce | 2.54 | 3.08 | 2.89 |
| 09. 12/11/22 | 20:00 | FC Sion vs St. Gallen | 2.80 | 3.60 | 2.37 |
| 10. 12/11/22 | 20:30 | Newcastle vs Chelsea | 2.32 | 3.34 | 2.99 |
| 11. 12/11/22 | 22:45 | Bologna vs Sassuolo | 2.38 | 3.34 | 2.89 |
| 12. 13/11/22 | 14:30 | Atalanta vs Inter | 2.90 | 3.54 | 2.29 |
| 13. 13/11/22 | 16:15 | FC Zurich vs Servette Geneva | 2.37 | 3.30 | 2.95 |
| 14. 13/11/22 | 17:00 | Istanbulspor vs Hatayspor | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 15. 13/11/22 | 17:00 | Kayserispor vs Konyaspor | 2.58 | 3.28 | 2.68 |
| 16. 13/11/22 | 17:00 | Montpellier vs Reims | 2.45 | 3.38 | 2.73 |
| 17. 13/11/22 | 17:30 | Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.44 | 3.41 | 2.72 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO- 09/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 4702 | Marines FC Gisenyi vs Gasogi United | 2.94 | 2.79 | 2.50 |
| 16:00 | 5006 | Bjelovar vs Lokomotiva Zagreb | 12.58 | 6.58 | 1.15 |
| 16:30 | 4335 | ES Hammam Sousse vs Esperance Tunis | 4.67 | 2.82 | 1.88 |
| 17:00 | 2526 | Paradou AC vs ES Setif | 2.54 | 2.78 | 2.88 |
| 17:00 | 2865 | CS Constantine vs MC Magra | 1.37 | 4.00 | 8.19 |
| 17:00 | 3260 | Singida BS FC vs Simba | 4.90 | 3.20 | 1.80 |
| 17:00 | 3530 | HB Chelghoum Laid vs MC Alger | 4.00 | 2.92 | 1.97 |
| 17:00 | 4073 | ASO Chlef vs CR Belouizdad | 5.43 | 3.20 | 1.66 |
| 18:00 | 4902 | Panetolikos vs Panathinaikos | 5.19 | 3.64 | 1.65 |
| 18:30 | 2124 | Petro Luanda vs CD Lunda Sul | 1.45 | 3.99 | 6.23 |
| 19:00 | 5531 | Atromitos vs Asteras Tripolis | 2.44 | 3.08 | 2.93 |
| 19:30 | 1997 | Vejle BK vs Horsens | 2.14 | 3.31 | 3.02 |
| 20:00 | 2032 | Thisted FC vs Copenhagen | 11.68 | 6.62 | 1.16 |
| 20:30 | 1404 | Sassuolo vs Roma | 3.32 | 3.42 | 2.06 |
| 20:30 | 2177 | FC Koln vs Bayer Leverkusen | 3.02 | 3.51 | 2.16 |
| 20:30 | 5400 | Lecce vs Atalanta | 4.38 | 3.48 | 1.77 |
| 21:00 | 1161 | AEK Athens vs OFI Crete | 1.23 | 5.81 | 11.01 |
| 21:00 | 2283 | Almeria vs Getafe | 2.16 | 3.19 | 3.39 |
| 21:00 | 4578 | Hapoel Beer Sheva vs Hapoel Hadera | 1.44 | 4.18 | 6.03 |
| 21:00 | 4708 | Levadiakos vs Olympiakos | 8.34 | 4.67 | 1.35 |
| 21:00 | 5117 | Sevilla FC vs Real Sociedad | 2.50 | 3.14 | 2.85 |
| 21:15 | 1118 | Hapoel Tel Aviv vs Beitar Jerusalem | 1.88 | 3.45 | 3.60 |
| 21:30 | 1874 | Sparta Prague vs Slovacko | 1.70 | 3.99 | 4.54 |
| 21:30 | 1950 | FC Wil vs FC Sion | 4.27 | 3.79 | 1.66 |
| 21:30 | 2544 | Hapoel Haifa vs Maccabi Haifa | 6.44 | 4.29 | 1.40 |
| 21:45 | 3588 | Vitoria Guimaraes vs FC Vizela | 2.05 | 3.26 | 3.26 |
| 22:00 | 2099 | Espanyol vs Villarreal | 3.04 | 3.19 | 2.33 |
| 22:00 | 2442 | Ajax vs Vitesse Arnhem | 1.12 | 8.50 | 14.83 |
| 22:15 | 2133 | Lausanne-Sport vs BSC Young Boys | 5.83 | 4.57 | 1.41 |
| 22:30 | 1648 | RB Leipzig vs SC Freiburg | 1.70 | 3.87 | 4.26 |
| 22:30 | 2698 | Eintracht Frankfurt vs Hoffenheim | 1.88 | 3.72 | 3.57 |
| 22:30 | 3670 | Union Berlin vs Augsburg | 1.53 | 4.07 | 5.56 |
| 22:30 | 4074 | FC Luzern vs FC Basel | 2.34 | 3.45 | 2.80 |
| 22:30 | 5182 | Schalke 04 vs Mainz | 3.22 | 3.57 | 2.04 |
| 22:45 | 1274 | Fiorentina vs Salernitana | 1.50 | 4.17 | 5.76 |
| 22:45 | 1487 | Arsenal vs Brighton | 1.75 | 3.58 | 4.49 |
| 22:45 | 1662 | Motherwell vs Celtic | 9.56 | 5.57 | 1.26 |
| 22:45 | 2100 | Newcastle vs Crystal Palace | 1.72 | 3.68 | 4.48 |
| 22:45 | 2832 | Rangers vs Hearts | 1.22 | 5.98 | 10.95 |
| 22:45 | 3776 | Inter vs Bologna | 1.30 | 5.35 | 8.13 |
| 22:45 | 3989 | Torino vs Sampdoria | 1.59 | 3.70 | 5.53 |
| 22:45 | 4136 | Southampton vs Sheffield Wed | 1.48 | 4.30 | 6.00 |
| 22:45 | 4251 | Wolverhampton vs Leeds | 2.25 | 3.44 | 2.94 |
| 22:45 | 4420 | West Ham vs Blackburn | 1.36 | 4.76 | 7.74 |
| 22:45 | 4562 | Nottingham vs Tottenham | 3.53 | 3.53 | 1.97 |
| 23:00 | 1021 | Manchester City vs Chelsea | 1.54 | 4.24 | 5.28 |
| 23:00 | 1468 | Liverpool vs Derby | 1.12 | 8.13 | 16.85 |
| 23:00 | 4280 | Mexico vs Iraq | 1.57 | 3.94 | 5.85 |
| 23:30 | 4324 | Mallorca vs Atletico Madrid | 3.65 | 3.10 | 2.11 |
| 23:45 | 5844 | GD Estoril vs Benfica | 8.60 | 5.08 | 1.27 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatano Novemba 9, 2022
Nipashe



UKURASA 31

## Chama azuiwa kuivaa Singida Big Stars leo

TUTAKIWASHA...



Wachezaji wa Simba Queens wakifanya mazoezi katika Akademi ya Fath Union Sport (FUS) nchini Morocco jana, wakijiandaa na mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns Ladies itakayochezwa leo jijini Rabat. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# YANGA: TUTAWASHANGAZA

## Yapania kufuzu makundi CAF ugenini dhidi ya Club Africain leo, Nabi asema...

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikishuka Uwanja wa Hammedi Agrebi Olympic jijini Tunis, Tunisia kuwavaa wenyeji wao, Club Africain kwenye mechi ya marudiano kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wawakilishi hao wa Tanzania, Nasreddine Nabi, amesema atawashangaza.

Yanga ilitua jijini Tunis jana jioni ikitokea mji wa Sousse ilipoweka kambi ya siku tatu kujiandaa na mchezo huo ambao inahitaji sare yoyote ya mabao ama ushindi ili kusonga mbele, na kama zikitoka suluhu, basi changamoto ya mikwaju ya penalti itaamua timu itakayosonga mbele kwenye michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

Katika mchezo huo, presha zaidi itakuwa kwa wenyeji ambao watakuwa na kazi kubwa ya kuhakikisha Yanga haipati bao la ugenini ambalo litawapa wakati mgumu wa kuongeza moja zaidi.

Lakini akizungumzia mchezo huo, Kocha wa Yanga, Nabi aliwataka mashabiki wa timu hiyo kutarajia 'sapraizi' kwa kuwa wamejipanga kupata matokeo.

Alisema presha ni kubwa, lakini anaamini nyota wake watapambana kuhakikisha wanatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

"Tumezungumza na mchezaji mmoja mmoja, na wameahidi kufanya vizuri, tunaamini mashabiki wetu wanasubiri kwa hamu kuona tunafuzu hatua ya makundi, kikubwa ni maombi tu," alisema kocha huyo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema huo ni mchezo mgumu na muhimu, lakini wanaamini kutokana na uzoefu wa wachezaji walionao watafanya vizuri na kuwafurahisha mashabiki.

"Kuna matumaini ya kupata matokeo mazuri, baada ya mchezo wa Al Hilal ya Sudan huu mchezo wachezaji wanauchukulia kwa umuhimu mkubwa lakini pia funzo," alisema.

INAENDELEA UK. 31

## Simba Queens na dk.180 ubingwa CAF

**Na Somoe Ng'itu, RABAT**

WAWAKILISHI wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kwenye michuano ya Ligi Mabingwa Afrika, Simba Queens kutoka Tanzania, wanatarajia kuwakabili Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini katika mechi ya hatua ya nusu fainali itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan hapa Morocco.

Mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 11:00 jioni ya hapa sawa na saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania na kufuatiwa na mchezo mwingine kati ya wenyeji ASFAR FC dhidi ya Bayelsa Queens kutoka Nigeria.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, alisema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kupambana katika mchezo huo ambao kwake anauona ni sawa na fainali.

Lukula alisema anahitaji kupata ushindi ili wakaribie kubeba kombe la michuano hiyo na si matokeo mengine.

"Tumebakiza dakika 180 ili kubeba Kombe la Afrika, tunajua mechi itakuwa ngumu, tunawaheshimu wapinzani wetu, tunajua ukubwa wao, hatutabweteka, tunafahamu wao ni mabingwa watetezi, lakini sisi pia tulijiandaa kuja kupambana katika mashindano haya," alisema Lukula.

Kocha huyo alisema anafahamu wapinzani wao wana safu nzuri ya ushambuliaji, hivyo wanajipanga namna ya kuwakabili huku akitarajia kuanzisha kikosi kitakachowazuia kutawala katika mechi hiyo.

Kocha huyo wa zamani wa She Corporate ya Uganda, aliongeza kuwa benchi la ufundi na wachezaji wake wanafahamu umuhimu wa mchezo huo kwa klabu na wao binafsi endapo wataibuka na ushindi.

"Tuko tayari kwa ajili ya kupambana, tunajua ni mechi ngumu na ni ya mtoano, tunataka kuweka rekodi nyingine ya kucheza fainali ya mashindano haya kwa mara ya kwanza, tuko imara na tunahitaji ushindi," alisema kocha huyo raia wa Uganda.

Nahodha Msaidizi wa Simba Queens, Fatma Issa 'Fetty Densa', aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wameahidi kucheza katika kiwango cha juu kwa sababu malengo yao ni kuweka historia mpya kwa CECAFA na Tanzania.

Fetty Densa alisema hatua ambayo timu yao waliyofika ni kubwa lakini wana uwezo wa kuendelea kuwafura-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >